Kikao cha Ishirini na Moja - Tarehe 13 Juni, 2014

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Ali Juma Shamuhuna (Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali):

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha mezani Hati ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka 2014/2015. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: (Kny: Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii):

Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, naweka Hati mezani makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka 2014/2015. Naomba Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

HOJA ZA SERIKALI

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea kama vile tulivyokubaliana jana. Nafasi ya kwanza kwa leo inakwenda kwa Mhe. Machano Othman Said - Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum, baadae atafuata Mhe. Waziri wa Fedha.

Mhe. Machano Othman Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Spika, awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuamsha salama siku hii ya Ijumaa, siku tukufu kabisa.

Pili naomba naomba nichukue nafasi hii kukushukuru na wewe Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii asubuhi hii ya leo. Mhe. Spika, naomba pia nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wao.

Mhe. Spika, wizara hii ni wizara muhimu sana katika nchi yetu lakini pia katika mawasiliano na miundombinu kwa wananchi wa nchi hii. Sasa mimi kabla ya kuanza kuichangia hotuba hii, naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Chumbuni naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia.

Mhe. Spika, mimi nitakwenda zaidi katika maeneo matatu au manne na nitazungumza kwa ufupi ili na Mhe. Waziri wa Fedha apate nafasi kabla ya wahusika kuingia. Lakini kwanza niipongeze wizara kwa kuendelea na miradi mikubwa ya kuimarisha huduma za mawasiliano.

Katika kitabu chao hiki wanayo miradi kama 14. Kati ya hiyo, 7 ni barabara kuu na mambo mengine. Mimi nitazungumzia miradi ya barabara, bandari na *airport*. Hiyo ndio miradi mikubwa niliohisi kwangu mimi na ambayo pia wenzangu wamezungumzia.

Mhe. Spika, katika mwaka 2005 kwenye kitabu cha ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, iliainisha barabara ambazo zitapewa kipaumbele kwa mwaka 2005-2010. Kwa upande wa Unguja na upande wa Pemba. Mathalani kwa upande wa Unguja barabara zilizoelezwa kuwa zitatengenezwa ni kama zifuatazo:-

- Mazizini/Fumba
- Mfenesini/Bumbwini

- Welezo/Dunga
- Tunguu/Kinyasini
- Makunduchi/Jambiani/Paje
- Mkwajuni/Nungwi
- Pongwe/Matemwe
- Paje/Pingwe
- Donge/Mkokotoni

Hizi ni kwa upande wa Unguja.

Kwa bahati nzuri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeweza kutekeleza vizuri ilani ya Chama cha Mapinduzi na barabara zote hizi zimeshatengenezwa.

Mhe. Spika, kwa upande wa Pemba baadhi ya barabara ambazo nazo zilikuwa katika ilani ni:-

- Mtambile/Kengeja/Mwambe
- Mtambile/Kangani
- Mizingani/Wambaa
- Chanjamjawiri/Tunduuwa
- Chanjani/Pujini
- Kenya/Chambani

Barabara za Mkoa wa Kaskazini Pemba ambazo mara hii bahati nzuri zimejengwa kwa kupitia ***MTC***. Mhe. Spika, kwa nini nimeanza hapa? Nimeanza hapa kwa sababu ninataka niwafahamishe Wajumbe wenzangu na wananchi kwa ujumla uzito na majukumu ya Wizara ya Miunndombinu na Mawasiliano. Juhudi ambazo wanachukua katika ufanyaji kazi wao.

Kwa bahati nzuri pamoja na uchache wa vifaa lakini kazi hizi wameweza kuzitekeleza. Lakini pia kuna baadhi ya wajumbe jana walivyokuwa wakichangia walisema kwa nini kuna baadhi ya mkoa wamepewa barabara mbovu na kuna wengine labda wamejipendelea.

Mhe. Spika, ukiangalia baada ya ilani ile ya Chama cha Mapinduzi, kasi kubwa ya utengenezaji wa barabara ilihamia Kisiwa cha Unguja. Kama nilivyozisoma zote ziliweza kumalizika lakini serikali baadae ikaona kwamba si vyema kuwa na kisiwa kimoja kikawa na barabara nzuri, kisiwa cha upande wa pili kikawa hakina barabara nzuri.

Kwa hivyo, Mkoa wa Kusini Pemba nao ukabahatika na kuna baadhi ya majimbo yana barabara za lami kuliko tatu ndani ya jimbo moja. Mfano wa Jimbo la Mkanyageni Pemba lina barabara nyingi tu za lami. Kwa hivyo Mkoa wa Kusini Pemba walibahatika kupata barabara za lami haraka kuliko Mkoa wa Kaskazini Pemba, ikiwemo barabara ya Mkoani/Makombeni, Mtukwao kupitia Mkanyageni.

Sasa ulipokuja mradi mwengine wa *MTC*, serikali ikaamua sasa kufanya maamuzi magumu. Maana kwenye *MTC* kulikuwa kuna barabara nyingi za Unguja na Pemba. Mfano kwa Unguja barabara ambazo mwanzo zilikuwa kwenye MTC lakini zikaondolewa ili kutoa nguvu kwa Pemba ni barabara ya Matemwe/Muyuni, Kichwele/Pangeni, Kizimbani/Kiboje, njia nne, Umbuji/Uroa, Fuoni/Kombeni, Koani/Jumbi, Jendele/Cheju Kaebona na Jozani/Ukongoroni.

Bahati nzuri nyengine tayari zimepata wafadhili wengine zinajengwa. Kwa hivyo miradi hii ikaamuliwa iende Pemba, kama Bahanasa/Mtambwe na zile nyengine zilizotajwa. Kwa hivyo wamepata barabara nzuri kwa sababu walikuwa pia ni watu mwisho katika mradi wa serikali katika kuimarisha miundombinu ya barabara. (*Makofi*).

Kwa hivyo, hata kule Kusini Pemba ambako kuliambiwa barabara mbovu, hakukupelekwa barabara mbovu, zipo barabara na zinaendelea kufanya kazi. Sasa kwa bahati nzuri niliwahi kuwa Waziri wa wizara hii. Ninataka nizungumzie kidogo historia ya barabara sita za vijijini Kusini Pemba. (*Makofi*).

Mhe. Spika, barabara hizi ni msaada wa Norway. Wakati wa msaada huu kulikuwa kuna miradi miwili. Kuna mradi wa barabara na mradi wa umeme Tanga/Pemba. Fedha hizi zilikuwa hazitoshi kwa miradi yote miwili. Norway wakazungumza wakasema basi chagueni mradi gani mufanye.

Serikali kwa kujua tatizo la wananchi wa Pemba la umeme, ingawa watu wengine walikuwa hawaamini kama mradi ule utawezekana, ikaamua fedha nyingi ziende katika mradi wa umeme Pemba/Tanga na umesaidia sana. Tuliamua hivyo kwa sababu tunajua kwamba unaweza ukajenga barabara moja moja, lakini huwezi kufanya umeme nusu nusu. Kwa hivyo, wao Norway nao wenyewe wakakubali na kuwa baada ya mradi wa umeme umeanza, nao wakasema na barabara tutasaidia ingawa kwa fedha kidogo.

Sasa mazungumzo yakaendelea pande mbili, kati ya SMZ na Norway kwamba hizi barabara za Kusini kwa uzito na zinavyopita gari, ziwe kwa *labour cost*, yaani wananchi watoe huduma, serikali inunue vifaa na barabara zijengwe. Barabara hizi Mhe. Spika, zimejengwa kwa lami baridi, hazikujengwa kwa lami moto.

Kila barabara ina muda wake wa matumizi. Lakini sote mimi ninataka tujiulize. Hivi nani kabla ya ujenzi wa barabara hizi aliweza kwenda Wambaa. Mimi mwenyewe mara nyingi nimekwama njiani kwa kwenda Wambaa. Kutoka Mtambile mpaka Kangani ulikuwa unachukua masaa matatu au manne. Leo Mtambile/Kangani unatumia si chini ya dakika 10 au 15. Mtambile kwenda Mwambe ilikuwa zaidi ya saa moja au masaa mawili, halafu Kenya/Chambani ni kilomita tatu tu lakini ulikuwa unaweza kutumia masaa mawili.

Kwa hivyo, mimi niwaombe Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu kwamba ni vyema wakati mwengine tunapochangia hapa na tutoe shukurani kwa serikali, kwa sababu serikali imefanya mambo mema na mengi. (*Makofi*)

Katika miaka ya 1980 mpaka ya mwanzoni ya 2000, barabara zetu zote karibu zilikuwa zimekwisha na sisi tuna bahati Zanzibar, wenzetu hata Tanzania Bara kuna wilaya haina hata kilomita moja za lami, sisi hakuna wilaya Zanzibar ambayo haina barabara ya lami.

Kwa hivyo nilitaka kuzungumzia sehemu ya barabara katika suala hilo. Lakini katika sehemu hii ya barabara na mimi naomba niungane na wenzangu kwamba niiombe Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano wafanye maamuzi magumu. Wakati ninazungumza nilisema tulizifuta barabara za Unguja kupeleka Pemba Kaskazini ili nao wao kule tutoe uzito wa shughuli za maendeleo.

Sasa naomba wizara hii ifanye maamuzi magumu kwa barabara mbili. Kwanza wafanye bidii na maarifa yao yote barabara ya Kijini waimalize. Shughuli za kuanza ninajua wameanza lakini barabara ya Kijini waimalize. Mazungumzo yaliyozungumzwa na Wajumbe hapa ni ukweli kwamba Kijini ni kijiji ambacho kipo nyuma kimaendeleo. Ninamkumbuka Mwakilishi aliyepita Mhe. Ame Mati, aliwahi kusema kwamba kutokana na kutokuwa na maendeleo katika kijiji kile, maana anasema umeme hakuna, maji hakuna na barabara hakuna, vitanda vyenyewe vya kamba, alitwambia hivyo hivyo. Kwa hivyo watu wanazaana sana kwa sababu vitanda vyenyewe vyote vinakuwa na shimo na wote ni lazima walale pamoja.

Sasa hili, serikali yetu kupitia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano Kijini waijenge ile barabara. Lakini barabara nyengine ambayo naiombea nayo pia imalizwe ya Mgagadu/Kiwani. Barabara ile ina miaka kama saba sasa, ina kilomita tano. Kwa hivyo Mhe. Waziri kwa upande wa Pemba basi barabara hii ninafikiri uipe kipaumbele ili iweze kumalizwa kwa kiwango cha lami kama ilivyokubaliwa. Hilo ni kwa upande wa barabara.

Mhe. Spika, ninataka nizungumzie pia suala la bandari kidogo na zaidi katika bandari nimpongeze Mkurugenzi na timu yake kwa juhudi kubwa za kuimarisha bandari yetu. Kama miezi tisa tu, yaani mpaka Machi wameweza kupita lengo la bilioni kumi na mbili na kufika bilioni kumi na nne, basi nina hakika pengine mpaka Juni wanaweza kufika bilioni kumi na tano na mpaka kumi na sita. Haya ni mafanikio makubwa sana katika utawala na *management* ya idara, pamoja na bodi yao ya Ukurugenzi ya Shirika la Bandari.

Sasa hivi wana juhudi ya kutafuta eneo la kuweka makontena na ninafikiri jana Mhe. Hamza Hassan Juma alisema kwamba mule ndani mutumike kwa ajili ya makontena na mimi ninaunga mkono suala hilo. Lakini pia kwa kupitia shirika hili ingawa ni mradi wa serikali ninawapongeza sana kwa mradi wa bandari mpya ya Mpigaduri. Bandari hii ndio itakayokuwa ukombozi wa nchi yetu katika mambo ya kiuchumi.

Juhudi ambazo Mhe. Waziri wa Fedha anazichukua kwa bandari hii tunaziona. Tumezungumza sana kwenye Baraza la Mapinduzi na hapa pia amezungumza, na hatua iliyofikiwa sio mbaya. Naomba tuwape msaada wote unaohitajika kwa wizara zote na wananchi wa Zanzibar, yaani tunapofanya mradi mkubwa kama huu basi kuna mambo madogo madogo ya kujitolea wananchi nao waone kwamba haya ni sehemu yao katika kujenga nchi yao. Huu ni mradi mzuri ambao utatusaidia sana.

Mhe. Spika, sasa naomba nimalizie kwa kuzungumzia Mamlaka ya Usafiri, yaani Mamlaka ya Anga Zanzibar. Mhe. Spika, mamlaka hii imezungumzwa sana lakini ninafikiri itakuwa ni mara ya pili kwa kusema kwamba mimi bahati mbaya, sikupata kufanya kazi na mkurugenzi huyu wa sasa hivi, kwa sababu alipoingia yeye mimi nimeshaondoka. Lakini ninahisi utendaji wake ni mzuri sana, kwa nini ninasema mzuri? (*Makofi*)

Ukenda sasa hivi *airport* kumebadilika sana na *airport* na bandari ni milango mikuu lakini kunatofautiana. Bandari kwa maumbile ni sehemu ya ghasia nyingi sana kwa abiria na mizigo. Lakini airport zote duniani ni sehemu nyeti, ingawa nako ni lango kuu lakini ni sehemu nyeti na kuna mambo pia yanakuwa na taratibu zake.

Kuna kipindi bandari kuna mashirika matano ya wachukuzi lakini hapa *airport* kulikuwa kunatakiwa kuwe na kampuni mbili. Sisi tulikataa tukasema haiwezekani kwa airport. *Airport* ni lazima ibakie kampuni moja tu. Kwa sababu *airport* ni eneo nyeti. Sasa na haya yanayofanyika sasa hivi, mimi naona kwamba labda pengine inatakiwa elimu kati ya Waheshimiwa sisi, maana na sisi tuna mipaka, hatupo juu ya sheria Waheshimiwa.

Sisi tunatakiwa labda tupate elimu ya kuelewa mazingira ya viwanja vya ndege yanakuwaje. Mhe. Spika, ninafikiri unaweza ukatayarisha semina hata sio kwamba ya fedha, hata ikiwa bure lakini ije pengine *management* ya *airport* na Waheshimwa Wawakilishi tuwepo tuelezane kama kuna kasoro ziwekwe sawa, lakini kiukweli tusimvunje moyo mkurugenzi anafanya kazi yake vizuri.

Anafanya kazi vizuri na wanaendelea vizuri, hata pale ukipita utaona hivyo. Isipokuwa nina ombi kwamba katika uwanja wetu wa kimataifa. Humu wamezungumzia suala la kumalizia uzio, uzio ni jambo muhimu katika masharti ya kimataifa kwa usalama wa abiria. Kwa hivyo naomba suala hili nalo, wizara imsaidie au isaidie mamlaka ile iweze kumaliza suala la uzio.

Ninajua kwamba mamlaka inapata fedha kutoka *airport*. Kuna kodi mbali mbali lakini sio kodi zote ambazo zinachukuliwa na mamlaka. Kuna kodi nyengine zinakwenda moja kwa moja katika serikali kuu kama bandarini. Kuna kodi zinakwenda serikali kuu moja kwa moja na airport hivyo hivyo kuna kodi zinakwenda serikalini moja kwa moja. Kwa hivyo ninajua mapato ambayo wanapata mamlaka bado hayawezi kukidhi mahitaji ya matumizi yao.

Mhe. Spika, la mwisho niseme kutokana na hizo gharama kuwa kubwa, basi ule mpango wa serikali, ninafikiri waziri asimamie uende kasi wa *PPP*, kwamba hata pale *airport* kuna maeneo. Kwa sababu itakuwa ni shida sana kila siku serikali kununua *X-ray* na vile vifaa vya ulinzi. Vifaa vyao vina gharama. Kwa hivyo ifike wakati kuna shughuli nyengine ziachiwe zitafanya taasisi binafsi katika kuendeleza uchumi wetu.

Mhe. Spika, baada ya hayo, mimi ninaunga mkono kwa asilimia mia. Naomba Waheshimiwa Wawakilishi, wizara hii ni ngumu tuwasaidie, bajeti yao tuipitishe ili tuwape majukumu kwa mwaka mwengine wa kifedha.

Mhe. Spika, ninakushukuru sana. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum, Mhe. Machano Othman Said. Sasa naomba nimkaribishe Mhe. Waziri wa Fedha.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, kwanza na mimi nataka nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Vile vile nataka niwapongeze Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa kazi nzuri wanayoifanya, wakiongozwa na waziri wao Mhe Rashid Seif Suleiman, pamoja na Naibu Waziri Mhe. Issa Haji Ussi Gavu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nataka niseme kwanza kwa kutoa takwimu ili waweze kuona wenzangu juu ya umuhimu wa wizara hii. Mhe. Spika duniani kote Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ni moja ya wizara muhimu sana na hata hapa

kwetu kwa sababu ya *nature* yake ya kukuza uchumi. Utakapotekeleza majukumu yaliopo chini ya wizara hii, basi unakuza uchumi na hiyo ndio nia ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, wizara hii nayo inakazi ambazo mahitaji ya fedha ni makubwa mno. Nitatoa mfano, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali unaweza kusema unawapa milioni 100 wakajenga madarasa, wizara hii milioni 100 miradi yake hakuna watakachoweza kukifanya. Miradi yake ni ujenzi wa barabara kilomita 1 ni zaidi ya milioni 900, miradi yao ujenzi wa bandari, miradi yao ujenzi wa viwanja vya ndege. Kwa hivyo, wanahitaji fedha nyingi sana wizara hii. Ndio maana hata Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, imeliona hilo na ndio imewawekea fedha nyingi. Nataka nitowe takwimu hapa nilizonazo.

Mhe. Spika, ukiangalia wizara hii katika fedha tulizowapa za *recurrent*, katika bajeti ya kawaida bilioni 5.7. Katika matumizi ya kawaida hii wizara ni ya saba kwa bajeti ya *recurrent* ni ya saba bilioni 5.7 imepitwa na Wizara ya Afya, imepitwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, imepitwa na Wizara ya Kilimo na Maliasili, imepitwa na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, imepitwa na hata Hospitali ya Mnazi Mmoja. Maana yake nini, maana yake haina watendaji wengi, ndio maana tumewapa bilioni 5.7 za *recurrent*.

Mhe. Spika, hebu tuangalie fedha za maendeleo. Wizara hii ni ya kwanza kupewa fedha za maendeleo bilioni 160.1. Sasa hebu angalia wa pili wake ambae ni Wizara ya Afya bilioni 28. Huyu ana bilioni 160.1 na wa pili ana bilioni 28 katika maendeleo, hii ni kwa sababu ya umuhimu wa hii wizara na kama nilivyosema wizara hii haiwezi kuikachukua shilingi milioni 100 ikafanya kitu. Kwa hivyo, wizara hii kwa kweli hata na upande wa serikali, kinachogomba Mhe. Spika, ni upatikanaji wetu wa mapato.

Mhe. Spika, juzi nilijibu hapa nikaeleza kwamba upatikanaji wetu wa mapato unategemea zaidi wafadhili, na pale ambapo wafadhili wanapopunguza mapato yao na huku lazima matumizi lazima yapunguwe, hilo ndio tatizo. Lakini mimi nawapongeza sana, wizara inafanyakazi nzuri na nitajaribu kuzisema baadhi ya kazi ambazo wamezifanya na mpaka sasa hivi wako hatua gani.

Mhe. Spika, kulizungumziwa suala la Bandari ya Mpigaduri. Mhe. Spika, siku zote *paper work* haionekani. Unapotaka kutekeleza mradi kwa kutumia mikopo au msaada, ni lazima hizi kazi za makaratasi zianze mwanzo. Kuna vitu mnaanza na *feasibility study*. Hiyo *feasibility study* inakwenda inabidi iboreshwe na wataalamu wa ndani na wataalamu wa nje. Mkimaliza hapo kuna *paper work* za kutafuta wapi mkatafute hiyo mikopo au misaada, mabarua ya kuandikiana yanachukua muda nayo, unakwenda unarudi waziri wa sekta, Waziri wa Fedha nenda rudi inachukua muda. Kwa hivyo kazi hizi tunapokuwa tunazifanya ndani ya serikali hazionekani kweli. Lakini mimi nataka niseme kwamba tunafanya kazi.

Mhe. Spika, Bandari ya Mpigaduri mchoro tayari, *feasibility study* iko tayari, barua ya kuomba fedha iko tayari, *Exim* China tumeshazungumza nao na ninamshukuru sana ndugu yangu somo yangu Mhe. Omar Ali Shehe, alisema jana kwamba miradi hii ni mikubwa kwa serikali peke yake, hebu tujaribuni kwenda *PPP*. Huu ni mradi wa kwanza Tanzania utakaokwenda *under PPP*, na wenzetu Wachina benki ya *Exim* wamefurahishwa sana na Zanzibar, kwa kuona kwamba tuna-*embark under PPP*. Tunatarajia mambo yakienda kama tulivyoyapanga, maana juzi tu mimi nilikuwepo China nilikwenda kuzungumza na watu wa *Exim Bank*. Ni lazima tusafiri, tunasafiri kwa sababu ya kazi. Tumezungumza na mambo kama yatakwenda vizuri basi tunategemea kwamba mradi huu mwisho wa mwaka tutapata saini.

Mhe. Spika, mimi namshukuru sana Mhe. Mjumbe mmoja hapa aliyesema kwamba tujitahidi tusimamie, nadhani ni Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Mkoani kwamba tufuatilie kwa karibu zaidi mradi huu, ili tuweze kuupata na ndio jukumu letu. Kwa hivyo, mradi huu sasa hivi hakuna *document* hata moja sasa hivi inayolala Tanzania; *documents* zote za mradi huu ziko China, zinapitiwa na zikishakupitiwa watatuambia kwamba sasa mkopo uko tayari twende tukasaini ili tuweze kupata fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Kwa hivyo, nawaambia ndugu zangu kwamba tunasubiri, lakini tunafuatilia.

Mradi mwengine ambao ulizungumziwa ni uwanja wa ndege wa Pemba. Ni kweli. Mimi nataka niseme tu Mhe. Spika, kwamba huko mbele ni kugumu nako. Kuna wajumbe wenzetu wawili humu ndani wana uzoefu wa mbele na nyuma. *(Vicheko/Makofi)*

Kwa maana ya *backbenchers* na kwa maana ya uwaziri. Mhe. Rashid Seif Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, alipokuwa *backbencher* alifikiria ni rahisi, lakini Mwenyezi Mungu kamjaalia sasa hivi yuko mbele, kugumu huku. *(Vicheko/Makofi)*

Kwa hivyo, ninachokuombeni ndugu zangu, tusiwe tunamlaumu huku ni kugumu. Mhe. Hamza Hassan Juma alikaa mbele, sasa yuko nyuma, hata maswali yake kama mnamsikiliza Mhe. Hamza ni ya tahadhari, kwa sababu anakuelewa mbele. *(Vicheko/Makofi)*

Kwa hivyo, ndugu zanguni nataka niseme kwamba huku ni kugumu sana. (*Vicheko/Makofi)*

Wajumbe: (Wajumbe walizungumza nje ya kipaza sauti). (*Vicheko/Makofi)*

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, sina nia hiyo waliyoikusudia wajumbe wenzangu. *(Vicheko/Makofi)*

Mhe. Spika: na mimi nashangaa, kwa sababu lugha yako iko safi na iko wazi, lakini naona. Endelea Mhe. Waziri. *(Vicheko/Makofi)*

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, nataka niwahakikishie wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba Mhe. Rashid Seif anafanyakazi kweli na sisi wenzake tunamsaidia sana na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atamsaidia ili aweze kutekeleza majumu yake chini ya wizara hii. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tumeunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa sababu tuna utaalamu wa pande zote, CCM na Chama cha CUF. Kwa hivyo, ndugu zangu wajumbe tunapokaa hapa kwa kweli huku mbele ni kugumu sana, kwa hivyo tunafanya kazi. Uwanja wa Ndege wa Pemba ni kweli hoja ililetwa ya kuweka taa na kweli Waheshimiwa Wajumbe mnachokizungumza kwamba ikitokea dharura uwanja ule hauna taa, ni kweli. Serikali imeona kwamba ni vyema kutafuta pesa na kuweka taa.

Bajeti iliyokuja kwenye Wizara yetu ya Fedha zinahitajika bilioni tatu. Lakini sio muda mrefu wenzetu wa Benki ya Uturuki *Exim*, waka-*respond* kwamba sasa tuko tayari na mazungumzo na serikali kuhusu ujenzi wa uwanja wa ndege wa Pemba. Tungeweka taa zile na kule kuna bajeti ya taa, basi taa zile zingekuja zikafumuliwa, ingekuwa tunaitia hasara serikali. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa hivyo sisi tukaona kwamba twende na benki ya Uturuki tuchukue mkopo wa kibiashara, ili tuweze kuujenga uwanja wa ndege wa Pemba; tuujenge kama uwanja wa ndege mwengine, sio tuuweke vijitaa tu kwa pembeni, tuujenge hasa. Jengo, *runway*, tuongeze *fence*, tuongeze *fare* na tuongeze kila huduma pale.

Waheshimiwa Wajumbe, hivi sasa nataka niwaambieni *feasibility study* imeshaletwa na imeshapitiwa na wataalamu wa Zanzibar, wataalamu wa Uturuki sasa tunawaita waje wapitie *comments* zetu. Tukimaliza hapo, benki tumeshazungumza nao na tayari Serikali ya Muungano imeshatoa barua kupeleka benki ya Uturuki kwamba tunataka mkopo huo kwa ajili ya uwanja wa ndege wa Pemba.

Hivi sasa wataalamu wa Uturuki wakimaliza kufanya kazi na wataalamu wetu, tunakwenda tena kumaliza mazungumzo na Benki ya Uturuki. Tunataka bandari ya Unguja na uwanja wa ndege Pemba, vianze sambamba ujenzi wake. Kazi zinakwenda na nia yetu ni kuwatumikia wananchi wetu. Najua Waheshimiwa Wajumbe wako Mhe. Spika, wanahoji kwa nguvu kwa sababu wanataka kuona tunawatumikia wananchi. Nasema tutaendelea kuwatumikia wananchi wetu mpaka mwisho wa damu yetu.

Mhe. Spika, kuhusu uwanja wa ndege wa Zanzibar umezungumzwa sana. Nasema hivi, tungeubomoa ule uwanja, ilikuwa ni jukumu letu sisi serikali kusema kama tunataka kuubomoa, lakini tumeshatoa milioni 35 dola, faida yake ni nini zile zingekwenda, ingekuwa ni hasara tu kwa serikali.

Mhe. Spika, nilisema katika kipindi kilichopita kuwa, mshauri ametoa maelekezo ya kuurekebisha na mshauri wetu ametoa maelekezo mazuri zaidi, ule uwanja kuu-*design* vizuri zaidi. Uwanja ule mwanzo *design* yake ya mwanzo haikuwa hata na *lobby*, sasa hivi umekuja na *lobby*. Tungeubomoa ule uwanja na tukajenga upya, basi gharama yake ingekuwa zaidi ya dola milioni 170 na muda sasa ungekwenda, lakini baada ya kuurekebisha ule uwanja na kuongeza *design* kidogo na kuufanya uwe mzuri, imeongezeka kama dola milioni 50.

Kwa hivyo, mimi nasema bado na sasa hivi ndugu zetu wa Kichina wapo *on the ground* wanaendelea na ule mradi na juzi tulikuwepo China, tumeshamaliza mazungumzo ya *addendum* na *extension* na mazungumzo ya kupata fedha zaidi. Tayari tumekubaliana na ndugu zetu wa China watatukabidhi *terminal* ile ifikapo mwezi wa *September* mwakani, sio mbali. Kwa hivyo, bado tunafanya kazi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, suala jengine ambalo lilizungumzwa ni suala la Mashirika ya Muungano kama yanatupa mgao wetu. Nataka niseme kwamba bado hawajaanza kutoa mgao, lakini mazungumzo yanaendeleo, hata *payee* ilichukua muda vile vile, hata gawio la *BOT* lilichukua muda vile vile. Lakini sasa *payee* inaletwa, gawio la *BOT* linaletwa na haya tuna imani kwamba tutafanikisha. Tunaomba twende taratibu, twende na nguvu za hoja na mwisho wake tutapata haki yetu.

Mhe. Spika, ilikuja hoja ya hesabu na bajeti za mashirika. Nataka niseme kwamba Kamati ya *PAC* ina haki ya kupewa *statement of account* na mashirika yote ya serikali. Ina haki hiyo na kama wataiomba shirika likikataa kuwapa basi waje kuripoti kwangu; waniambie shirika fulani wamekataa kutoa na wana haki hiyo ya kutazama *account* na hesabu zao; hizi sio za kufichwa yale ni mashirika ya umma, isiwe shirika lenyewe linataka kuficha ficha hapana. Mwenyekiti wa *PAC* namuomba sana, aombe apewe.

Mhe. Spika, imejitokeza hoja pale ya safari zetu na hili liliulizwa sana. Mimi nasema kweli, serikali tumesema kwamba tupunguze safari, lakini hatujasema kuwa tusitishe safari.

Pia ilikuja hoja kuhusu habari ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Miundombinu kusafiri sana. Mimi mwaka huu nimeshasafiri naye safari tatu, lakini ilikuwa ni lazima niende naye kwa sababu kuna kesi za kitaalamu hizi ni lazima anisaidie.

Nataka nikuhakikishieni Mhe. Spika, hakuna hata senti moja tuliyotumia ya SMZ. Tulikwenda na mashirika yenyewe ndio yaliyogharamia na tukenda tukafanya kazi. Kwa hivyo, mimi nasema kwamba kupunguza safari ni muhimu na kufanya kazi ndani ya wizara ni muhimu, wala siwakatalii Waheshimiwa Wajumbe. Lakini na safari nazo zilizokuwa ni za lazima nazo ni muhimu. Kama waziri anakwenda safari, haelewi tija ya safari anazokwenda hilo ni tatizo lake yeye mwenyewe binafsi. Kwa hivyo, mawaziri kama wale ni lazima tutawabana, hatutumii pesa za umma kwenda kutembea tu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, jengine ambalo nilitakiwa nijibu na hili lilikuja kwa ujumla wake na ndugu yangu Mhe. Ali Salum Haji, alitaka nieleze hasa kuhusu hawa *ZAT*. Mhe. Spika, *ZAT* ni kampuni ambayo inatoa huduma pale uwanja wa ndege. Kampuni hii ina kodi inatakiwa ilipe, kodi za wafanyakazi wanaita wenyewe *payee*, nataka niseme wanalipa kila mwezi. Kodi ya Kampuni, mapato ya kampuni wanalipa kupitia *TRA (Makofi)*

Mhe. Spika, tatizo la kampuni hii ilikuwa kodi inayotokana na faida ya asilimia 5, walikaa kipindi hawakuwa wakilipa ni zaidi ya miaka 16, kampuni hii haikuwa ikilipa. Mhe. Spika, mimi nimeingia madarakani baada ya miaka 2 nikakuta kesi ya kampuni hii. Nikamwambia Mkurugenzi wa Mamlaka ya Anga, kwa nini huniandikii unasema tu kwa mdomo, serikali inafanya shughuli zake kwa karatasi. Niandikie ulete malalamiko yapo dhidi ya kampuni hii. Hapa ndipo nilipoambiwa ugomvi ulipoanzia baina ya mamlaka na kampuni.

Aliponiandikia na mimi sikusita nikamwita Mwenyekiti wa Kampuni, nikamwambia Mwenyekiti wa Kampuni unadaiwa. Asilimia 5 inayotokana na faida hujalipa. Nikamwambia kwanza nataka unilipe hizi ambazo mamlaka inazokulalamikia, milioni 440 na nikamuandikia barua nikampa siku tano.

Mhe. Spika, namshukuru Mhe. Raza ndio Mwenyekiti wa Kampuni. Katika muda wa siku tano alikuja kuniambia Mhe. Waziri nimesha-*deposit* pesa zenu milioni 440 kwenye *account.* Nikawatuma vijana wangu wakatizame kwenye *account*, wakakuta milioni 440 zipo. Lakini nikawatuma vijana wangu wafanye *ruffle estimate* kampuni hii tunaidai milioni 440 tu. Wakaniambia bado kwa mahesabu ya haraka haraka kampuni hii inadaiwa zaidi. Nikamwita tena Mwenyekiti, kwa bahati nzuri Mwenyekiti ni mjumbe hapa ni Mwakilishi wa Jimbo la Uzini. Mimi sitaki niseme akiwa hayupo, nimefurahi sana alipoingia, maana yake mwanzo nilimtazama hayupo na hili suala lake nimeliweka mwisho, ili anisikie hasa, asije akaambiwa kama nimesema tofauti na nikamwambia Mhe. Mohamedzara Hassanali Mohamedali nakuandikia nataka unilipe tena shilingi milioni 450 halafu tutakuja kufanya hesabu. Mhe. Spika, barua yangu ya mwanzo nilimpa siku tano na barua ya pili nilimpa siku tatu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ninamshukuru sana Mwenyekiti wa *ZAT* ali-*deposit* shilingi milioni 450. Kwa hivyo, nilimwambia sasa hizi sikudai kwanza mpaka nikamilishiwe hesabu. Sasa vijana wangu ninawaambia waende wakafanye kazi na Kampuni ya *ZAT* wakipitia kwenye *accounts* zao, ili tuone faida walioipata kwa muda wa miaka 16.

Vile vile kuna taarifa kwamba waliwahi kulipa awali dola laki tano na hiyo nimewaambia nataka nione risiti na wakesha kuniletea hesabu kamili tutajua nani anayemdai mwenzake na nani hadaiwi. *(Makofi)*

Kwa kweli kampuni hii ilikuwa hailipi kwa sababu sisi tulioachiwa majukumu hatukutaka walipe, yaani hatukuwafuatilia na huo ndio ukweli na wala tusifike pahala tukawa tunalaumu tutayafukuza haya makampuni. Kwa mfano, leo mimi nimekuja na zimelipwa na wala sina ugomvi na Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali, kwa sababu anajua ni haki ya serikali kama Mwenyekiti wa Kampuni ya *ZAT*. *(Makofi)*

Mhe. Spika, namalizia kwa kusema kwamba fedha shilingi milioni 890 ziko kwenye *account* na nimewaambia Mamlaka nataka kuzitumia kwa ajili ya kununulia *X-Ray machine*, kwa sababu suala hili limezungumzwa sana hapa kwamba taratibu za *procurement* zimekiukwa. Nimewaambia watu wangu wakafanye *audit*, ili waangalie kama zimekiukwa wafute utaratibu ule. Kwa hivyo, hatuwezi kwenda kienyeji kama hivi, kama taratibu za ununuzi zimekiukwa wafute na tumeshawahi kufanya hivyo.

Kwa mfano, taratibu za manunuzi zilikiukwa kwenye Kiwanja cha Kufurahishia Watoto tukafuta na tukaitisha *tender* upya, lazima tuheshimu sheria, kwa sababu hawa Wawakilishi wanapopiga kelele Mhe. Spika mengine wanakuwa na sababu za msingi na wala hatuwezi kuyadharau kama serikali. Kwa hiyo, shilingi milioni 890 ziko kwenye *account* ya Hazina na wala hazijatumika. Vile vile ninaipongeza sana Kampuni ya *ZAT* inafanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ninamalizia kwa kusema kwamba ninaiunga mkono bajeti ya wizara hii ya Miundombinu na Mawasiliano kwa asilimia mia moja. Vile vile ninawaomba sana wenzangu Waheshimiwa Wawakilishi kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba tuiunge mkono na Mhe. Rashi Seif Suleiman (Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano) huu ni mwaka wake mmoja tumempa bajeti mwaka jana, hivyo tuiunge mkono, ili aweze kwenda kutekeleza majukumu yake tukishirikiana na sisi wenzake. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba nimalizie kwa kukushukuru sana na ninawaomba sana wenzangu kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba tuiunge mkono bajeti hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa naomba tumkaribishe Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, lakini nategemea kwamba tutakuwa watulivu na tusikie kinachozungumzwa kuanzia maelezo aliyoyatoa Mhe. Machano Othman Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum), Waziri wa Fedha, Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano pamoja na Mhe. Waziri mwenyewe wa Miundombinu na Mawasiliano yote ni sehemu ya majumuisho kwa hotuba hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, naomba na mimi nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujaalia uzima wa afya, pia tukiwa tupo hapa katika kutimiza wajibu wetu wa kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

Aidha, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru wewe binafsi Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu katika bajeti ya Wizara hii ya Miundombinu na Mawasiliano.

Mhe. Spika, kabla ya kusema mengi naomba nichukue nafasi hii mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wenzangu wa Jimbo la Chwaka niseme kwamba ninaunga mkono hotuba ya bajeti hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mchango wangu utajielekeza katika kutoa ufafanuzi wa baadhi ya mambo, ambayo yameulizwa na Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wa Baraza lako hili tukufu katika kuona shughuli za utendaji na taarifa zinazohusiana na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano.

Kwa kuanzia kulikuja hoja iliyozungumzia suala la ongezeko la makadirio ya makusanyo kutoka mwaka 2014/2015. Mhe. Spika, makusanyo yaliyoripotiwa yalikuwa ni kwa ajili ya miezi 9 hadi kufikia mwezi wa Machi, matarajio yetu ni kuweza kufikia lengo lililowekwa itakapofika mwisho mwa mwezi wa Juni mwaka 2014 na hii ilikuwa ni katika Shirika la Bandari na liliulizwa na Mhe. Panya Ali Abdalla.

Suala la pili lilikuwa ni kuwapatia wataalamu Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ya wizara. Mhe. Spika, wizara kupitia mpango wa mafunzo inaendelea na kuwapatia mafunzo wafanyakazi wanne wa idara hii fani ya uchumi na usimamizi wa miradi ngazi ya shahada ya pili, kwa ajili ya kuwajengea uwezo wafanyakazi hao, ili waweze kutekeleza vyema majukumu yao ya idara.

Aidha, katika bajeti ya mwaka 2014/2015 wafanyakazi wengine zaidi ya hao wanne wa idara hii watapatiwa mafunzo ya shahada ya pili, ili kuimarisha zaidi idara hii katika ufanyaji wa kazi kwa ufanisi mkubwa zaidi. Mhe. Spika, ongezeko hili linatokana na shughuli zilizopangwa kufanywa mwaka ujao wa fedha ikiwemo ziara ya wajumbe wengine.

Mhe. Spika, suala jengine lililoulizwa na Mhe. Salmin Awadh Salim kuhusiana na vifaa pamoja na zana kwa Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara. Suala hili tumelipokea na ushauri ni mzuri na wizara tayari tumeshaanza kulichukulia hatua, kwani tayari tumeshawasilisha Wizara ya Fedha barua ya mahitaji halisi ya zana pamoja na vifaa vya ujenzi. Pia wizara inatarajia kupata zana nzito na magari kupitia mradi wetu wa Ole/Kengeja kama vile tulivyoweza kutangaza katika hotuba yetu ya bajeti.

Suala jengine ambalo amelizungumza Mhe. Mjumbe ni kuhusu namna ya mfumo mzuri wa uendeshaji wa Karakana Kuu ya Serikali. Mhe. Spika, ni kweli kwamba Karakana hii kwa kipindi kirefu imekuwa haifanyi vizuri na sababu kubwa ni kuona kwamba mifumo au mitambo iliopo pale ni ya kizamani, yaani mitambo iliopo pale ni ya Kifaransa na hivi sasa soko letu kubwa la bidhaa za magari liko katika soko la bidhaa za Japan. Kwa hiyo, serikali pamoja na wizara tayari tunaandaa utaratibu mzuri wa kuweza kupata mbia kwa kushirikiana naye kwa mfumo wa *PPP*.

Jambo jengine ambalo lililalamikiwa ni kuhusu uuzaji wa tiketi kiholela, kwa maana ya kwamba tiketi za ulanguzi na hasa katika upande wa bandarini. Mhe. Spika, suala la uuzaji wa tiketi linasimamiwa na Kanuni za Usalama wa Vyombo Vidogo Vidogo vya Kienyeji kwa sheria ya mwaka 2008. Kanuni hiyo inapiga marufuku kuuza tiketi kwa bei ya juu, yaani zaidi ya ile bei iliyoainishwa kisheria, pia kanuni inakataza kuuza tiketi katika sehemu ambazo sio rasmi.

Kwa kweli tatizo la ulanguzi wa tiketi zinasababishwa na sababu zifuatazo. Kwanza uhaba wa vyombo vya abiria vinavyokwenda Pemba, wananchi hawatoi ushirikiano wa kutosha katika suala la kupambana na magendo ya tiketi. Hata hivyo, mamlaka inaendelea kuchukua hatua kadhia, ili kupambana na kulidhibiti tatizo hilo.

Miongoni mwa hatua hizo ni kusimamia zoezi la uuzaji wa tiketi kwa kutumia vitambulisho, ili kuimarisha uhakika wa tiketi na vitambulisho wakati abiria wanapoingia bandarini, kufanya *operation* maalum za kupambana na ulanguzi wa tiketi kwa kushirikiana na Vyombo vya Ulinzi na Usalama na Shirika la Bandari. Kwa mfano, tarehe 26 Machi, 2014 Mamlaka ya Usafiri Baharini kwa kushirikiana na Vyombo vya Ulinzi na Usalama vilifanya *operation* maalum ya kupambana na ulanguzi katika Bandari ya Malindi na tarehe 30 pia kurejea tena zoezi kama hili katika Bandari ya Malindi.

Mhe. Spika, hatua nyengine tunayochukua ni kufanya mikutano na Kamati za Ulinzi na Usalama, Wakuu wa Mikoa na Wilaya na kuwaomba watoe msaada katika kupambana na ulanguzi wa tiketi. Jambo jengine ni kuwaagiza wamiliki wa meli kuwachukulia hatua watendaji wao wanaojihusisha na ulanguzi wa tiketi. Kwa mfano, hivi sasa tayari Kampuni moja ya meli imeshamsimamisha kazi mfanyakazi wake mmoja baada ya kugundulika kwamba yeye anajihusisha na suala hili la ulanguzi wa tiketi.

Hatua nyengine ni kuwakamata watu wanaojihusisha na ulanguzi wa tiketi na kuwafikisha polisi. Aidha, Mamlaka inaendelea kuwapa leseni mawakala wote rasmi wa kuuza tiketi walioteuliwa na kampuni za meli kwa lengo la kuwatambua na kuwadhibiti ufanyaji wao wa kazi.

Mamlaka inaendelea kutoa elimu kwa wananchi wote kwa kutumia televisheni, redio pamoja na magazeti, ili waweze kufahamu na kuweza kutoa ushirikiano kama unavyotakiwa na serikali.

Mhe. Spika, kwa wale wengine waliozungumzia suala la bandari kuhusiana na eneo la ziada la kuegesha makontena. Kwa kweli tayari ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri umezingatia suala hili, ili kuweza kupata eneo zuri zaidi la kuweza kujenga mnara kwa ajili ya kuongozea vyombo.

Vile vile kufanya mabadiliko ya kimfumo Shirika la Meli na kuandaa utaratibu wa kuwastaafisha wafanyakazi waliofikia umri wa kustaafu. Shirika tayari limeshafanya zoezi hili na mapitio ya shirika la kupendekeza mfumo bora wa uendeshaji wa shirika hilo.

Mhe. Spika, wizara pamoja na shirika tumeomba Uongozi wa Chuo cha Chwaka kutusaidia kuupitia huu mfumo, ili kuweza kutushauri serikali mfumo gani mzuri zaidi katika malengo haya ya kukusudia kuweza kufanya *reform* kwa Shirika hili la Meli.

Pia Mhe. Makame Mshimba Mbarouk naye alizungumzia kuhusu mwendo wa kasi wa magari yanayobeba makontena na hatua zinazochukuliwa na wizara katika kukabiliana na jambo hili. Mhe. Spika, kikao cha Idara ya Usafiri na Leseni na Jeshi la Polisi tumekubaliana kuchukua hatua za kufaa katika kukabiliana na tatizo hilo.

Hata hivyo, kutokana na ukosefu wa vifaa ikiwemo vifaa vya kupimia mwendo kasi wa magari utekelezaji wa hatua hizo umekuwa mgumu na hata kupelekea kushindwa kuwatia hatiani washtakiwa wa makosa ya aina hii, kutokana na kukosekana na ushahidi wa kutosha unaotokana na kukosekana kwa kifaa hicho.

Aidha, jambo hili imetoka rai kwamba ni busara makontena haya tukayasafirisha wakati wa usiku. Kwa kweli rai hii ni nzuri isipokuwa ina changamoto yake, kwamba lazima tukutane na wenzetu wa *TRA*, kwa sababu utaratibu wa kuyatoa makontena lazima wenzetu watu wa Forodha wawepo. Kwa hivyo, tunalichukua tutakaa na wenzetu wa *TRA*, ili kuona kwa kiasi gani tunaweza kushirikiana kuweza kutoa huduma hii ya kusafirisha makontena kwa nyakati za usiku. *(Makofi)*

Mhe. Spika, suala jengine lililozungumzwa ni kuhusu ubovu wa barabara ya Mkokotoni/Gamba/Kinyasini mpaka Mahonda. Mhe. Spika, barabara hii ni miongoni mwa barabara katika ule mradi wa barabara saba zinazoingia mjini zenye urefu wa kilomita 78.

Hata hivyo, kutokana na umuhimu wa barabara yenyewe serikali kupitia Mfuko wa Barabara imekuwa ikizifanyia matengenezo barabara hizo, ili ziweze kupitia kabla ya mradi wenyewe uliokusudiwa kuanza. Katika mwaka uliopita kipande cha kutoka Gamba hadi Mshelishelini maeneo ya Chaani tayari kimefanyiwa matengenezo makubwa. Kwa hivyo, tutaendelea na matengenezo hayo hatua kwa hatua.

Suala jengine ambalo lililozungumzwa na Mhe. Ismail Jussa Ladhu ni kujua kiasi gani wizara inaweza kufanya matengenezo ya barabara kilomita 600. Mhe. Spika, hapa kidogo naomba nieleze hivi ni kwamba matengenezo yaliyokusudiwa hayakukusudiwa matengenezo ya barabarani moja kwa moja, isipokuwa matengenezo haya yanakusudiwa kuna baadhi ya maeneo tutaweka viraka, ukataji wa majani pembezoni mwa barabara, usafishaji wa michirizi na mitaro. Kwa maana hiyo, kwa ujumla maana ya usafishaji na matengenezo ya barabara ndio hizi kilomita 600 na wala haimaanishi kuwa ujenzi wa barabara zenyewe ndio hizo kilomita 600.

Mhe. Spika, jambo jengine ni kuifanyia matengenezo barabara ya Mwanakwerekwe/Tunguu na barabara hii ni miongoni mwa barabara katika mradi maalum. Lakini serikali pamoja na wizara kwa kutumia Mfuko wa Barabara imepanga kuifanyia matengenezo maalum barabara hiyo kuanzia Mwanakwerekwe Makaburini kwa urefu wa kilomita 1.7 hadi maeneo ya Meli Tano, ili kuona lile eneo ambalo limeathirika tunalipatia huduma ya awali kabla ya kuanza kwa mradi wetu mkubwa tunaoutarajia wa barabara zinazoingia mjini kuweza kuchukua hatua.

Mhe. Mjumbe, pia alitaka kujua kuhusu shilingi milioni 50 zitatumika vipi. Mhe. Spika, miongoni mwa fedha zitakazotumika katika uimarishaji wa barabara hii ya Mwanakwerekwe mpaka Meli Tano pembezoni kwa ajili ya kuongeza maeneo ya barabara husika, kwa sababu barabara yenyewe imekuwa nyembamba. Kwa hivyo, fedha hizo shilingi milioni 50 zitatumika kwa ajili ya kuongezea eneo la barabara hii tunayokusudia kuifanyia kuifanyia marekebisho ya awali, ili iweze kupitika vizuri kwa kuziba viraka na kuongeza eneo la pembezoni mwa barabara husika.

Vile vile suala jengine ambalo limezungumzwa ni kuhusu kutolipwa fidia kwa baadhi ya wananchi sehemu zilizopita barabara. Mhe. Spika, ni kweli kwamba kikawaida kabla ujenzi wa barabara kuanza wizara kwa kushirikiana na taasisi husika hufanya tathmini kwa ajili ya malipo ya fidia za mali za wananchi zilizoainishwa katika maeneo ya ujenzi wa barabara, hivyo kabla ya ujenzi kuanza wananchi wanaostahiki hulipwa fidia, ili kuruhusu kazi ya ujenzi iendelee.

Hata hivyo, kuhusu wananchi ambao hawakuwemo kwenye zoezi la awali la ulipwaji wa fidia kwa namna moja au nyengine nyumba zao zimeathirika baada ya ujenzi hutakiwa kuwasilisha malalamiko yao kupitia kwa sheha na maeneo yao. Kwa mfano, katika ujenzi wa barabara za Kaskazini Pemba zinazogharamiwa kwa ruzuku Serikali ya Marekani kupitia Mfumo wa Changamoto wa *Millennium*, wizara imefanya tathmini ya athari baada ya ujenzi wa barabara ya Mzambarautakau, Finya hadi Mapofu.

Pia serikali inaendelea kufanya tathmini kwa barabara zilizobaki ikiwemo barabara ya Chwale/Kojani na kuhusu barabara za Jendele, Cheju na Kaibona wizara imeanza kulipa fidia na nyumba ambapo eneo la kilomita nne za barabara limelipwa fidia.

Mhe. Spika, kiutaratibu ni kwamba malengo ya serikali hatutovunja nyumba ya mwananchi kabla ya kumlipa fidia, isipokuwa kuna tatizo la fidia ya vipando. Suala hili ni kweli kwenye miti na mimea tunang'oa kabla ya kumlipa fidia, ili kupisha ujenzi wa barabara. Lakini baada au wakati wa ujenzi tunapopata fedha tunaanza utaratibu wa kuwalipa fidia.

Vile vile kuna tatizo la pili; kuna watu wanaoathirika katika harakati za ujenzi kwa hiyo watu hawa huchelewa kulipwa. Kwa hiyo, sisi utaratibu wetu tutahakikisha kwamba barabara mtu yeyote aliyeathirika nyumba yake baada au wakati wa ujenzi, tunaona kwamba mtu huyo naye tunamzingatia na tutatafuta fedha, ili tuweze kumlipa kwa uzito ule ule kama tunaofanya kabla ya kumvunjia nyumba yake kwa ajili ya ujenzi wa barabara.

Mhe. Omar Ali Shehe naye alitaka kujua kwa kiasi gani serikali inachukua jitihada za kupunguza ajali. Mhe. Spika, serikali inaendelea kuchukua hatua za kudhibiti madereva wote wanaofanya vitendo vinavyohatarisha usalama barabarani kwa kuongeza doria za Jeshi la Polisi na Usalama wa Barabarani.

Mhe. Hamza Hassan Juma pia alitaka kujua kuhusu gari za Bububu ambazo zinakatisha *route* hazifiki kituo cha mwisho cha Hospitali ya Mnazimmoja. Mhe. Spika, suala hili tumelipokea na tunaendelea kuzungumza na wenzetu wa Polisi kwa kuona kwamba hatua stahiki zichukuliwe. jambo hili limekuwa ni tabia ya kujirejea, yaani linakuja na kuondoka.

Kwa hiyo, tutakaa na wenzetu wa Jeshi la Polisi kuona watu hawa wanaofanya vitendo hivi tuone kama upo uwezekano wa kuwafutia *route* zao, ili gari zao zifanye shughuli nyengine, kwa sababu yale malengo ya kuhudumia wananchi hawayatimizi na sisi hatutokuwa na jukumu tena la kusimamia jambo hili kuona wanalirejea. Mhe. Spika, hivyo ule ambae tutambaini anafanya jambo hili na anayo tabia hiyo tutahakikisha kwamba leseni yake tunaifuta na gari hiyo haitatumika tena kwa shughuli za kupakilia abiria.

Suala jengine ambalo lilizungumzwa ni kuhusu matatizo ya usafiri wa Pemba/Tanga. Mhe. Spika, sisi kama serikali tunalipokea na tutaona kwa kiasi gani tunaweza kuchukua hatua za kuweza kurekebisha jambo hilo kwa kuwashauri na kuwashawishi wafanyabiashara wenzetu waliopo, ili kuweza kuja kuekeza katika eneo hilo.

Mhe. Fatma Mbarouk Said naye alitaka kujua barabara yake ya Amani Fresh/Boriborini. Mhe. Spika, ombi la Mhe. Mjumbe wizara tunalifanyia kazi na tunajua kwamba kweli barabara hii imo ndani ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi na kwa namna moja au nyengine tunalazimika kuitekeleza.

Sisi kwa kushirikiana na wenzetu wa Manispaa kwa kutambua kwamba nguvu maalum ambazo zimeweza kujengwa mara hii kwa kupitia Mfuko wa Barabara, tutakaa na wenzetu wa Manispaa, ili tuweze kuona na wao kwamba wanaweka umuhimu maalum na sisi kama wizara tupo tayari kutoa mchango wa ufundi pamoja na vifaa na wenzetu wa Manispaa wakiweza kuchangia fedha, barabara hii nayo tutaona kwamba tunaweza kuijenga, ili kuondosha usumbufu wanaoupata wananchi wa maeneo husika.

Mhe. Spika, suala jengine lilikuwa la Mhe. Ali Salum Haji ambae aliomba uwekaji wa matuta. Kwa kweli suala hili tumelipokea na tutakaa na tuweze kuona hatua gani tunaweza kuchukua, ili kuweza kuweka matuta hayo kwa malengo yale ya kunusuru wananchi na watumiaji wa barabara husika, kwani kweli kama tunavyotambua kwamba barabara hii imepita katikati ya mtaa na kuna baadhi ya athari nyingi ambazo tunaweza kuzipata za watoto wadogo wadogo ambao wanakatisha barabara hiyo.

Aidha, Mhe. Mjumbe, pia alitaka kujua kwamba wizara inachukua jitihada gani katika kuimarisha barabara ya Kwabiziredi hadi Amani. Mhe. Spika, barabara ya Biziredi/Amani ni miongoni mwa barabara za Mradi wa *Town Entry Roads*. Kwa hivyo, jukumu letu sisi tunalichukua kuweza kuona kwamba kwa kiasi kikubwa tunafanya marekebisho madogo madogo, ili barabara hii isichimbike na iweze kuendelea vizuri.

Suala jengine ambalo lilizungumzwa na Mhe. Mgeni Hassan Juma ni kuhusu barabara ya Kikwajuni/Welesi. Mhe. Spika, ni kweli kwamba barabara hii tuli-*outsource* kwa kuipa Kampuni Binafsi kwa malengo yale yale ya kujenga uwezo makampuni binafsi yaliopo ndani, kwamba ajenge kwa kiwango cha kifusi na sisi serikali kwa kupitia Idara yetu ya UUB tutatumia mitambo yetu kwa ajili ya uwekaji wa lami baada ya kuona kwamba barabara hiyo imekamilika, na utaratibu huo tumekuwa tukiutumia maeneo mbali mbali; tumetumia barabara ya Mkokotoni, barabara ya Kiwengwa, barabara ya Tunguu kwa kuwapa makampuni binafsi mpaka mwisho baadae Serikali inaingia mkono wake kwa uwekaji lami.

Mhe. Spika, suala jengine limeulizwa na Mhe. Ismail Jussa Ladhu la kadhia ya *CCTV* pale *Airport* na suala zima la kukamatwa kwa madawa ya kulevya kwa kiasi gani kwamba Mamlaka au watendaji wa Uwanja wa Ndege wameweza kuhusika na kadhia hiyo. Mhe. Spika, ni kweli kwamba Mamlaka ya Uwanja wa Ndege imefunga mashine za *CCTV* na ni kweli wana mashine kumi na tisa (19); mashine hizi zinatumika eneo la ndani na eneo la nje la jengo la Uwanja wa Ndege. Hasa upande wa ndani na ni kweli kwamba siku ya Tarehe hiyo nyakati za asubuhi ilipofika ndege inayotoka Dar es Salaam kati ya hizi ndege zetu ndogo za abiria; kuna abiria ambae hakufuata taratibu za usalama na maelekezo ya utumiaji mzuri wa Uwanja wa Ndege, baada ya kushuka ndege abiria huyu kikawaida ukishuka ndege unatakiwa upite katika mlango wa *arrival lounge* lakini yeye hakwenda katika *arrival lounge* akaja katika *departure lounge* na alipokuja akaweka mikoba miwili rangi nyeusi.

Baadae akatoka mlango ule ule wa *arrival lounge* akaja akaingia tena kwa mlango wa *departure lounge* akaja ndani, Maafisa wetu wakamuona wakampisha akazungumza na maafisa wetu, akazungumza na maafisa wa *ZAT* akazungumza na maafisa wa *operator* wa ndege, baadae akatia mkono mfukoni akatoa kipochi, akatoa fedha akawakabidhi watu hao, akatoka baada ya kutoka kunako mapande kama ya saa nne ikaingia tax, gari nyeupe *saloon* wakashuka watu watatu, baada ya kushuka watu hawa wakaingia ndani ya uwanja wanasafiri ndege ya Saa sita ya Mango inayokwenda South Afrika.

Baada ya wale wasafiri kuingia ndani yule mtu wa kwanza akarudi akaingia uwanjani akazungumza na watu wa *Immigration,* akazungumza na watu wa afya baadae akatoka. Watu wale watatu wakenda wakapokewa na mfanyakazi wa *operator* wa ndege akenda kuwapokea wakazungumza, walikuwa wawili wamebeba *rascket* mgongoni mmoja hakuwa na *rascket* wakaingia uwanjani na tiketi zao kama wasafiri wa kawaida, wakaingia wawili wakakaa pamoja mmoja akakaa kando. Baada ya kuona yule *operator* akasimama kabla ya kuingia katika *checking* ya mwisho ya kuingia katika *departure lounge,* akawa ananong'ona na mmoja kati ya wale wasafiri, kunong'ona nae wawili wako ndani baadae mmoja aliyekuwepo ndani akatoka kana kwamba akaomba ruhusa amesahau kitu. Wakati anatoka akakutana na askari polisi akasimama akainama kama kwamba anafunga kamba kiatu, baada ya kupishana na polisi akatoka moja kwa moja hakurudi tena uwanjani.

Ndani kilichojiri wakati watu hawa wanasubirishia kuingia uwanjani mfanyakazi wetu mmoja ndege ya saa tatu na ndege ya saa nne zinaondoka mikoba ipo akenda akasema, watu wa *security* walikuwa wamekaa kwenye mashine kwamba ndege ya kwanza imeondoka, ndege ya pili imeondoka mikoba hii haijaondoka mwenyewe nani! Ikawa haina mwenyewe na kwa utaratibu wa usalama wa *airport* unapokuwa mkoba hauna mwenyewe la kwanza wanachotakiwa kufanya ni kuutizama kama mkoba ule hauna athari za mripuko, baada ya kwenda kufanya *checking* mkoba ule wakagundua kwamba huu mkoba una unga. Walichokifanya mamlaka ni kuukabidhi kwa jeshi la polisi na kwa bahati nzuri siku ile ile ukapelekwa kwa Mkemia, Mkemia akathibitisha kwamba haya ni madawa ya kulevya.

Kwa hivyo baada ya watu wale kuingia ndani na baada ya kwisha kuambiwa na yule *operator* na watu wao mle ndani kwamba ule mzigo umeshakamatwa na umeshakabidhiwa kwa Jeshi la Polisi, watu wale mmoja yule akawa ametoka wale wawili wakasafiri kwa ndege ya ndani wakati huo wana tiketi za ndege ya Mango wamesha-*board* na watu wa *Immigration* kwenda South Afrika, lakini kwa uzembe na malengo ya makusudi yaliyofanywa na *operator* wakawaruhusu watu hawa kupanda ndege ya ndani kutoka Zanzibar kwenda Dar es Salaam.

Kwa hiyo ni makosa ya mtu ambae ame-*check* ndege ya Kimataifa kumruhusu kupanda ndege ya ndani bila ya kutoka ndani ya uwanja kuja nje kukata tiketi, ni mle mle amekaa ndani ya *Departure* anasubiri kupanda ndege ya nje ameenda kupewa tiketi ya ndani, haya ni makosa, huu si utaratibu.

Mhe. Spika, baada ya hapo Mamlaka ilichokifanya ilikwenda kuwasiliana na wenzetu wa *Immigration* na kuwaambia katika orodha ya wasafiri waliokuwa wanakwenda South Afrika kuna watu wawili hawakupanda ndege ya Mango kwenda South Afrika. Ujumla wao watatu wakapewa majina mawili na watu wa *Immigration* mtu wa tatu akaambiwa mzungu kitu ambacho sio kweli. Watu waliokuwa wanataka kusafiri wote ni weusi, wote ni Watanzania, na ni wa hapa hapa. *Immigration* wakapotosha; wakasema kwamba watu waliokuwa hawakusafiri ni wawili wazalendo na mmoja mzungu kitu ambacho si kweli. Mamlaka wakawasiliana na wenzao wa Dar es Salaam wakatajiwa majina, wakatumiwa na picha, ukiangalia picha walizotumiwa na ukiangalia watu uliotumiwa unawatambua hawa ndio wahusika.

Kwa hivyo kilichofuatia Mamlaka wakakamilisha jukumu lao kwa kukabidhisha polisi na bahati nzuri siku ya pili yake Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum alikuwa ndio Kaimu Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili, kanipigia simu kuhusiana na kadhia hiyo tukenda mimi na yeye tukazungumza na Kamishna wa polisi bahati mbaya katika utambulisho wa *IGP* mpya akamuelekeza Kamanda wa Mkoa wa Mjini Magharibi, tukafuatana nae na Mkurugenzi msimamizi wa madawa ya kulevya *Inspector* Heri Yangu, tukenda tukaangalia *CCTV* ukiangalia *CCTV* inaelekeza yote ambayo nimeyasema.

Kwa hivyo mamlaka kwenye hili jukumu lake ni kuhakikisha kwamba mzigo umekamatwa, nani wahusika jeshi la polisi lichukue hatua za kisheria, kama kuna ucherewesha ji wa kwenda kushtaki kama kuna taratibu za kiusalama za kiuchunguzi, hilo ni jukumu la jeshi la polisi sio tena jukumu la mamlaka. Mamlaka walichokifanya nini? Mamlaka ina wafanyakazi wake ambao imewasimamisha kwa sababu kwa namna moja au nyengine ndani ya *CCTV* wameshiriki kama walivyo wafanyakazi wa *ZAT*, kama walivyofanya kazi wa *operator* ambao wameshiriki moja kwa moja katika hiyo *CCTV* unawaona.

Tunachokiomba wenzetu wa *Immigration* Wizara ya Afya nao wachukue hatua za kuwazuiya watu wao, ili kutoa ushirikiano kwa jeshi la polisi kuona kwamba hatua stahiki zinachukuliwa kwa watu hawa. Tunatambua kama hatukuchukua hatua madhubuti Uwanja wetu wa Ndege utakuwa mlango mkuu wa kusafirishia madawa na watu hawa aliyekuja nao mimi nina uhakika Jeshi la Polisi wanamjua, maana tumemuona kwenye *CCTV* tumemuona ushiriki wake tumeyaona matendo yake na tumeona watu aliokuja nao. Kwa hivyo kilichobaki wao kumchukua na kuhakikisha kwamba anafika mbele ya vyombo vya sheria, ili haki iweze kutendeka.

Mhe. Spika, jambo la pili liliulizwa na Mhe. Hamza Hassan Juma lilikuwa ni suala la mradi wa Chuo cha Marubani; mradi huu unataka kuanzishwa na kampuni ya *ZRP* ambayo ni *Zanzibar Reaction Project.* Kampuni hii ni kampuni ya kizalendo kwa namna moja au nyengine na hivi sasa inamiliki ndege tatu lakini wana mpango wa kumiliki ndege saba. Jambo hili hawakulianza leo wameanza muda mrefu na wao mimi mwenyewe binafsi nimepata nafasi ya kufanya nao mazungumzo wakakiri namna ya ushirikiano ambao wameupata kutoka Mamlaka ya Uwanja wa Ndege, ingawa kati kati mawasiliano hayakuwa mazuri sababu wanazijua wenyewe.

Mhe. Spika, nini kilichopo katika mradi huu wa *ZRP* mradi huu kwa namna moja au nyengine unapotoshwa haujasemwa ukweli haswa uliokusudiwa, mimi mwenyewe binafsi niliwahi kumsikia Mhe. Hamza mwaka jana anasema, lakini pia nimewahi kuziona *Correspondences* za barua ambazo wanazituma Serikalini katika maombi yao haya, bahati nzuri kwamba waliwahi kwenda kwa Makamu wa Pili wa Rais naye akatoa agizo kwa Wizara tuweze kuzungumza nao, tumezungumza nao wenzetu hawa tumewafahamu nini malengo yao.

ZRP wanataka kuazisha *Airstrip. Airstrip* hii inatofautiana na malengo wanayoyasema; maana wao wanachokisema kwamba wanataka waanzishe *Airstrip* kwa ajili ya kufunza marubani. Hili halina ukweli moja kwa moja, ukweli

wake upo asilimia 40 mpaka 50 wanataka kuamzisha *Airstrip* ili kufanya biashara na hili wamelikiri baada ya mazungumzo.

Kwa sababu wakati tunazungumza mimi niliwauliza mnasema mnataka kuanzisha *Airstrip* kwa ajili ya kuwafundisha marubani, ukiangalia ukubwa wa *runaway* ukiangalia majukumu na kazi zinazofanywa na Uwanja wa Ndege wa Zanzibar katika masaa 24 ya siku, muda ambao tunautumia uwanja wetu wa ndege hayazidi masaa manane, tuna masaa 16 mengine uwanja uko *free* kama lengo lenu kuwafundisha watu u-*pilot* mna masaa 16 ya kuutumia Uwanja wa Ndege. Wakwatwambia hatujakwaza na suala la pahali pa kurusha ndege kufanya shughuli hizo tunataka kufanya biashara. Mnataka kufanya biashara gani, wanachokitaka kuanzisha uwanja wa Ndege *Airstrip* katika eneo la Nungwi maeneo ya Kigunda, ili waweze kuchukua wageni wanaoshuka ndege uwanja wa ndege wa kimataifa wapande ndege ndogo washuke eneo wanalokwenda Nungwi watumie ndege badala ya kutumia magari.

Nikawajibu Serikali kwenye hilo hatuna pingamizi na hatuna pingamizi kwa sababu mwaka 2011 tulipokuja hapa tulipitisha sheria mbili kwa wakati mmoja; tulipitisha sheria ya mamlaka ya Uwanja wa Ndege tukapitisha na Zanzibar *Hydro Act* katika Zanzibar *Hydro* Act jukumu la Serikali la Waziri ni kuunda bodi au chombo cha kumshauri. Nilimshauri kwamba eneo hili kiusalama kwa mazingira ya Uwanja wa Ndege hakuna tatizo nayo.

Kwa hiyo wao walipokwenda kuomba ardhi wakasema kwamba wao wameambiwa hawatopewa ardhi mpaka wathibitishiwe kwamba hapa wanapotaka kujenga Mamlaka ya Uwanja wa Ndege Wizara ya Miundombinu haina pingamizi, na tukawajibu wajibu wetu sisi kwa mujibu wa sheria hata kama una nyumba ya ghorofa kwenye ghorofa yako ukitaka *land pad* sisi tunakuja kuanalia. Sasa kama wewe huna kiwanja unatutia sie lawamani vipi kanunue kiwanja chako lipa fidia tuje tuangalie sisi hatuna tatizo. Kwa utaratibu wa Viwanja vya Ndege popote duniani viwanja kukaa pacha sio tatizo *runaway* ya Dar es Salaam tunaiona ipo pacha na nyezake, *TCA* wametoa vibali karibu 190 kwa maeneo mbali mbali Tanzania watu wanamiliki *Iand pad* watu wanamiliki *Airstrip* hatuoni tatizo.

Kwa hivyo sisi tulichowaambiya kwamba wao waende Serikalini wakatafute ardhi malengo ya Zanzibar *Airport Authority* ni kuongeza eneo la biashara, wanataka kuwekeza kiwanja kama hicho Kigunda; hilo sio tatizo. Kwa sababu tunapokwenda kufanya biashara ndio malengo ya Serikali tutaongeza kodi, tutaongeza kazi, na hatutaikusudia Nungwi tu tuna malengo kama hayo kwa upande wa Paje, na tayari *ZAA* wameshapata kiwanja Paje wanakiendeleza.

Nungwi wanadaiwa milioni 16 na Wizara ya Ardhi watalipa wataweka kiwanja chao na tulipozungumza na *ZRP* wakasema wao wenyewe wako tayari kutoa ushirikiano ikiwa ubia, ikiwa ufundi, sasa nashangaa mazungumzo yetu mazuri tumeelewana nao wanalalamika; hawana haja ya kulalamika. Serikali imewafungulia milango kisheria hatuna pingamizi nao kama wanataka kufanya wenyewe wafanye, wakitaka kushirikiana na Serikali tuko tayari, hatuna pingamizi nao.

Mhe. Spika, naomba nichukue nafasi hii kuwasihi sana wawakilishi wenzangu kwamba sote tuna lengo moja la kutaka kusaidia na kujenga nchi yetu. Tunajua tuna mapungufu katika utendaji wetu huo ni ubinaadamu, tunajua kwamba Serikali hii ina malengo mazuri ya kutaka kuwasaidia wananchi wetu, kuna mapungufu makubwa ya upatikanaji wa fedha ambayo sio changamoto ya Tanzania tu, sio changamoto ya Bara la Afrika tu, lakini pia changamoto kwa nchi za dunia ya tatu zinazoendelea. Kwa hivyo niombe sana tushirikiane katika kukosoa kwa malengo na madhumuni ya kutaka kujenga nchi hii hatutoona tabu kuelekezwa, kukosolewa lakini msingi kwa malengo na madhumuni mamoja ya kutaka kujenga.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo nasema naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja kwa mia moja, ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kwanza naomba nichukue nafasi hii kumshukuru *Allah* katika siku ya Ijumaa ya leo kutujaalia uhai na uzima na pia kutuwezesha kuja katika baraza lako tukufu katika kuendeleza mbele maslahi ya nchi yetu. Pia naomba nikushukuru wewe binafsi kwa kuweza kuliongoza baraza lako tukufu kwa busara na uadilifu na pia kwa kuwapa fursa waheshimiwa Wawakilishi, kuchangia kwa kadiri ya uwezo aliowapa Mwenyezi Mungu kuhusiana na maendeleo ya Wizara yetu hii ya Miundombinu na Mawasiliano.

Mhe. Spika, ni dhahiri kwamba binaadamu hatukutimia kadri tulivyoumbwa tuna mapungufu na haiwezekani katika jambo lake lolote binaadamu hususan lile ambalo wanaongoza wengine, kwenda peke yake bila ya kupewa maelekezo, kwa hivyo mimi kwanza napenda nitoe shukurani zangu za dhati kwa wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi waliochangia binafsi na waliochangia kwa maandishi kwa kutupa maelekezo ya kina kuhusiana na uendeshaji wa Wizara.

Mhe. Spika, ni imani yangu kuwa sisi hata tungesimama wote tusingeweza kujibu kila suala ambalo tuliulizwa lakini *ishaalla* kwa uwezo aliotupa Mwenyezi Mungu tutajitahidi kujibu masuala mengi iwezekanavyo, lakini kwasababu tumeya-*document* masuala na tunayabakisha yatabaki kwamba ni *reference* yetu ya kufanya kazi kipindi kinachokuja.

Mhe. Spika, kabla sijaendelea mbele naomba nianze kwa kutoa utangulizi mdogo. Mhe. Spika, kulitokezea kisa pale Dar es Salaam yuko mtu kazi yake yeye ni kuchimba makaburi, kwa hivyo akapata taarifa kuwa mtu ameshafariki huko kachimbe kaburi akachimba kaburi lile ilikuwa ni asubuhi mazishi yapo saa saba. Kwa hivyo alilimaliza lile kaburi, kuuchimba ule mwanawandani akamuona nyoka, loo! Kazi haiendi tena akakimbia akenda akachimba jengine kufika kuuanza ule mwanaandani nyoka tayari, akaondoka akenda akachimba jengine, kuuanza mwanaandani nyoka akatokeza. Hapo hakustahmili tena alisimama akanyanyua mikono juu akasema *yaallah* ikiwa huyu nyoka ni kwa huyu ajaye si mimi, mimi nimekuja kutafuta kijio changu tu hapa. Bahati nzuri Mwenyezi Mungu akaitakabalia dua yake nyoka akaondoka akaendelea na kazi yake akapata kijio chake.

Sasa Mhe. Spika, mimi ni mchimba kaburi lakini hayo majoka yalikuwa huko nyuma nisitwike nayo mimi. Sisi tumelikuta jengo la *terminal II* haliendi, sasa linakwenda. Sasa bado tunalizungumza lile *terminal II* tutalijibu sisi lakini sasa linakwenda, kazi inaendelea *terminal II* inajengwa. Nilipoingia hakuna mazungumzo ya mpiga duri sasa mpiga duri mkataba karibu uko njiani kusainiwa. Tulipoingia pale masuala ya barabara zote zinaendelea sasa nyengine zimekamilika, kwa hivyo nasema kwamba bora umuhukumu mtu kwa lile alilofanya yeye na sio yale waliofanya wengine yeye akaja akayarekebisha. Baada ya utangulizi huo Mhe. Spika, naomba sasa niwashukuru wajumbe waliochangia 29 binafsi na waliochangia kwa maandishi ni 10 kama hivi ifuatavyo:-

1.	Mhe. Panya Ali Abdalla	Makamu Mwenyekiti wa Kamati
2.	Mhe. Mohammedraza Hassanali	
3.	Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	
4.	Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	
5.	Mhe. Mohammed Haji Khalid	
6.	Mhe. Saleh Nassor Juma	
7.	Mhe. Ismail Jussa Ladhu	
8.	Mhe. Marina Joel Thomas	
9.	Mhe. Rufai Said Rufai	
10.	Mhe. Farida Amour Mohammed	
11.	Mhe. Hassan Hamad Omar	
12.	Mhe. Nassor Salim Ali	
13.	Mhe. Hija Hassan Hija	
14.	Mhe. Ashura Shariff Ali	
15.	Mhe. Mgeni Hassan Juma	
16.	Mhe. Omar Ali Shehe	
17.	Mhe. Suleiman Hemed Khamis	
18.	Mhe. Ali Salum Haji	
19.	Mhe. Fatma Mbarouk Said	
20.	Mhe. Salmin Awadh Salmin	
21.	Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	
22.	Mhe. Asha Bakari Makame	
23.	Mhe. Kazija Khamis Kona	
24.	Mhe. Abdalla Mohammed Ali	
25.	Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa	
26.	Mhe. Hamza Hassan Juma	
27.	Mhe. Salim Abdalla Hamad	
28.	Mhe. Machano Othman Said	Waziri asiye na Wizara Maalum; na

29. Mhe. Omar Yussuf Mzee Waziri wa Fedha

Waliochangia kwa maandishi ni:-

1. Mhe. Asha Abdu Haji
2. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
3. Mhe. Salma Mussa Bilal
4. Mhe. Salma Mohammed Ali
5. Mhe. Bikame Yussuf Hamad
6. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo
7. Mhe. Thuwaibah Edington Kissasi
8. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
9. Mhe. Ussi Jecha Simai na
10. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa

Ninawashukuru sana wote na kama nilivyotaja mwanzo pale naahidi kwamba mimi pamoja na watendaji wote tukifuatiwa na Naibu Waziri tumeyachukua kama yalivyo na yale ambayo hatutowahi kuyajibu lakini kwa sababu ya wakati na mambo mengine tutakuwa tunayo katika document zetu na tutayatekeleza kama ambavyo Baraza lako tukufu limeelekeza.

Kwanza naomba nianze na suala la Mhe. Ismail Jussa Ladhu kuhusiana na maelezo ya kina na matumizi ya fedha za serikali za mfadhili zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa jengo jipya la abiria. Mhe. Spika, mkataba wa awali ulijumuisha ujenzi wa jengo lenye ukubwa wa mita za mraba 15,600 maegesho ya ndege yenye ukubwa wa mita za mraba 23,000 na maegesho ya magari yenye ukubwa wa mita za mraba 4570, mikonga mitatu ya kupandia na kushukia ndege ya *quad* C.

Jengo la mitambo pamoja na uwekaji wa vifaa vyote muhimu katika jengo jipya. Gharama za awali zilikuwa ni dola za kimarekani 70.4 milioni. Ongezeko la kwanza lilihusiana na mabadiliko ya *design* ya jengo na kupelekea jengo kuongezeka kwa mita za mraba 2209 zaidi na kufikia mita za mraba 17,809. Hali hii ilipelekea ongezeko la nguzo za vyuma, marekebisho ya *certtern wall,* kuongeza nguvu za mashine na vifaa vya umeme, ujenzi wa eneo la mbele, ujenzi wa ngazi na kadhalika. Marekebisho haya yalipelekea gharama kuongezeka na kufikia milioni 82.228.

Ongezeko la pili ambalo lilifanyika hivi karibuni *gate number 2* lilitokana na uamuzi wa serikali kutekeleza mapendekezo ya mshauri muelekezi wa ADPI, hii ilibadilisha ukubwa wa jengo kufikia mita za mraba 23,000 kutoka mita za mraba 17,809. Eneo la kuegesha ndege litaongezeka ukubwa kutoka mita za mraba 23,000 na kufikia 37,800. Eneo la kuegeshea magari litafikia ukubwa wa mita za mraba 7556 kutoka mita za mraba 4570. Kwa ujumla jengo la abiria limeongezeka kwa asilimia 30, eneo la kuegeshea limeongezeka kwa asilimia 64 na maegesho ya magari limeongezeka kwa asilimia 65. Gharama za jumla za ujenzi ni dola za Kimarekani milioni 128.5.

Mhe. Spika, uwanja wa ndege wa Pemba naomba wanisikilize vizuri hapa wajumbe kwa sababu liliulizwa na wajumbe wengi akiwemo Mhe. Mohammed Haji Khalid, Mohammed Mbwana Hamad, Mhe. Saleh Nassor Juma, Mhe. Ismail Jussa, Mhe. Farida, Mhe. Hassan Hamad Omar, Mhe. Ashura, Mhe. Asha Bakari na wengi walioliuliza suala hili.

Mhe. Spika, suala la uwanja wa ndege wa Pemba kwanza lilianza na kuwa tunatia taa, lakini baada ya juhudi za upatikanaji wa fedha kutekeleza mradi huu kushindikana kutoka mfuko wa serikali, serikali imeamua kutekeleza mradi huu kwa kutumia mkopo kutoka Benki ya Exim ya Uturuki ambayo kimsingi imekubali kuipatia mikopo serikali kwa ajili ya ujenzi wa kiwanja hicho ambao utahusisha pamoja na maelezo yaliyomo katika hotuba yangu.

Serikali kupitia Wizara ya Fedha imekubaliana na Kampuni ya *Resense* ya Uturuki kutekeleza mradi huu. Kwa hivyo maelezo yale ya awali tayari yamo ndani ya kitabu ya uwanja utakavyokuwa. Sasa haya matokeo ya karibuni Wizara imepokea ripoti ya awali ya upembuzi yakinifu na kuendelea kufanyiwa mapitio ya kina.

Aidha, katika hatua za kujiridhisha zaidi serikali itatafuta mtaalam wa kufanya mapitio na kutoa ushauri wa kufaa kabla ya kuruhusu hatua nyengine ziendelee. Kulingana na ripoti hiyo muda wa ujenzi unakadiriwa kuwa ni miaka 2 baada ya kuanza kazi. Mhe. Spika, kwa ruhusa yako hapa ninavyo vitabu viwili; hiki kimoja kinaeleza ramani na

maelezo kamilifu ya ujenzi wa uwanja. Hiki cha pili ni *feasibility study* ya ujenzi wa uwanja kutokana na hiyo Kampuni ya *Resense*. Sasa hizi ni *draft report*, kwa hivyo hivi sasa Wizara imeshaitawanya kwa wataalam mbali mbali ili kuipitia na kuijadili, watakapokuja wataalam wa Kampuni watakaa nao pamoja na kutoa masahihisho yao.

Kwa hivyo utaratibu wa kuupatia suluhu ya kudumu uwanja wa ndege Pemba na sio taa peke yake tayari umo katika machakato ambao umeshakubaliwa na serikali. Kwa hivyo sisi Wizara kazi yetu kufuatilia kwa kina na kuona. Kama nilivyosema Exim Bank ya Uturuki tayari imeshatoa barua ya kutoa fedha kukubaliana na mradi huu. Kwa hivyo kinachotakiwa ni kupitia hii *feasibility study*. Sisi hapa na wataalam wetu na tukawaita wale wanaotaka kujenga tukaja kukaa nao kitako ili kuweza kufikia lengo la makubaliano na kutia sahihi mkataba.

Kwa hivyo hili halina tena kuyumbisha, si kwa kutia taa lakini kujengwa kama nilivyosema ujenzi wenyewe ni kuongeza mita 800 kutoka 1500 mpaka 2300, kuongeza upana, kuweka taa, kujenga jengo jipya jengine la *Terminal*, kulitengeneza lile liliopo pamoja na maeneo ya kuwekea gari za zimamoto pamoja na *fence*.

Mhe. Spika, ninaendelea mchango uliotolewa na Mhe. Mohammed Haji Khalid, Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe. Marina Thomas, Mhe. Rufai Said Rufai, Mhe. Farida kuhusu sababu za kutokumalizika kwa ujenzi wa barabara ya Wete/Gando na Wete/Konde. Ujenzi wa barabara ni mgumu sana kwa sababu tatu kubwa;

Kwanza, barabara nyingi tunajenga kwa njia ya mkopo kwa kutumia wafadhili, kwa hivyo ule muda wa mazungumzo baina ya serikali na wafadhili ni sehemu moja ya kuwa barabara zinachukua muda hata kama mshatiliana mkataba, kuna marejesho na kuna kukubaliwa yale marejesho halafu zikaingizwa tena fedha.

La pili sisi katika nchi yetu ni ndogo kwa hivyo maeneo mengi ambayo yanataka kujengwa barabara yanapambana na ujenzi wa nyumba, huwa kuna nyumba nyingi na katika *component* moja ya wafadhili hawataki kuingiza fedha za fidia katika ule mkopo. Isipokuwa hilo lilifanywa na MCC tu kwa njia za msaada lakini wote hii inayopatiwa mikopo fedha za fidia zinatoka serikalini. Sasa na hapa tunajua ufinyu wetu bajeti, kwa hivyo mara nyingi mkandarasi huwa hapati ile *sight* yake kikamilifu wakati anataka kujenga, hubidi kungojea ili serikali ilipe fidia. Na huo ushahidi kwa njia ya Wete/Gando ni kuwa 2013 ndipo walipolipwa watu wa Bopwe kutoka Wete kuelekea Gando watu wa Bopwe ndio walivyolipwa pesa zao katika kipindi chote hicho.

Halafu sasa, kuna madeni ambayo anadai mkandarasi, lakini kama tulivyokwisha sema kwamba kwa njia ya Wete/Gando na Wete/Konde serikali haina tena jukumu sasa hivi mpaka atakapofanya kazi akadai pesa zake, pesa zake zote amelipwa na kazi inaendelea vizuri.

Jana tumeangalia na *engineer* wetu ambae yupo kwenye *sight* huyu anaitwa Japhet ambaye alikuwa ni *sight engineer* katika barabara za MCC, *response* yake ni kwamba kazi inakwenda kwa kasi nzuri katika ujenzi wa barabara hizi mbili. Kwa hivyo ni matumaini yetu kwamba kwa tarehe zilizowekwa, barabara hizi zitakamilika bila ya vikwazo vyengine vyovyote.

Mhe. Spika, sasa ninakuja kwenye suala la usimamizi wa karibu wa ujenzi wa meli ya serikali na kutoingizwa maelezo ya meli katika kitabu. Mhe. Spika, ujenzi wa meli ya serikali unaendelea vizuri na tumeingiza katika kitabu isipokuwa baadhi ya wahaheshimiwa hawakukiona pale kilimo. Huu ni mradi wa serikali kwa hivyo uko katika kifungu mwanzo huku katika sehemu ya mipango sera na sio kwenye Shirika la Meli, ukenda kwenye Shirika la Meli utakuwa huuoni huo mradi, kwa sababu ni mradi wa serkali. Program ya meli inaendelea vizuri, kazi za usimamizi wa ujenzi zinafanywa na Kampuni mahiri ya usimamizi wa ujenzi wa meli *Lloyd's class* kwa mujibu wa utaratibu wa ujenzi wa meli.

Mhe. Spika, hili niliwahi kulieleza hapa katika kipindi cha nyuma kwamba utaratibu wa ujenzi wa meli tofauti na ujenzi wa nyumba. Nyumba mpaka yule muelekezi umtafute lakini hawa wanaoshughulikia na usalama wa meli ukenda tu ukitaka kufanya *contract* ya ujenzi wa meli tayari wapo waelekezi wameshawekwa lazima uzungumze nao, mkubaliane, ndio meli ijengwe.

Kwa hivyo hawa wako duniani wanangoja kazi na huwezi kupata ruhusa ya kujenga meli kabla hujazumngumza na hawa. Inategemea ni nani tu unayemtaka wewe. Kwa hivyo sisi sana hapa tumezoea kuchuku hawa *Lloyd's class* ambao makao makuu yao yapo Uingereza. Na hao ndio tumekubaliana nao na ndio wanaosimamia ujenzi wa meli.

Kwa hivyo Mhe. Spika, kulingana na ratiba ya ujenzi wa meli iliotolewa na kuridhiwa na msimamizi wa ujenzi wa meli hiyo *Lloyd's class*. Ujenzi wa meli hiyo unatarajiwa kukamilika mwezi wa April 2015 kama ilivyopangwa.

Aidha, ili meli hiyo iweze kupita hapa nchini mapema na ikiwa katika hali ya usalama inatarajiwa kuchukua muda wa mwezi mmoja kutoka Korea ya Kusini kupitia njia itakayokubaliwa na serikali. Hivyo ikiwa ujenzi wa meli hiyo utakamilika kwa wakati uliopangwa inatarajiwa kuwa meli hiyo itafika ndani ya mwezi wa Juni 2013.

Mhe. Spika, sasa naomba niingie katika suala la Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Hija Hassan Hija, Mhe. Ashura Shariff Ali, Mhe. Salmin Awadh na Mhe. Hamza Hassan Juma. Ongezeko la idadi ya abiria katika meli ya *Sea link* Mhe. Spika, ilinunuliwa na Kampuni ya Azam Marine nchini Ugiriki mwaka 2012. Mkaguzi wa Mamlaka ya Usafiri…

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe Wizara hii ya Miundombinu inahitaji nondo nyingi sana, sasa nondo nyengine ilikuwa bado hazijafikishwa pale bandarini kwa ajili ya ujenzi huo, naona sasa ziko tayari.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, naomba nianze Meli hii ya *Azam Sea Link* ilinunuliwa na Kampuni ya *Azam Marine* nchini Ugiriki mwaka 2012. Mkaguzi wa Mamlaka ya Usafiri Baharini alikwenda nchini Ugiriki kuikagua kabla haijaja Zanzibar, na baada ya ukaguzi huo ilipewa usajili wa muda (*provisional registration*). Meli hiyo kutokana na umadhubuti na uimara wake ilisafiri wenyewe kutoka nchini Ugiriki hadi Zanzibar ikivuka bahari kadhaa zenye dhuruba na mawimbi makali. Kwa mujibu wa *stability booklet* hasa Mheshimiwa hapa ndiyo nilipoagiza ule mkoba nimesahau kidogo. Hiki Mhe. Spika, ndiyo kitabu kinachoitwa *stability booklet* na ndiyo kinaeleza wazi wazi idadi ya abiria ambao wanatakiwa wapakiwe katika meli ile.

Kwa hivyo, humu kuna mambo mawili, hiki kitabu ilikuwa mimi nimeshaletewa barua na Baraza la Wawakilishi kwa ile kauli niliyoitoa kwenye suala la nyongeza la Mhe. Hija Hassan Hija niilete. Na nilikuwa nimeshaandika barua ya kukileta hiki kitabu pamoja na maandishi yake kulijibu lile suala la nyongeza kama nilivyotakiwa. Kwa hivyo, kwa hudhuri hii leo naomba nipige ndege wawili kwa pamoja, kwa sababu na barua ya Katibu imo naomba nihudhurishe hiki kitabu kinachoeleza *stability* ya meli kutoka kwao na kipitiwe na wale wajumbe wote waliochangia na wanaotaka kujua, na kwa kuelekeza zaidi kwenye ukurasa wa 18 ndipo kilipoandikwa hao idadi ya abiria ambao wanaruhusiwa kupakiwa katika meli, na kitabu hiki ndiyo kinachotumika dunia nzima kuifanya kama meli ina nini na nini. Kama huna hiki hakuna chochote, kwa hiyo kina maelezo yake kamili na kila kitu kamili.

Mhe. Spika, kwa sababu hili suala lilimuhusu mfanyabiashara ambae ni mahiri, ni mkweli, anayesaidia Zanzibar bahati mbaya sana Mhe. Spika, kutokana na namna ambavyo lilizungumzwa sisi tumepokea taarifa rasmi kwa mwekezaji huyu kwamba amekatisha safari zake za kwenda Pemba, kwa sababu hili suala limezungumzwa vibaya bila ya ushahidi. Kwa hivyo, mimi nakuachia wewe Mhe. Spika uamue watu wanaozungumza masuala magumu, makali tena bila ya ushahidi, na pale niliposema mimi katika jibu la nyongeza kwamba ushahidi upo na nitauleta, na nikapokea barua ya Baraza la Wawakilishi. Kabla sijaleta ushahidi likaja likazungumzwa tena na mtu huyo huyo ambae nilimpa uhakika bila ya kupitia ngazi za Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, sheria tuliyoibadilisha hapa kama ilivyozungumzwa; ilizungumzwa kuhusu kuongeza na siyo kubadilisha seti ya ndani. Kuongeza na kubadilisha *setting* ya ndani ni vitu viwili tofauti. Mhe. Spika, ukumbi huu huu tunakaa watu 80, ukumbi huu huu ukitaka ukae watu 200 watakaa. Bungeni juzi tumekwenda muhimu ni ile *turn age* ya meli ndiyo ile ile au siyo na siyo viti vinawekwa vipi. Mhe. Spika, meli haikuongezwa kilichobadilishwa katika meli ni *setting arrangement* ya ndani ya meli iliyokuwepo wakati ule na iliyokuwa hivi sasa. Kwa ushahidi kamili na hii hapa *booklet* yake. Sasa haya maneno yaliyotolewa hapa bila ya ushahidi mimi napenda niseme kwamba waiombe radhi wizara, wamuombe radhi mfanyabiashara huyu maarufu bila ya hivyo Baraza litachukua hatua inayofaa wenyewe.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa *stability booklet* kitabu cha uzani wa meli kilichotayarishwa na *Delta Technical Bureau* Kampuni ya Kimataifa inayosimamia uchoraji wa ramani za meli, usimamizi wa ujenzi wa meli, ukaguzi wa meli, upimaji wa wizani wa meli (*in cleaning test*) ya nchini Ugiriki inaonesha meli hiyo inayo uwezo wa kubeba abiria 1500 na tani 315 za mizigo. Kwa sababu ni mara ya kwanza meli ya aina hii *roll on and roll of* kufanya kazi katika maeneo ya visiwa vya Unguja na Pemba mamlaka iliamua kutoa kibali cha abiria kwa kiwango tofauti kwa kila awamu kwa lengo la kupima na kujiridhisha uwezo wake wa kufanya kazi katika maeneo ya bahari ya Zanzibar. Kwa hivyo, mamlaka ilitumia uwezo wake wa kisheria wa kuviangalia vyombo.

Mhe. Spika, sasa tunakuja katika mchango wa Mhe. Makame Mshimba Mbarouk na wawakilishi wengine waliochangia kuhusu mwendo wa kasi wa magari yanayobeba makontena, hatua zinazochukuliwa na wizara katika kukubaliana jambo hilo.

Kikao cha Idara ya Usafiri na Leseni na Jeshi la Polisi kimekubaliana kuchukua hatua za kufaa kukabiliana na tatizo hili. Hata hivyo, kutokana na ukosefu wa vifaa ikiwemo vifaa vya kupima mwendo kasi wa magari utekelezaji wa hatua hizo umekuwa mgumu na hata kupelekea kushindwa kuwatia hatiani washtakiwa wa makosa ya aina hii. Kutokana na kukosekana kwa ushahidi wa kutosha unaotokana na kukosekana kwa kifaa hicho.

Mhe. Spika, matengenezo ya barabara iliyotajwa na Mhe. Makame Mshimba ni kwamba ushauri wa Mhe. Mwakilishi tumeupokea na tutaufanyia kazi.

Kuna suala hili kubwa vile vile lilozungumzwa kuhusiana na barabara ya Ole/Kengeja, hili limechangiwa na Mhe. Mohammed Mbwana Hamad, Mhe. Mohammed Haji Khalid, Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe. Rufai Said Rufai, Mhe. Saleh Nassor Juma, Mhe. Farida Amour Mohammed, Mhe. Hija Hassan Hija na Mhe. Nassor Salim Ali.

Mhe. Spika, suala hili wizara ikishaingia makubaliano na Jumuiya ya Kimataifa ya Ufadhili haiwezi kudharau ikawa isilitaje tena, kwa sababu haya mambo yanasikikana kila pahali, yanasomwa kila pahali. Sasa tukisema huu ni mradi wa muda mrefu haujafanywa kitu itakuwa haitutendei haki. Ziko *stage* tunajua kwa mfano kama watu wanawajua watu wa *World Bank* miradi yao mpaka ukiipata si chini ya miaka mitano. Kwa hivyo, kila mfadhili na ule utaratibu wake wa muda wake wa kufanya kazi, inawezekana muda wa miaka mitano unatajwa mradi ule lakini uko katika *different stages*. Kwa hivyo, mradi wa Ole/Kengeja ni mradi endelevu.

Mimi kwanza nimjibu Mhe. Mohammed Mbwana Hamad yeye alisema kwamba vitabu vitatu vyote vinazungumza lugha moja, siyo kweli *paragraph* ya mwanzo zote ni sawa, lakini *paragraph* ya pili na ya tatu zinatofauti kila mwaka, kila mwaka zina tofauti kwa hatua iliyofikiwa. Kwa hivyo, nasikitika wamesoma maneno ya mwanzo halafu umeyabakisha mengine umeyaachia. Kwa hivyo, kila mwaka baada ya kusoma kwa sababu ile sentensi ya mwanzo inakusudiwa kuujuulisha ule mradi usiwe mgeni na wewe, halafu wa pili na ya tatu ndiyo inakusudiwa kuweka ile *status* ya ule mradi ulipo. Kwa hivyo, *paragraph* ya pili na ya tatu ukisoma vitabu vyote vitatu ni tofauti. Mwanzo ilikuwa haijakubaliwa, ikakubaliwa halafu ikawa hivi, hivyo maneno ni tofauti hayako hivyo hivyo kama ulivyosema yote ni sawa.

Mhe. Spika, ni kweli katika bajeti ya mwaka 2013 serikali ilikuwa na lengo la kutekeleza mradi huo kwa kutumia *labour base.* Kwa vile fedha zilizotengwa zingetosha kukamilisha ujenzi wa barabara yote kwa kutumia mkandarasi. Katika bajeti ya mwaka 2013/2014 *OFID* ilikubaliana na wazo la serikali ya kuijengwa barabara hii kwa kutumia mfumo wa nguvu kazi watu. Katika bajeti ya mwaka 2014/2015 serikali inakusudia kujenga barabara hii kwa mchanganyiko wa nguvu kazi na *machine* katika hatua ya utiaji wa lami. Kwa sasa msimamizi wa mradi tayari ameshaanza kazi ya upimaji wa eneo litakalopita barabara zimeanza na jumla ya kilomita 11 zishapimwa kutoka Ole hadi Mfikiwa. Na haya ndiyo ambayo niliyosema mwanzo kwamba sentensi zinatofautiana, sisi Mhe. Spika, katika kitabu chetu cha bajeti tuliripoti kilomita 7 zishapimwa, leo najumuisha kilomita 11 zishapimwa katika kipindi hiki cha kuandika ile bajeti na hiki.

Kwa hivyo, hii kazi inaendelea siyo kweli kwamba imesita, lakini nataka niwatoe wasi wasi kwamba wale waliofikiria kwamba barabara hii haitokuwa madhubuti itajengwa kwa mchanganyiko kama ambavyo bajeti yetu ilionesha kwamba kuna ununuzi wa zana tena zana nzito. Kwa hivyo, ilivyokuwa kuna ununuzi wa zana nzito basi ni dhahiri kwamba umadhubuti wake utakuwa mkubwa zaidi.

Mhe. Spika, waheshimiwa hawa hawa walichangia kuhusu kuwepo kwa mashimo katika barabara sita za Kusini Pemba. Mhe. Spika, moja katika kazi ya mfuko wa barabara ni kuzitengeneza barabara zile ambazo zishatiwa lami lakini zikazipitia. Na hapa naomba nichanganye na lile suala lililoandikwa wizara itapitia matengenezo ya barabara ya kilomita 640, hii ni pamoja na hizo. Kwa hivyo, zote hizi zimo katika utaratibu wa kupitiwa na kufanyiwa matengenezo, kujazwa kufanya hivi ndiyo barabara hizi zilizokusudiwa.

Mhe. Spika, vile vile waliuliza kuhusu kufumua barabara ya Mkoani ni dhahiri tukiifumua barabara ya Mkoani ushaifunga Pemba, lakini tukimaliza barabara ya Ole/Kengeja ni rahisi sasa kuifumua barabara ya Mkoani kwa

stage, kwa sababu gari sasa zitakuwa na njia ya kupitia na kutokea mpaka Wete na Konde. Lakini ukiifumua sasa hivi ni dhahiri kwamba umeufunga utaratibu wote wa usafiri Pemba. Kwa hivyo, kwa sasa hakuna nia hiyo kutokana na hali hiyo halisi iliyopo.

Mhe. Mohammed Mbwana, Mhe. Mohammed Haji Khalid na Mhe. Hija Hassan Hija walizungumza kuhusu barabara ya Mgagadu/Kiwani. Sababu imeshatajwa na Mhe. Waziri wa Fedha ametueleza hapa asubuhi na kueleza kwamba sisi wakati zikiingizwa fedha ilifanywa sasa hakuna fedha na tumesema sisi kwamba ile daraja inajengwa baada ya ku-*straggle* na kuona kwamba fedha za mfuko wa barabara zitumike ijengwa daraja. Na daraja ni kitu ghali kwa sababu unaweza ukajenga barabara moja kwa kilomita chungunzima za barabara. Kwa hivyo, lazima hapo ujue kwamba fedha ndiyo hakuna, sisi hatukatai kujenga barabara lakini fedha hakuna hatujaingiziwa.

Mhe. Spika, hapa nataka tuelewane kidogo Waheshimiwa Wajumbe, hii wizara yetu inayo Idara inaitwa UUB lakini nyie Waheshimiwa Wajumbe hamjawahi kuona kifungu chake mkakisemea, kwa sababu fedha zinazoingizwa UUB ni fedha za matumizi ya kawaida si za ujenzi wa barabara. UUB inategemea *hundred percent* fedha za Mfuko wa Barabara ndiyo zijengee barabara, haitiliwi kifungu cha ujenzi wa barabara UUB ni fedha za matumizi ya kawaida ambazo hata hiyo ya kawaida tulidai kwa Wizara ya Fedha sisi yaondolewe yale maandishi kwa sababu ununuzi wa *spare*, moja ya zana nzito ni gari mpya kwa sehemu nyengine. Kwa hivyo, hiyo idara wenyewe ku-*equip* ukaiweza ni hali ngumu sana.

Kwa hivyo, ukisema kwamba njia mara hii haikupitiwa ni kwa sababu ya ukosefu wa fedha, lakini kama fedha zimekuwa *mentioned* katika bajeti halafu sisi hatukuipitia pale inakuwa kweli tuna kosa. Lakini bila ya kuingiziwa fedha tutakwenda fanya nini sisi, hatuna la kufanya na ndiyo mana tunaripoti kuwa hatukuingiziwa fedha na Waziri wa Fedha anakiri mwenyewe kwamba hali ni ngumu.

Mhe. Saleh Nassor Juma aliuliza kuhusu ubovu wa daraja la Vitongoji, wizara inasema kwamba daraja hili tayari limefanyiwa uchunguzi na kubainika kuwa ni kweli linahitaji kufanyiwa matengenezo makubwa. Wizara inakusudia kulifanyia matengenezo daraja hili katika mwaka wa fedha ujao.

Vile vile Mhe. Saleh Nassor Juma aliuliza kuhusiana na malipo ya fidia wakati njia ya umeme inapitishwa kutoka *Fidel Castro* kwenda Vitongoji. Mhe. Spika, ni kweli malipo ya fidia ya wananchi hawa bado hayajakamilika hata hivyo wizara imeanza kulipa fidia wananchi 12 kati ya 75. Na hawa aliowataja Mhe. Mwakilishi akiwemo ndugu Mohammed Najim Omar na ndugu Najim Omar Abdalla ambao wote kwa pamoja wanadai ni kati ya hao hakuna anayedai muembe. Kwa hivyo, mwakilishi alivyosema mlikuwa na miembe haikuwa jambo la kweli, iliyokuwemo ni mihogo na mibuyu.

Suala la Mhe. Ismail Jussa Ladhu la uwezo wa wizara kutengeneza kilomita 600 nilishalijibu kwamba iliokusudiwa ni matengenezo madogo madogo ya kuziba viraka na mengineyo, lakini siyo kwamba matengenezo makubwa kilomita 600. Ni matengenezo madogo madogo ambayo nayo yanakera kwa sababu njia itakuwa safi utakuwa ushatulia kwenye gari yako utaingia kwenye kishimo kidogo itatikisika. Kwa hiyo, hayo ndio matengenezo yaliyokusudiwa.

Sasa kuna Wajumbe akiwemo Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mhe. Mohammed Haji Khalid, Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, kuhusiana na suala la kwanza la *Zantel. Zantel* sisi kama wizara hatuna uhusiano wa kimaendesho, tuna uhusiano wa kiufundi tu *technical corporation*, nayo masuala ya kimaendesho ni Wizara ya Fedha wenyewe ndio wanaoshughulikia na *shareholder* kwa sababu wao ndio wenye mwakilishi anayeingia katika *shareholder's committee*. Kwa hivyo, majibu yake ya kiasi gani, maendesho yake siku gani, ni Wizara ya Fedha.

Vile vile mashirika mengine ya Muungano, tunao uwanja wa ndege pale *TCA* na *TMA* tuna uhusiano wa kiufundi, taratibu zao za kufanya kazi ni tafauti na taratibu zetu.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe naomba tumsikilize Mhe. Waziri anafanya majumuisho ili tuweze kuja kuendelea na kazi hii mara baada ya kumaliza majumuisho hayo. Tumsikilize kwa makini ili tuelewe kile anachokizungumza. Mhe. Waziri tuendelee.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Sisi upande wetu wa wizara tunayo *TCRA* nayo vile vile tuna uhusiano wa kiufundi tu na sio mengineyo, masuala ya kimaendesho na mapato yao yanashughulikiwa na Wizara ya Fedha pengine kupitia *ZRB* na mwenginemo.

Suala la wafanyakazi waliotimuliwa hii ni Wizara ya Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma ndio wanaoshughulikia wafanyakazi ambao wameonewa kutoka katika mashirika au serikalini.

Mhe. Mgeni Hassan Juma alitaka kujua kuhusu wafanyakazi wanawake wangapi, wanaume wangapi. Kwa ujumla wizara ina wafanyakazi 1,113; kati ya hao wafanyakazi 240 ni wanawake na wafanyakazi 873 ni wanaume. Aidha, jumla wa wafanyakazi 307 walipandishwa vyeo ikiwemo wanawake 132.

Kuhusu suala la mafunzo mchanganuo wa idadi ya wafanyakazi waliopatiwa mafuno umeoneshwa katika kiambatanisho Nam.3 ukurasa wa 57 wa kitabu chetu.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad, Mhe. Marina Joel Thomas, Mhe. Hassan Hamad Omar na Mhe. Ashura Sharif Ali, wao waliulizia suala la Shirika la Meli kuuza *ticket* kwa bei ya juu na kinyume na utaratibu. Sisi suala hili kwa sababu ni shirika letu tutalifuatilia kwa karibu sana, lakini tunawaomba sana Wawakilishi, wananchi watusaidie katika kuwapata hawa watu. Limejibiwa hapa na Mhe. Naibu Waziri kwamba mtu mmoja ambae hata si katika Shirika la Meli lakini *ZMA* ilitoa barua kwa wanaomiliki meli na vyombo vya baharini wote na mimi nilipata nakala, kwamba yeyote atakayegundulikana katika maa-*agents* wanafanya ulanguzi wa tiketi atafungiwa moja kwa moja. Kwa hivyo, yule atakuwa kashapoteza, sio adabu nyengine anafungiwa kabisa kwa hivyo hana tena ruhusa. Kama wao Shirika la Meli au nani wamempa *agent* kuuza na akauza kwa ulanguzi linafungiwa moja kwa moja. Tatizo lililopo ni sawa sawa na hayo tunayozungumza siku zote hata mwanasheria anatwambia hapa, kwa Zanzibar hakuna mtu atakayekaa ushahidi akasema huyu ndiye tuliyemkamata sisi.

Mhe. Spika, kwa mfano tulipokuwa ofisi ile ya kule pwani kabla hatujahamia hapo Kisauni, walikuja vijana watano siku moja shababi wakanambia sisi tumeuziwa tiketi za magendo, tumekosa tiketi, nikawaambia basi nyinyi watu watano mnashindwa kumkamata mtu mmoja mkamleta hapa mkatizama tutamfanya nini, mnakuja kunambia keshandoka. Kwa hivyo, tushirikiane tuwapate, huyo mmoja tayari keshapewa *red card* wakitimia watano hawafanyi tena hao, lakini mtu akishakwenda ana haja ya safari akishauziwa basi anaona yeye keshapata anakuja kukunung'unikia tu tena. Tushirikiane tuwapate hawa vyenginevyo watatumaliza. Kwa sababu pesa hiyo hiyo mtu keshaitegemea anataka kwenda na kurudi anatoa ya kwenda tu.

Mhe. Hassan Hamad Omar alishauri na wengine kuhusu safari ya Pemba/Tanga. Waheshimiwa Shirika la Meli linasema hivi, kuhusu meli ya MV. Maendeleo kwenda Tanga shirika limezingatia ushauri huo, lakini kwa vile shirika lina meli hiyo tu moja ya abiria halitaweza kufanya safari za Tanga kwa sasa na kwa sababu ya kina kidogo cha maji kwenye bandari ya Tanga na kupelekea meli kusubiri maji yajae ndipo iweze kufunga au kuondoka. Kusubiri huko kutaathiri ratiba ya safari za meli huko Pemba na kupelekea usumbufu wa abiria. Na hili nimezungumza sio na Shirika la Meli tu, nimezungumza na wenye vyombo wengine vile vile *personally* na wamenijibu hivi hivi kwamba tatizo la Tanga ni bandari haitoshelezi kufunga vyombo kwa wakati chombo kinapofika, au kinataka kuondoka kikafunga, kikapakia abiria na kuondoka. Kwa hivyo, hili suala kidogo liko nje ya uwezo ila tutakapofika wakati Shirika la Meli lina meli zake mbili basi hiyo moja tunaweza tukai-*sacrifice* kwa sababu haitopangua ile ratiba ya ile meli.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu huo mguu naomba usipige kwa hili ninalojibu ni juu ya deni la Mji Mkongwe shilingi 40 milioni. Baada ya kufuatilia kwa kina suala la uingizwaji wa fedha za Mhe. Mbunge wa Jimbo la Mji Mkongwe wizara ilibaini kuwa Mhe. Mbunge huyo ametuma fedha hizo kupitia Baraza la Manispaa katika *account* ya wizara inayoitwa *revolving account*, ambayo hutumika kuingiza mapato ya aina mbali mbali, tarehe 18/ 06/2012. Kwa bahati mbaya fedha hizo zimeingizwa bila ya kuwa na nyaraka yoyote inayoonesha kuwa ni kweli Baraza la Manispaa limeingiza fedha hizo. Hata hivyo, wizara imekubaliana na Mhe. Mbunge wa Jimbo la Mji Mkongwe kufanya kazi ya ujenzi wa barabara hizo kwa thamani ya fedha zilizotolewa. Kwa hivyo, hiyo wizara ishakubali, sasa tuulize tu ni lini basi, lakini kukubali tushakubali. Sasa mtu akiwa na deni akikubali tena ananyongwa huyo, Hanyongwi.

Mhe. Ismail Jussa na Mhe. Nassor Salum Ali maelezo ya matumizi ya shilingi 50 milioni zilizotengwa katika mradi wa barabara zinazoingia katika mji wa Zanzibar. Fedha hizi zimetengwa kwa ajili ya ufuatiliaji wa upatikanaji wa

fedha kutoka kwa wafadhili mbali mbali kuhusiana na utekelezaji wa mradi huu ambao bado haujapata ufadhili. Hii ni *follow-up fund*.

Mhe. Ashura Sharif Ali ubovu wa barabara ya Mkwajuni - Kijini. Barabara hii ni miongoni mwa barabara sita za vijijini Unguja ambazo zinafanyiwa upembuzi yakinifu kupitia ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika. Hata hivyo, kwa kuzingatia kwa ujenzi wa barabara hizi utachukua muda mrefu hadi kukamilika kwake wizara kupitia Mfuko wa Barabara itaendelea kuifanyia matengenezo barabara hii ili iendelee kupitika mpaka hapo utakapofanyika ujenzi kamili wa barabara hiyo. Haya ndio majibu.

Mhe. Rufai Said Rufai, Mhe. Ashura Sharif Ali, Mhe. Hassan Omar Hamad kutolipwa fidia kwa baadhi ya wananchi sehemu zinazopita barabara. Mhe. Spika, kikawaida kabla ya ujenzi wa barabara kuanza wizara kwa kushirikiana na taasisi husika hufanya tathmini kwa ajili ya malipo ya fidia za mali za wananchi, zilizoainishwa katika maeneo ya ujenzi wa barabara. Kabla ya ujenzi wananchi wanastahiki kulipwa fidia, hulipwa fidia ili kuruhusu kazi za ujenzi ziendelee.

Kuhusu wananchi ambao hawakuwemo katika zoezi la awali la ulipaji fidia na kwa namna moja au nyengine nyumba zao zimeathirika baada ya ujenzi hutakiwa kuwasilisha malalamiko yao kupitia masheha wa maeneo yao. Kwa mfano, katika ujenzi wa barabara ya Kaskazini Pemba zilizogharamiwa kwa ruzuku ya Serikali ya Marekani kupitia Mfuko wa Changamoto *Millennia.*

Wizara imefanya tathmini na athari baada ya ujenzi wa barabara ya Mzambarautakao, Finya, Mapofu naendelea na tathmini ya barabara zilizobaki ikiwemo barabara ya Chwale/Kojani.
Kuhusu barabara ya Jendelele/Cheju/Kaebona, wizara imeanza kulipa fidia za nyumba ambazo eneo la kilomita nne za barabara zimelipwa fidia.

Mhe. Omar Ali Shehe serikali kuangalia namna ya kupunguza ajali za barabarani. Serikali inaendelea kuchukua hatua za kudhibiti madereva wote wanaofanya vitendo vinavyohatarisha usalama wa barabarani kwa kuongeza doria za Jeshi la Polisi na Usalama wa Barabarani. Hata hivyo, hili ni suala letu pamoja kuelimishana kwa sababu moja katika tatizo kubwa la hapa petu ni kwamba madereva hawafuati taratibu za uendeshaji gari barabarani.

Hivi karibuni katika *junction* tano za hapa Mjini Unguja tutaweka taa za kuongozea gari ili kuweza kupunguza hizo ajali za barabarani, alama ukiziweka zinapapachuliwa kwa hivyo tunawaomba sana wananchi waijali akhera yao. Kwa sababu ukipapachua alama za barabarani pakitokea ajali na wewe umo kuanzia siku ile mpaka *Yaumul-kiyama*.

Vile vile uwekaji minzani una wizara kama tano hivi, kwa hivyo hii ni moja tu, tunaomba na wizara nyengine zikija uweze kulisema neno hili. Wizara ya Fedha inahitaji minzani kwa sababu *ZRB* wanakusanya mapato, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko wanahitaji minzani. Kwa hivyo, hili ni jambo la kukaa pamoja kila wizara ikatizama kitu gani kitatoa ili kuweza kununua. Minzani ni muhimu sana lakini kwa bahati mbaya sana ni kwamba hapa hapana minzani hata moja, hata ya kupimia zile bidhaa zinazotoka pale bandarini hapana.

Mhe. Spika, naungana mkono na shauri lake lakini namuomba kwa sababu bajeti hazijesha alichukue vile vile kwa wizara nyengine alichangie na mimi nishazungumza.*(Makofi)*

Mhe. Ali Salum Haji nashukuru michango yake hasa kwa kutuunga mkono, alizungumza kuhusiana na kusimamia ipasavo usalama barabarani na magari kulingana na leseni za kibiashara zilizopewa. Wizara imepokea ushauri uliotolewa na kusimamia vyema usalama barabarani na itaendelea kufuatilia gari zinazokatisha njia na kuzichukulia hatua za kinidhamu.

Kuhusu leseni za magari ya kibiashara gari zote zimepewa leseni kufanya biashara ya usafirishaji wa abiria na mizigo kulingana na maumbile ya gari. Gari aina ya *carry* zimepewa leseni ya kupakia mizigo ya daraja la 'C' yaani mizigo ya nyumbani na sio kupakia abiria. Hivyo gari hizo zinapopakia abiria zinakuwa zinavunja sheria na kutakiwa kuchukuliwa hatua stahiki na vyombo husika.

Mhe. Hamza Hassan Juma gari za Bububu kukatisha *route;* suala la kukatisha *route* kwa mujibu wa Sheria ya Usafiri Barabarani na endapo kutakuwa na dereva atakayefanya ni vyema akaripotiwa polisi kwa hatua zaidi.

Mhe. Hassan Hamad Omar tatizo la usafiri wa baharini baina ya Pemba na Tanga nimeshalizungumza.

Tatizo la Meli ya *Azam Sin link* kuchelewa kuondoka bandarini Zanzibar. Mheshimiwa ikiwa hiyo meli itaendelea lakini ndio tushapata dosari mimi nilikuwa nasema hivi, kila aliyae hukamata kichwa chake. Kwa hivyo, meli ile kuchelewa hapa ni kwa ajili ya kuwasubiri wale ndugu zetu ambao wanakwenda huko huko Pemba wanaotoka Dar es Salaam, ili wasipate tabu ya kushuka meli wakaja wakaingia kwenye gari, wakenda nyumbani, wakakata tiketi nyengine, wakarudi tena kupanda chombo ndio wakenda Pemba.

Kwa hivyo, inawangoja pale pale gatini wanashuka boti wanaingia katika chombo wanakwenda zao Pemba. Sasa wewe ujitolee kwa sababu huwezi kuwasaidia wengine bila ya kujitolea nafsi yako, wewe ulioko pale unayengoja uone kwamba na wale ndugu zako wanataka vile vile kufika Pemba, lakini na wao kwa kupunguza gharama na kuwahi ule muda.

Kwa hivyo, sisi tunalishukuru sana suala hili la kuwangoja abiria wanaotoka Dar es Salaam ambao wataunganisha Pemba moja kwa moja ni suala muhimu sana. Kwa hiyo tunamuomba sana Mheshimiwa na wale ambao wana *idea* kama hizi wawavumilie wale wenzao. Watu wanaema maisha ni kuvumiliana bila ya kuvumiliana hamna maisha. Lakini kama nilivyosema tushaingia dosari isipokuwa tunamuomba Mwenyezi Mungu ampe huruma ndugu yetu huyu ayachukulie maneno haya ni maneno ya mjadala, kwa sababu hapa ni pahali pa kufanya mjadala na ukianza mjadala yule atasema hili, yule atasema lile halafu tunafahamishana tunakubaliana. Kwa hiyo tunamuomba alichukulie hili ili ndugu zetu waendelee na safari zao.

Mhe. Spika, nilikuwa na michango midogo hapa ya Waheshimiwa Wajumbe kwa jumla jumla; Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, jina halisi la Uwanja wa Ndege wa Unguja ni *Abeid Amani Karume International Airport,* na kwa Pemba unaitwa *Pemba Airpoti* na sio *Karume Airport* tena. Hayo ndio *latest,* nakupa.

Mhe. Hamza Hassan Juma kuhusu kuongeza eneo la kuwekea makontena na kuvunja mabanda ya mizigo bandarini Malindi. Wazo limepokelewa na kwa bahati nzuri nalo ni wazo la wizara na wazo la serikali. Kwa hivyo, sijui ameegema wapi lakini ameota ndoto. Kwa hivyo, tunakushukuru na wewe ku-*share idea* hii na ndio wazo la serikali.

Kuhusu kukodiwa kwa *crane* ya binafsi kwa bandari ya Mkoani naomba niseme hivi; kuna mfanyabiashara mmoja sitaki kumtaja alileta *crane* akataka kuikodisha, Shirika la Bandari likaichukua ile *crane* likaifanyia majaribio, lakini ni *spanner* mkononi. Kwa hivyo, wakasema wao hawaiwezi *crane* ile kwa sababu kila baada ya saa mbili uvunje kazi utie *spanner,* sasa huyo huyo anataka kuipeleka Mkoani ikiwa ni nzuri inatoka Dubai njoo tuzungumze. *(Makofi/Kicheko)*

Ahsante sana Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kutoa fursa hii nawaomba Wajumbe haya yafuatayo:-

Mhe. Spika, mimi ni binadamu na watendaji wangu nao ni binadamu, mapungufu tunayo mengi lakini na kazi tunafanya.

Labda suala la mwisho la Mhe. Ismail Jussa Ladhu ziara za Katibu Mkuu wangu. Safari alizofanya kwenda nje ni safari 10 katika kipindi hiki cha mwaka 2013/2014, aliyolipiwa na serikali ni safari moja na nusu, alizolipiwa na waliomuliaka ni safari nane na nusu na zote alikwenda safari za kazi, ikiwemo Uwanja wa Ndege wa Pemba Uturuki, Gati Uchina, Ujenzi wa Meli Korea, na kwengineko.

Kwa hivyo, mimi nasema hivi, wewe ni mtumiaji sana wa teknolojia, Katibu Mkuu kuondoka kwake anaondoka kile kiwiliwili tu, kwa sababu ya mtumizi wa teknolojia achilia mbali na watendaji, mimi na yeye tunazungumza kwenye kompyuta kila hatua anayofikia kule anakokwenda, kabla hajarudi hapa mimi nishajua alilolifanya, alilopata, alilolikosa na matatizo gani, huyu ndio Katibu Mkuu wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Namshukuru sana ahsante sana. *(Makofi)*

Nakushukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika, samahani naomba kwa heshima na taadhima baada ya yote hayo niwaombe wajumbe waipitishe Bajeti yetu hii bila ya vipingamizi, ili tuweze kuwatengenezea miundombinu. Naomba kutoa hoja Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa na sasa tuiamue, niwahoji basi wale wanaokubaliana na hoja hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa mwaka 2014/2015 wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe tuna shughuli kubwa leo ambayo kwa barua ambazo zimenipitia pitia hapa inaonekana karibu Wajumbe wengi tuna hamu ya kushiriki kwenye Ijitimai; ufunguzi wake ambao utafanyika leo Ijumaa mara baada ya kusali Ijumaa pale pale. Nadhani ni muhimu hilo kulifanya na kwa maana hiyo basi nafikiri tusitishe shughuli zetu ili jioni tuje kupitisha vifungu, kwa sababu hata tukiendelea na vifungu nadhani hatufikii hata nusu. Kwa hiyo, tuone kama jambo hilo Wajumbe mnalikubali basi Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais aje aseme maneno kidogo ili tuone kama Wajumbe wamekubali twende kwenye Ijitimai vifungu tufanye jioni.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa leo ni siku ya Ijumaa na kwa kuwa Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano tayari amefanya majumuisho ya maelezo mbali mbali ambayo Waheshimiwa Wajumbe walitaka kuelewa, na kwa kuwa muda ulio mbele yetu ni mfupi ambao hautoweza kuifanya shughuli hii na kumaliza kupitisha bajeti hii. Kwa hivyo, naliomba Baraza lako tukufu liweze kuahirisha nusu saa kabla ya wakati uliopangwa ili tuweze kwenda kusali sala ya Ijumaa na kushiriki mambo mengine ya kidini kwa siku hii tukufu ya Ijumaa ili baadae jioni saa 11 barabara tuweze kurudi tena na kuendelea na shughuli yetu.

Kwa hivyo, naomba nitoe hoja tuliahirishe Baraza lako hili mpaka saa 11 jioni leo. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

Basi baada ya hayo tusitishe shughuli zetu na tuahirishe kikao hiki hadi saa 11 jioni leo.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Saa 5:27 Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, nimesimama kwa kanuni ya 156 ya Baraza la Wawakilishi. Kifungu 156 kutenga kando kanuni. "Kwa idhini ya Baraza, yoyote kati ya kanuni hizi yaweza kutengwa kando kwa madhumuni mahsusi baada ya Mjumbe yeyote kutoa hoja kwa ajili hiyo."

Mhe. Spika, hiki chombo ni cha wananchi, na hoja tunayoijadili hapa ni ya wananchi. Kwa hoja tatu kwa Wajumbe Mhe. Spika, naona itakuwa ndogo na hatuwafanyii haki wananchi, angalau tungepata hoja tano mpaka sita. Kwa heshima na taadhima, hii wizara ni muhimu kwa wananchi. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Tunataka tufanyeje. Mimi nafikiri ni kweli kuna hoja nyingi lakini inategemea na majibu yatakayotoka. Kama majibu yatatoka mazuri hakuna haja ya kutayarisha hoja ziwe nyingi zaidi jambo ambalo litafanya shughuli zetu zichukue muda mkubwa zaidi. Sasa nisingependekeza hoja hii niilete kwa Wajumbe kwa kuamuliwa. Kwa hiyo mimi nadhani tuendelee na hali tuliyonayo, imani yangu tutakwenda vizuri bila ya kuleta

matatizo. Nitawaomba tu Mawaziri na Serikali kwa ujumla iwe inajaribu kutoa maelezo yanayofahamika kwa hoja mbali mbali za Waheshimiwa Wajumbe. Hilo moja.

La pili ambalo nalo halipendezi hata hiyo hoja ingekuwa tunataka tuiamue ina uzito wa kuiamua kutokana na watu tuliomo humu ndani. Na kwa sababu hizo hizo kuna tatizo vile vile la kuendelea na kazi kwa sababu Wajumbe waliomo kufanya maamuzi. Ingekuwa ni majumuisho angalau basi tungeweza kuendelea tu majumuisho yalikwishamaliza, hoja ilikwishaungwa mkono, ilikuwa nimwite Mhe. Waziri ili aweze kuomba Kamati ya Matumizi ikae. Lakini nikiwatazama Waheshimiwa Wajumbe tutakuja kufanya maamuzi yasiyokuwa halali. Na jambo hili ni tatizo kidogo kusema kweli. Ni mambo ambayo tunaambizana mara kwa mara kwamba tujitahidi.

Ingekuwa tunaendelea na mjadala basi tungeweza kuendesha kwa sababu tufanye maamuzi. Lakini kwa kuwa tunataka kufanya maamuzi kuanzia kwenye Kamati ya Matumizi tuna ugumu. Waheshimiwa Wajumbe hii ni nidhamu mbaya sana tunafanya. Mimi hainifurahishi hata chembe, wajibu wetu hatuutimizi vizuri. Maana haraka haraka Wajumbe nawaona sijui kama wanafika angalau 35.

Mimi nawatazama kwa macho tu, nilikuwa nakisia labda kwenye 35 kumbe ilikuwa tunapaswa tuwe angalau 41. Maana angalau tungekuwa 40 ningesema na mimi nipo, na mimi ni Mjumbe kwa mujibu wa katiba. Kwa hivyo ningesema hiyo *quorum* sasa imetimia ukihesabu na mimi.

UTARATIBU

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, huku tukiwa tunafanya jitihada ya kulisukuma hili gurudumu ili Wajumbe waweze kuingia, mimi tu nilikuwa na mapendekezo yanaweza yakatofautiana kidogo na Mhe. Jaku Hashim Ayoub lakini yanaweza pia yakafanana kwa upande mwengine.

Mhe. Spika, kama tulivyosema tulipokuwa tukichangia kwamba wizara hii kwa kweli ina hoja nzito sana. Mimi jana nilikuomba kama unavyomtafuta Mhe. Waziri wa Fedha wakati wa bajeti yake, nilikuomba umtafute na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ambae ni Kiongozi wa Shughuli zetu za Serikali hapa Barazani. Kwa hivyo tunakushukuru sana kwamba tangu asubuhi tunae, na sasa hivi tunae, na ninaamini kwa busara zake gurudumu hili anaweza akaturidhisha ili liweze kwenda vizuri.

Sasa katika hoja tutakazozizungumza katika vifungu na mimi nina rai. Kuna baadhi ya vifungu katika baadhi ya taasisi kasma zake au mafungu yake hayaonekani moja kwa moja kwenye vifungu. Pahala pekee ambapo tunaweza tukazungumza hoja hizo ni katika fungu la mipango, ambalo hata mimi niliyemnyang'anya Mhe. Waziri shilingi katika mshahara wake imo katika fungu hili. Na nilikosa fungu hilo huko mbele kote hakuna kifungu nitakachoweza kwenda kujenga hoja yangu ambayo ni ya msingi sana.

Sasa mimi nitaomba tu kwa wale watakaosimama katika fungu hilo la mipango, basi unaweza ukachagua moja kwa moja. Lakini kwa wale ambao hoja zao zitakuwa zina mafungu moja kwa moja huko mbele katika ibara mbali mbali, basi uwaombe radhi wasubiri katika yale mafungu. Na sisi wengine ambao njia yetu kwa hoja zetu nzito ni moja tu katika fungu hilo, basi angalau uweze kuturuhusu.

Sasa Mhe. Spika, kwa kuwa wewe ni mtu mzima, una busara, naamini huu ushauri wetu unaweza ukauzingatia. La kama itakuwa wengi hoja zetu hazina mafungu kule mbele, basi ile hoja ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub nafikiri itakuwa ya msingi sana, unaweza ukaruhusu fungu moja tukaweka kanuni kando badala ya hoja tatu zikaja hoja sita, ndio tunajenga.

Mhe. Spika, unajua nyumba ukitaka kujenga iwe imara lazima kila penye nyufa uvunje ujenge msingi uliokuwa imara. Sasa nadhani Wajumbe wameongezeka kidogo.

Mhe. Spika, katika kukusaidia kusukuma hili gurudumu lako naamini ushauri wangu unaweza ukauzingatia kwa busara zako. Ahsante.

Mhe. Spika: Nadhani tutapata Wajumbe sijui kama ni mmoja aliyebaki au vipi. Lakini Mhe. Makamu wa Pili wa Rais sikumtafuta, isipokuwa kwa ratiba yake leo ilikuwa anaingia kazini na namshukuru kwamba amewahi.

Haidhuru pengine amesikia unaponguruma humu ndani lakini kwa kweli sikumtafuta. Ilikuwa ameniaga kwamba tarehe 13 atakuwa tayari yupo kazini. Tunamshukuru sana kwa kuchukua hatua hiyo.

Nafikiri Wajumbe sasa wanakaribia, ili tu waliopo nje waingie ili tuendelee na kazi.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali hotuba ya bajeti ya Wizara, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi vya wizara yangu.

Kamati ya Matumizi

Fungu 26	**-**	**Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano**	
Kifungu 0301	-	Ofisi Kuu Pemba	62,000,000
Kifungu 0701	-	Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara	10,000,000
Kifungu 0801	-	Idara ya Usafiri na Leseni	364,000,000
Jumla ya Fungu			**436,000,000**

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Najua kama mapato, na swali langu lipo kwenye mapato, na najua ninachokiuliza.

Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Maana nilikuwa natafuta hicho kifungu kinachohusiana na suala lile nililomuuliza Mhe. Waziri mapato yanayotokana na *Zantel* pamoja na mashirika mengine ya Muungano kama *TCRA, TMA, TCAA.* Mimi sikuridhika na jibu lake kwa sababu wakati anajibu ameeleza kwamba mapato yale wao wanashughulikia kiufundi, mapato yale yanaelekea Wizara ya Fedha au yanaingizwa katika Wizara ya Fedha zaidi.

Kwa uchache kabisa ambacho nilikuwa nategemea Mhe. Waziri angejibu ni kwamba tunapata *allocation* ya kiasi gani. Najua zitaweza ku-*appear* kule kwa Mhe. Waziri wa Fedha, lakini hatuzioni kule kwa Waziri wa Fedha *itemize* kwa sababu wizara inayohusika na masuala haya ya mawasiliano Zantel, *TCAA* ni hii.

Hata kama wanashughulikia kiufundi kwa uchache kabisa jibu lake angetwambia kwamba kwa *share* zetu au *dividend* zetu, maana Serikali ina asilimia 18 ya hisa zake ndani ya *Zantel*. Na *Zantel* thamani yake sasa hivi nadhani kwa haraka haraka ni dola milioni 400. Kwa hivyo, kwa hisa za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar peke yake ndani ya *Zantel* ni sawasawa na bajeti ya wizara hii ya miaka mitatu peke yake hisa ya *Zantel* tu. Sasa nilichokuwa nauliza mimi Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa nataka kujua angalau kwa uchache angetwambia *allocation* inayopatikana. *Allocation* tu, sio lazima kile anachopokea. Kwa sababu kwa hisa hii angeweza kuweka mahesabu yake vizuri kwa kutwambia kiasi gani anapata. Sasa mimi sikuridhika na jibu lile la mapato alilolitoa Mhe. Waziri. Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. Wakati nilipokuwa nikijibu suala hili nilisema ule ukweli wa mambo na *structure* ilivyo katika uendeshaji wa haya mashirika. Katika uendeshaji wa haya mashirika kuna *shareholder's meeting or committee* ambayo Mjumbe wake ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha. Kwa hivyo, mapato yote na kila kitu kinachohusiana na mashirika haya yanaunganishwa na Wizara ya Fedha, hayaunganishwi na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, kama ni kupitia *ZRB* au vyenginevyo.

Kwa hivyo, sisi hatuhusiki na mapato ya aina yoyote yanayotokana na vyombo hivi. Na nilisema kwa ujumla wake, nilianza *Zantel*, nikaingia vyombo hivi vya Muungano *TCRA, TCAA* na *TMA*; hivi sisi hatuhusiani moja kwa moja kimapato, tunahusiana nao kiutendaji katika shughuli zetu kiufundi. Sasa sisi tutajibu suala ambalo hatulijui. Ndio nikasema kwamba watu wa Wizara ya Fedha ndio wanaohusika na kujibu masuala ya kifedha yanayotokana na mashirika haya.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, labda kwa kuongeza yale aliyoeleza Mhe. Waziri, kwamba hili si suala la matakwa ya Mhe. Waziri, ni suala la sheria. Sheria Nam. 4 ya mwaka 2002 inayohusu mitaji ya umma

"Suala lolote la uwekezaji na biashara ya hisa za Serikali, ni suala la Kamishna wa Mitaji ya Umma ambae yupo chini ya Wizara ya Fedha."

Kwa hivyo, kumtaka Mhe. Waziri kwamba ajue *allocation* yetu, ajue *dividend* tunapata kiasi gani, hiyo ni *mandate* ya Kamishna wa Mitaji ya Umma. Kwa maana hiyo, hiyo ndio *mandate* ya Waziri wa Fedha. Na bahati nzuri Waziri wa Fedha hajaja kuleta bajeti yake. Kwa hivyo, nadhani tutapata muda mzuri. Lakini kumlazimisha Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano kufanya kazi ambayo chini ya Sheria Nam. 4 ya mwaka 2002 kapewa Waziri mwengine, nadhani ni kumtwika mzigo ambao anaweza akasema taarifa ambayo sio sahihi.

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mhe. Waziri, na namshukuru Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa masawazisho hayo. Lakini ninachotaka kusema mimi Serikali ni moja, nilichokiomba mimi ni *figures* inayotoa *allocation* au inayopatikana katika mapato kutokana na *Zantel*. Na wengine nimewataja kama *TCRA, TMA, TCAA.*

Mhe. Mwenyekiti, mimi nina gazeti hapa ambalo linasema *Zantel* kama mhusika mkuu amekopa dola milioni 100, hili hapa. Na huku tunaona kwamba Serikali yetu ina hisa nzuri si ndogo asilimia 18. Katika thamani ya *Zantel* ya dola milioni 400 ina maana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar takriban ina dola milioni 75. Milioni 75 ni bajeti takribani ya miaka mitatu au zaidi ya wizara hii, ukipiga hesabu za haraka haraka.

Sasa mimi ninachokiona kwamba hizi *shares* za *ZANTEL* ambazo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zinaning'inia. Kwa sababu pale ndani kuna *board members* wawili wanaotoka kwenye Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Wa kwanza ni Katibu Mkuu Wizara ya Mawasiliano anaingia kama Mjumbe wa Bodi na wa pili ni Katibu Mkuu Wizara ya Fedha.

Sasa serikali ni moja, kikao cha *board* kile ni kimoja, *papers* za *board* zinazotolewa ni moja, *financial technical* zote zinakuwemo humo humo, mambo ya kiufundi na mambo ya kibiashara na mambo ya kifedha, yote yanakuwa kwenye *paper* hiyo hiyo.

Watashindwaje kutoa jibu ya kwamba *dividend* au *shares* za Serikali ya Mapinduzi ndani ya *ZANTEL* ni kiasi fulani na zinapatikana kwa njia fulani. Zile hazipiti kwenye Muungano kwa sababu hizi nyengine za *TCRA, TMA* na *TCCA,* Mheshimiwa alisema kwamba zinapitia kwenye mfuko mkuu wa muungano, zinakwenda *BOT*, halafu ndio zinakuja Wizara ya Fedha.

ZANTEL haipo hivyo. Sasa katika serikali hii kupata jibu hilo la kwamba fedha zinazopatikana ikiwa Wizara ya Fedha, ikiwa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, wote hao *board members* wao wanaingia na *figures* hizi wanaziona.

Kwa hivyo naomba tupatiwe hiyo *figure* Mhe. Mwenyekiti, sio kama jibu liondoshwe tu kwa kusema kwamba hii itafika wakati wa Wizara ya Fedha itasemwa, hapana. Anatakiwa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ajue kwa sababu yeye ndio *responsible*, mbali ya kuwa *responsible* wa mitaji ya umma lakini ni *responsible* kwa *shares* zile kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, wakati *TCRA* inatoa leseni ya ku-*operate* ile *operator* imetoa kupitia Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi ya Zanzibar, na wakati huo Waziri wa Mawasiliano alikuwa ni Mhe. Aman Abeid Karume na Rais alikuwa ni Salmin Amour Juma ndipo ilipotolewa leseni ile.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, hapo bado sijaridhika. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Eeh! una maelezo zaidi Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, muda mfupi uliopita tulikuwa tunakuita Spika. Sasa tunakuita Mwenyekiti. Mtu ni wewe, hujabadilika jina, umebadilika cheo. Umebadilika cheo kwa sababu ya Kanuni zetu. Hapa tunachozungumza ni hoja ya bajeti ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Miundombinu haihusiki na suala la mapato ya serikali katika uwekezaji uliofanywa na serikali katika suala la kibiashara.

Anachosema Mhe. Mahmoud Thabit Kombo kwamba serikali ina asimilia 18 ya *shares*, tunalijua na mimi ndiye niliye-*negoatiate* mpaka tukapata hiyo asilimia 18. Lakini hisa si mali, hisa ni *liability* ya kisheria. Ni mali pale inapokuwa ile biashara yenyewe imetengeneza faida.

Sasa la kwamba tuna asilimia 18, ile ni *liability* yetu ya kwamba tutakapotokea *ZANTEL* ika-*wind up*, tuna wajibu wa kulipa hizo dola, lakini na pia itakapotokea ikafanya faida tuna haki ya kupata faida kwa mujibu wa kiwango hicho.

Sasa Sheria ya Mitaji ya Umma Nam. 4 ya 2002 imesema wazi, "Mwenye dhima na dhamana ya kusimamia hisa za serikali na mapato yake ni Kamishna wa Mitaji ya Umma aliyepo chini ya ...

Kwa hivyo, serikali sio kwamba tunakataa kutoa lakini tunasema hapa tunajadili hoja ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ambayo haihusiki na suala la biashara ndani ya *ZANTEL*, wala haihusiki na biashara au na mapato ya serikali ndani ya *TCRA*.

Hiyo itakuja hoja hatujafika kwenye hoja hiyo Mhe. Mwenyekiti, ndio tunalozungumza. Likifika hilo akitaka maelezo atapewa.

Mhe. Mwenyekiti: Maelezo ya ziada Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, kwanza ninamshukuru sana Mhe. Mwanasheria Mkuu.

Mimi nilikuwa na moja tu la nyongeza kumsaidia Mhe. Mahmoud Thabit Kombo; kwamba katika hichi chombo cha *ZANTEL* kuna vyombo viwili. Kuna Bodi ya Wakurugenzi ambayo ndio anaingia Katibu Mkuu wetu, lakini kuna chombo chengine kinaitwa *Share Holders Meeting.* Yule Katibu Mkuu anayetoka Mawasiliano haingii, anaingia wa Wizara ya Fedha tu.

Sasa huko ndiko hivyo anavyozungumza Mhe. Mwanasheria Mkuu. Kwa hivyo, sio kwamba sote tuna taarifa za aina moja.

Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru.

Mhe. Mwenyekiti: Eeh! Mhe. Mahmoud Thabit Kombo.

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Mhe. Mwenyekiti, ahsante. Kwanza naomba nimkumbushe Mhe. Mwanasheria Mkuu *principles* za *accountancy*, *shares can be liability* kama ulivyosema, *also shares can be an asset*. Hizo ndizo *principles* za *accountancy*. Kwa hivyo yote mawili yanawezekana, inawezekana ikawa *liability* na pia inawezekana kuwa *asset*, inategemea itaingia upande gani katika *balance sheet*.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi ninahisi ninaonekana kama ninahoji wakati mimi ninaitetea serikali kwa *shares* zake. Ninatetea serikali kwa thamani yake ambayo inaning'inia haijulikani. Ninaitetea serikali yetu na wananchi wetu ambao wana fedha nyingi kupitia hisa zao, ikiwa kupitia sheia Nam. 4 ya Mitaji ya Umma ikiwa kupitia Wizara ya Fedha, ikiwa kupitia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, zile ni *shares* za serikali, *it means indirectly* zile ni *shares* za wananchi wa Zanzibar. Sasa mimi ninaitetea wizara hii. Ninashangaa kwamba wizara, Waziri pamoja na Mhe. Mwanasheria Mkuu wana-*defend* wakati mimi ninawatetea wao kwa *shares* za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. (*Makofi*).

Ninachotaka kuuliza hivi hata kama ipo mitaji ya umma au Wizara ya Fedha, tunashindwa kupewa hiyo *figure* tu, tupewe kwamba thamani ya *shares* ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ndani ya *ZANTEL* ni kiasi fulani na *dividend* yetu.

Kuna wakati walinipa wale *dividend* na walionesha kwenye televisheni na walitoa *cheque* na *dividends* zetu mara ya mwisho tumepokea kiasi fulani au thamani yake ni kiasi fulani sasa hivi, ili tujue kwa sababu hizi *shares* zinaonekana hakuna *censor ownership*, hakuna mmiliki mpaka sasa hivi, tunarushiana tu mpira. Hii ni thamani ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia leseni ambayo imezawadiwa kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Mwenyekiti, ningeomba tupewe *figure* hiyo, ninaitetea serikali kwa thamani yake ndani ya *ZANTEL*. (*Makofi*).

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, mimi sijafahamu hasa kwamba Mhe. Mahmoud Thabit Kombo hajatuelewa au hatujamuelewa yeye au hajatuelewa sisi. Lakini ninadhani jibu lipo wazi, na ninaamini yeye kwa alichokieleza hapa kwamba ni mtaalamu zaidi wa hiyo biashara wa *accounting* pengine na uchumi na pengine hiyo na *industry* yenyewe hiyo ya mawasiliano.

Anaelewa vizuri kwamba *dividend* ukiwa *shares* haina maana moja kwa moja unapata *dividend*. Unaweza ukapata *loss*. Na kupata *dividend* inategemea na *dividend* na *policy* ambayo inawekwa na *Share Holders Meeting*, ndicho hicho alichokizungumza Mhe. Waziri, kwamba *dividend* inatolewa kulingana na *share holders, dividend policy* inayowekwa katika *share holders meeting*.

Wanaweza wakaamua kwamba badala ya kulipwa *dividend*, wapate *issue pairs* zaidi au *right issue pairs* za zaida. Wanaweza wakaamua wakazi-*invest* zaidi, wanaweza wakaamua kitu chochote kile. Sasa hizi taarifa haitegemei tu kwamba wewe una asilimia 18, unapata kiasi gani. Ndio maana tukasema hebu asubiri katika ile mamlaka iliyohusika, na kwa sababu hapa hatujadili hoja ya mapato ya serikali kutokana na uwekezaji wake.

Kwa sababu hili pamoja na kwamba imeekezwa katika sekta hii, lakini bado ni biashara ambayo inafanywa na serikali. Imetokea tu kwamba biashara hii inafanywa katika kampuni ambayo inahusika na mawasiliano, haina maana kwamba Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano inahusika na uwekezaji ule moja kwa moja na faida inayopatikana na hasara inayopatikana.

Suala la kwamba kwa mfano inapata kiasi gani au haipati kiasi gani. Mimi akiniuliza tunaweza tukampa hiyo *figure* labda tuliipata kwenye gazeti. Lakini maelezo ya kwamba kwa nini hatupati *dividend* pengine *dividend policy* hii, hilo ni suala litajibiwa katika hoja inayohusu wizara inayohusika na uwekezaji wa serikali katika makampuni mbali mbali ambayo ni Wizara ya Fedha, hoja yake haijafika hapa. Ndio tunachozungumza hapa.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi ninadhani ukubali tu kwamba hapa hilo jambo hatuwezi tukalipata. Kwa sababu muhusika wa kutoa taarifa hizo rasmi hayupo na ni Waziri wa Fedha hayupo. Mhe. Waziri angeweza kupata kitu hicho ninafikiri isingekuwa dhambi akizipata rasmi kutolewa si dhambi hata kidogo.

Sasa tutasimama tunakaa, tutasimama tunakaa, juu ya jambo ambalo kwa hapa hivi sasa na kutokana na maelezo yaliyotoka hapa aliyosema Mhe. Mwanasheria Mkuu na Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, haliwezi kupatikana bila ya kuwepo Waziri wa Fedha.

Ukweli wa mambo, hapa ndio penye umuhimu kwamba serikali iwepo. Umuhimu wa kuwepo serikali katika chombo hichi muda wote ni huu, kwa sababu tunafanya kazi kwa pamoja. Sasa mimi labda kwa niaba ya Wajumbe wote kwa jumla, tumuombe radhi Mhe. Mahmoud Thabit Kombo kwamba hili jambo akubali aje alipate baadae kwa maandishi, lakini kwa hapa inaonekana haliwezi kupatikana.

Lakini kimsingi ni kitu ambacho ninaamini kabisa kwamba mahesabu yake iwe kwenye hiyo Idara ya Mitaji ya Umma lakini kwa ujumla wake itakuwa ni kitu ambacho kinaeleweka. Hata hivyo, *dividend* kwa mara ya mwisho ilitolewa ngapi pia inaweza kupatikana, lakini Mjumbe sahihi wa kutoa taarifa hiyo hapa ni Waziri wa Fedha ambaye hayupo. Sasa nimuombe radhi atuachie Mhe. Mahmoud Thabit Kombo hilo jambo. Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini labda anazo taarifa. Ninajua alikuwa Waziri wa masuala ya fedha kwa muda mrefu karibu.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli ninafanya mawasiliano ya haraka haraka, nimepata fununu kidogo labda ninaweza kumsaidia Mhe. Mahmoud Thabit Kombo.

Mwaka 2007/2008, serikali ilipata gawio la kwanza zipatazo dola za Kimarekani laki mbili na hamsini elfu(250000). Mara ya pili, tulipata gawio la pili kama dola za Kimarekani laki moja arobaini elfu(140000). Hizo ndizo *latest figures* tulizonazo, sijapata tokea niwe Waziri wa Fedha sina *update*, lakini hizo nimewasilishiwa haraka kwa mtandao sasa hivi kutoka Wizara ya Fedha.

Hivyo ndivyo ninavyoweza kusaidia. Tumepata mara mbili gawio kutoka Zanzibar. La kwanza ni *two hundred and fifty thousands* mwaka 2007/2008 na la pili ni dola laki moja arobaini elfu. Hicho ndio *alhamdulillah* SMZ tulichopata.

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi nidhani nikubaliane na ombi lako ulilolitoa Mheshimiwa, kwa sababu ombi lako wewe kwa utu uzima wako, kwa heshima ninayokupa, kwa hekma na busara zako ni utumwa ndani ya nafasi.

Kwa hivyo naomba nikubaliane na ombi lako. La sivyo ningemuomba Mhe. Waziri sasa hivi aliyesimama atuletee *auditing account* za *ZANTEL* za miaka mitatu iliyopita ili nimthibitishie jinsi gani Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaibiwa pesa zake. (*Makofi*).

Lakini naomba na hizo *auditing account* ni *public documents* kwa sababu ile ni *public intensity* na zinafanywa na *bright copper copper* lakini naomba tusifike huko kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, wewe umeshatoa kauli yako.

Lakini kwa *figures* hizi alizotaja Mhe. Waziri za dola laki mbili na nusu na dola na dola laki moja arobaini, hizo ni sawa sawa na kadi zinazouzwa kwa wiki tu za *ZANTEL*. Hivyo, Mhe. Mwenyekiti, naomba nikukubalie wewe hilo ombi lako la mwanzo, na nimekubali Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Tunashukuru lakini pia hii ni *concern* kwamba tuwe makini na vitu hivi ili serikali inafuatilia kila pale haki ya serikali basi iwe inapatikana kikamilifu kwa mahesabu kamili. Tunakushukuru Mhe. Mahmoud Thabit Kombo. Tuendelee.

Jumla ya Fungu Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano **Shs.436,000,000.00**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 26 - WIZARA YA MIUNDOMBINU NA MAWASILIANO

Kifungu 0301 Afisi Kuu Pemba Shs.1,362,501,000.00
Kifungu 0401 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti

Mhe. Mwenyekiti: Ninajaribu kutafuta ile buti ya mwanzo ilikuwa wapi. Haya inaonekana wanakubaliana Mhe. Asha Bakari Makame, baadae atafuata Mhe. Ismail Jussa Ladhu, tuendelee na hao kwanza. (*Kicheko*).

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kukushukuru wewe lakini pia nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri wa wizara hii kwa jinsi alivyotujibu vizuri, maana mtu lake umpe. (*Makofi*)

Lakini Mhe. Mwenyekiti, ninazuia fungu hili kwa sababu ya Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Mimi bado pamoja na mazungumzo yote yaliyozungumzwa Waziri wa Fedha na nani, wakasimama mawaziri. Bado suala la uwanja wa ndege wa Pemba sijaridhika kabisa.

Kwa sababu Waziri ndio kanichafua kabisa alipokuja kuzungumza mazungumzo yake. Maana kipindi kilichopita Waziri wa Uwezeshaji wa Wanawake, Watoto na Vijana aliambiwa hafai, huyu ndio hafai hasa. (*Makofi*)

Kwa sababu ninarudia tena, huyu ndio hafai hasa, kwa sababu mimi simwambii Rais kwamba kakosea, lakini hafai. Maana alikuwa *backbencher* huyu alituadhibu sana kwa uwanja wa ndege. Ilifika hadi akasema kwamba tutumie vibatari na mafuta atasaidia yeye, huyu Waziri huyu.

Sasa na mimi ninawaomba Waheshimiwa Wawakilishi utuchangie katika hayo mafuta ya taa kule tuashe vibatari uwanja wa Pemba. Sasa mimi bado sijaridhika na uwanja wa Pemba, kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, hii ni hadithi ya

Alinacha. Kwa sababu si miaka hii tu uwanja wa Pemba, ni miaka mingi sana na wewe Mhe. Mwenyekiti, ni shahidi. (*Makofi*)

Kwa sababu wewe ndiye Spika wetu ambaye umeishi miaka mingi katika Baraza hili. Kwa hivyo mimi bado sijaridhika na jawabu, kwa sababu wameona hii ni bajeti, sasa wametueleza maneno Waziri wa Fedha.

Waziri hivi karibuni alitwambia mambo wewe usiwe na wasi wasi Mhe. Asha Bakari Makame ukienda Pemba taa zitawaka. Sasa kwa nini Mhe. Waziri asitwambie kwamba kwa sababu ya ughali wa taa hizi za Pemba tumeona tufanye moja, mbili, tatu, nne, tano, leo anakuja kutwambia Waziri wa Fedha. Mimi sikubali na silipitishi fungu hili, sikubali Mhe. Mwenyekiti. Nataka jawabu rasmi.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mhe. Asha Bakari Makame kama nilivyokuwa mimi akawa na uchungu wa kile kiwanja cha ndege cha Pemba.

Pili, katika maelezo yetu Mhe. Mwenyekiti, tulisema kwamba tulipanga ndani ya bajeti kuweka taa katika kipindi hiki cha bajeti 2012/2013. Hali iliyoelezewa na Waziri wa Fedha inaonekana, tulikosa pesa zile na ikaonekana dalili kabla ya kufika hapa kuja bajeti ya pili, dalili ya kuwa pesa hizi hazitopatikana ilionekana.

Kwa hivyo, kupitia wizara yetu serikali ilianza mchakato mpya wa kufuatilia uimarishaji wa uwanja wa ndege wa Pemba, ikatoka timu yetu kuzungumza na benki ya *Exim* ya Uturuki na Kampuni ya Uturuki ya ujenzi, kwa sababu kwa mujibu wa hali zilivyo sasa hivi duniani, ukitaka kukopa basi sharti lake na wao waingie katika mambo yale. Kama tunavyofanya kwa China, *Exim Bank* ya China na Kampuni za China. Kwa hivyo, utaratibu ule ukashughulikiwa katika kipindi chote hiki, nimekuja na *documents* zilizoandikwa si za kubuni, na kila mmoja anaweza akazichukua akasoma, hii inaelezea *plan* ya uwanja wa ndege na hii inaelezea *feasibility study* ambayo imetolewa tarehe 15 Mei 2014, imeletwa hapa *document* hii ya *feasibility study* wataalamu wetu waipitie, halafu wataalamu wa Uturuki watakuja wafanye majadiliano na kukubaliana kitakachotakiwa kufanywa.

Vile vile tulisema katika utaratibu huu wa utanuzi wa uwanja wa ndege wa Pemba. Kwanza masafa ya urefu yatatoka kutoka mita 1,500 mpaka 2,300 zitakazotua sasa ndege za *boeing* 737/200. Pia utatanuliwa upana kutoka mita 30 mpaka 45, kutajengwa jengo jengine jipya la *terminal*, lile liliopo litatengenezwa na *fence* itajengwa. Hii hapa *project* ni mkopo wa *Exim Bank*, na humu kuna barua ya uhakika ya *Exim Bank* imeshakubali kukopesha kwa mradi huo, lakini sasa sio kuwa jambo litafanywa *over night*, ndio nasema kutokana na ukosefu wa fedha zilizokuwepo kwa urahisi, serikali tulianzisha mchakato huu ili kuona kwamba hii *project* inafanyika.

Kwa hivyo, uwanja ule mbali ya kutiwa taa tu, basi utajengwa hasa sasa Mhe. Asha Bakari, tafadhali tukubalie uwanja utajengwa. Kama utakuwa hai na mimi nitakuwa hai tukijaaliwa, basi itakavyokuwa vyovyote nitakupa tiketi ya kwenda kutia jiwe la msingi. (*Makofi)*

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na yote, kwa sababu Mhe. Waziri huko nyuma liliulizwa swali, na ndio maana nikasema hivyo. Kwa hivyo mimi sikubaliani na yeye kabisa, alinihadaa kwa hizo *documents* zake alizonazo na ikafika mwaka mwengine wa keshokutwa akaja kuniambia *Exim Bank* sijui, hatukupata nini na nini. Mimi nataka serikali itoe tamko, nitamuomba mkuu wa serikali hapa atoe tamko rasmi ili na wananchi wasikie, wajue kwamba ule uwanja wa ndege Pemba utajengwa sasa, mambo ya Alinacha siyataki.

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano kwa maelezo aliyoyatoa. Mhe. Spika, suala la ujenzi wa uwanja wa ndege wa Pemba, umo ndani ya ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010 mpaka 2015.

Kwa hivyo, kitu kilichomo ndani ya ilani ya Chama cha Mapinduzi ni lazima kitekelezwe. Maelezo aliyoyatoa Mhe. Waziri ni sahihi, kwamba Kampuni ya Uturuki tayari imekubali kujenga uwanja na sio kuweka uzio tu na taa, ingawa nilimsikia Mhe. Makame Mshimba Mbarouk akisema kwamba tayari ana maboksi ya mishumaa nje, lakini sijaona sherehe ya kumkabidhi maboksi hayo Mhe. Waziri.

Lakini niseme kwamba ni kweli kabisa kwamba Kampuni ya *Exim Bank* ya Uturuki imekubali kuchangia uwanja ule na sio tu kuweka taa na uzio, lakini kujenga kiwanja kizima, pamoja na kupanua kiwanja na kurefusha zile *runway*. Tayari *Exim Bank* imekubali kutoa mkopo ule kwa Kampuni ya Uturuki. Hivi karibuni nilikuwa Pemba,

nilithibitishiwa na Mkuu wa Kusini Pemba, kwamba wataalamu wa Kampuni ya Uturuki walikuwepo Pemba kufanya uchunguzi na wamemaliza uchunguzi.

Kwa hivyo, Mhe. Asha Bakari usitie wasi wasi, mimi natoa kauli hiyo kwa niaba ya serikali, kwamba uwanja wa Pemba utajengwa, kwa sababu umo ndani ya ilani ya Chama cha Mapinduzi, na yanayowekwa ndani ya ilani ya Chama cha Mapinduzi siku zote huwa yanatekelezeka na hili litatekelezeka. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, roho yangu sasa hivi imeridhika kwa sababu serikali kamili imetamka. Kwa hivyo, Mwenyezi Mungu atusaidie ili tuzipate hizo fedha na Mwenyezi Mungu atupe uhai mimi na Mhe. Rashid Seif na wengine wote, ili siku ya kufunguliwa kiwanja hicho niende nikatie jiwe la msingi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Nilitamka Mhe. Ismail Jussa eeeh.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi hii na mimi nilizungumza mambo mengi, lakini kwa hapa naomba nisimamie suala moja muhimu sana ambalo mwaka jana nililitolea maelezo marefu sana, kuhusu suala la ujenzi wa *terminal II, terminal* mpya ya uwanja wa ndege wa kimataifa wa Abeid Aman Karume hapa Unguja.

Mhe. Mwenyekiti, nilipotaka maelezo nilijibiwa, niliyasikiliza kwa kina sana na kwa utulivu majibu aliyoyatoa Mhe. Waziri wa Fedha na baadaye kwa kiasi fulani yakarejewa na Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, lakini Mhe. Mwenyekiti, nasikitika kusema kwamba bado chombo chako hiki hakitaki kuambiwa ukweli na serikali au serikali haijataka kusema ukweli juu ya chombo hiki.

Mhe. Mwenyekiti, nimeshtuka zaidi na ndio maana nimelazimika kusimama tena sasa hivi, kwa sababu majibu ya Mhe. Waziri aliyoyatoa asubuhi yanaonekana dhahiri kwamba Baraza hili linadanganywa. Mhe. Mwenyekiti, nilitoa hoja katika mchango wangu, kwamba lile ambalo mwaka jana tulilisema la uwanja ule kubakia pale pale na kufanywa marekebisho yanayotaka kufanywa, katika muda mfupi ujao itakuja kuitia hasara serikali badala ya kuwasaidia wananchi, lakini suala la kulihamisha kwa maana ya kulifungua na kulirudisha nyuma na kulijenga upya, lingekuwa na faida ya muda mrefu na gharama zake zingefika kama hivi ambavyo sasa hivi zimeshafika kwa kulifanyia marekebisho ya lile jengo lililokuwepo.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, katika ripoti iliyosomwa mwaka jana hapa wataalamu wa *EDPi* washauri waelekezi walisema kwamba kuliondosha na kulirudisha nyuma kungeongeza gharama ya ziada ya baina ya dola milioni 9 mpaka dola milioni 13 dola. Kwamba ukichukua dola milioni 114,350,000 tukajua kwamba zingetumika kwa kuzibakisha pale pale kufanyiwa marekebisho, ukiongeza hizo maana yake ni dola 127 milioni. Tayari kwa maelezo waliyotuambia wizara katika kamati na leo Mhe. Waziri alipokuwa akijibu, imeonesha kwamba tumeshafikia pale, kwamba tumeshafika dola milioni 128. 5 tumeshazidi kuliko zile ambazo tulizidi mwaka jana, lakini zaidi nimesikitika, na nimalizie hoja yangu ili nipate majibu, ni kwamba mwaka jana na *hansard* ninayo Mhe. Mwenyekiti, walisema Wajumbe wengi. Tunachosikitika ni kwamba serikali kila siku majibu yake yanabadilika, hiyo haioneshi kama serikali inasema kweli humu ndani.

Mwaka jana Mhe. Waziri, pamoja na kwamba ripoti ya wataalamu ilisema dola milioni 128, yeye alituambia itafika dola milioni 140 na *hansard* yake ninayo. Leo anatuambia likivunjwa lingefika dola milioni 170. Sasa wao wenyewe hawatuambii kweli, wanatukuzia gharama ili tutishike na hoja ya kuliondosha pale, ambapo kulibakisha pale ni hasara kubwa zaidi na ingekuwa sio muda basi ningeyasoma hapa yale ambayo yameelezwa.

Kwa hivyo, nataka maelezo Mhe. Mwenyekiti, kwa nini serikali kwa sababu tu ya kutaka kuinusuru Kampuni ya kibiashara ya Kichina, ambayo kwa sababu ilifanya makosa makubwa pale, kulivunja kwao kutaharibu taswira yao, tunataka kuinusuru ile na tunataka kulazimisha kulifanyia marekebisho, hali ambayo kwa gharama sasa hivi imeshatufikisha kule kule ambako mwaka jana tuliambiwa zitafika dola milioni 128 jengo likiwa pale pale, lakini zaidi huku tukidanganywa kila siku kwa kukuziwa gharama ambazo sio za kweli. Je serikali inataka kuwaambia nini wananchi wa Zanzibar kuhusu suala hili Mhe. Mwenyekiti?

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Mwakilishi azingatie mambo yafuatayo. Tulipokuwa tunataka kufanya ujenzi mpya baada ya ujenzi kusita, wizara ilipata ruhusu ya serikali kumuajiri Mshauri Mwelekezi, alikuwa yeye afanye kazi mbili.

Kwanza kutushauri lile jengo lilivyo tulifanye nini ili liweze kutumika, hiyo ilikuwa ni *clear* kwa serikali, kwa sababu serikali ilikwishaamua kwamba *alternative* ya serikali ni kulibakisha jengo. Sasa alipokuja Mshauri Mwelekezi alitakiwa atoe ushauri, sio kulivunja ili tuweze kulitumia tufanye nini. Baada ya hapo atutayarishie hiyo michoro tufanye nini na aweze kuipasisha yeye baada ya kushauriana na Mkandarasi.

Vile vile alikuja na miundo minne, miwili ni kulibakisha lile jengo, jengo linaweza likabakishwa pale pale, lakini tukafanya marekebisho haya na haya. Kama tunaona kwamba ile hatuiwezi basi tunaweza sasa tukalivunja. Mhe. Mwenyekiti, ikiwa ni kulivunja basi tusingehitaji Mshauri Mwelekezi, kwa sababu tungeweza kwenda kuvunja tukajenga jengine, ya nini kutafuta Mshauri Mwelekezi aje atuelekeze kwamba tulivunje. Hilo ni la pili.

Suala la tatu Mhe. Mwenyekiti, ni kweli huyo Mshauri Mwelekezi alisema kwamba gharama yake ya kulivunja itachukua kama dola milioni 9 mpaka dola milioni 11, lakini wakati ule jengo limeshajengwa zilikuwa zimeshatumika dola milioni 35, sasa hizi zingekuwa *recovered* wapi na tayari zimeshatumika. Kwa hivyo, ingebidi sasa ukaanze tena kutumia dola milioni 35 halafu ndio ujaze hizo nyengine.

Lakini suala jengine ambalo hili katika ripoti hiyo ya *EDPi*, Mhe. Mwakilishi anajaribu kuiacha ni taarifa ya wakati. Mshauri Mwelekezi alisema mkilivunja jengo lile mukataka kujenga jengine, basi muda wake huo wa kulijenga hili basi utachukua tena mwaka mzima zaidi wa kulijenga na imo katika maandishi, pamoja na huo muda wa kulijenga hili, kama hili litachukua miezi 18 basi tukilivunja na kuanza upya basi tutachukua mwaka mmoja na hiyo miezi 18, serikali ikakaa na kwa sababu tumeshaletewa na Mshauri Mwelekezi kwamba kuna uwezekano wa kulitumia jengo lile bila ya kulivunja tukaliendeleza lile lile, na kwa sababu maamuzi yalikwishakupita, tukawa sasa tunabakia na kuchagua katika zile mbili, wala hakuna ubaya Mhe. Mwenyekiti, kuna viwanja duniani viko vya kila aina, lililobadilika sasa hivi ni kwamba mwanzo ndege zilikuwa zikae mbele zote, ndogo 737 na kubwa 777 zikae mbele. Sasa kilichobadilika ni kwamba zile ndogo, hatusemi hivi vichata hapana, zile ndege ndogo zile za *boeing* zitakaa mbele, lakini zile ndege kubwa za 777 zitakuwa ubavuni upande wa kusini ndicho kilichobadilika. Sasa ukienda kwenye hivyo viwanja vya kimataifa ndege utazikuta zinazunguka hasa kila upande ziko, sasa kuna ubaya gani hapo.

Kubwa zaidi ambalo Mhe. Mwakilishi hajaliona na ambalo wizara imeliona. Mhe. Mwenyekiti, niliuliza mimi kulirudisha nyuma jengo lile kwa mita 60 kama ambavyo inapendekezwa. Je ni *row* ngapi za nyumba ambazo zitabidi zivunjwe za Kiembesamaki, hatuna njia nyengine ya kupata kiwanja, isipokuwa tuvunje nyumba ni *row* zisizopungua mbili. Kwa hivyo, kuanzia mwanzo mpaka mwisho nyumba mbili mbili ziende ndio tuweze kupata hicho kiwanja, angalia ni bilioni ngapi hizo hazipo. Hivi sasa tunapigiwa kelele kwamba kuna sehemu ukuta umeshindikana kwa sababu kuna baadhi ya nyumba hazijalipwa.

Kwa hivyo, sisi tumepima Mhe. Mwenyekiti, mambo yote hayo tukaona kama hao wataalamu wa kiulimwengu wanatuambia kwamba jengo lile litatumika. Sasa sisi tukaingia kazini kuichukua hiyo na hatukuichukua ile ya kulivunja kwa sababu hizo. Siku zote Mhe. Mwenyekiti, katika *principle* ya *administration*, kuna kitu kinaitwa *alternative.* Ukitaka kufanya *decision* ni lazima uwe na *alternative one, two and three*, lakini wanasema wataalamu wa *administration*, kwamba hakuna *alternative* iliyokuwa haina *risk* ndani yake, huwezi kuipata hii yote.

Mhe. Mwenyekiti, siku zote huwa natoa mfano mimi, mtu akikupa shilingi milioni 10 akakuambia nenda kawekeze, utaanza kupanga nijenge nyumba niikodishe ina *risk* zake, je utapata mteja. Je, ninunue gari na siku ya pili ikipata ajali, yaani kila kitu kina *risk* yake, lakini baada ya kupanga wewe mwenyewe utachagua. Sasa serikali pamoja na wataalamu tumechagua hiyo na wataalamu hao hao baada ya kuchagua hiyo wanatufanyia kazi mpaka wamemaliza *design* yote, sasa kazi inaendelea.

Sasa sifahamu kwa nini linakuja tena suala la kuwa hatukukubaliana na kuwa lazima livunjwe, wakati sasa jengo limeshaongezwa lilikuwa halina kile kipaa cha mbele, hawa wataalamu ndio wakasema jengo lazima kuwe na *reception*, huu ndio utamaduni wetu, imeshatiwa *frame* yake. Kule mbele upande wa Kusini ile sehemu ambayo itakaa hiyo mikongwe tayari imeshajengwa kwa chuma na kuna sehemu ambayo itakuwa *VIP*.

Kwa hivyo, suala hili namuomba atukubalie kwa sababu ndivyo walivyoamua wataalamu na sisi tukawaunga mkono, nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, katika hali ya kawaida ungenitegemea nadhani na Waheshimiwa Wawakilishi na waheshimiwa wananchi, kwamba turidhike tusonge mbele, lakini Mhe. Mwenyekiti, tunapozungumza mradi wa ujenzi wa jengo jipya la abiria katika uwanjwa wa ndege kwa Zanzibar kwa udogo wake, tunazungumzia mradi mkubwa sana. Kwa msingi wa bajeti yetu ilivyokuwa ndogo kuzungumzia mradi uliokuwa unagharimu dola 128 milioni, ni fedha nyingi sana Mhe. Mwenyekiti.

Tunachokitaka sisi Wawakilishi ni kimoja tu Mhe. Mwenyekiti, kwamba serikali inapofanya maamuzi izingatie *long term interest* na alichosema ni sahihi, lakini tunajenga halafu baada ya miaka mitano au kumi tuje tuseme tunaongeza abiria tukajenge jengine. Kwa kweli kwa nchi masikini kama yetu vipaumbele vinabadilika inakuwa ni kuwabebesha mzigo; hizi ni fedha za mkopo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kusema kwamba Mshauri Mwelekezi ameletwa na amesema Mhe. Waziri kuwa yeye ndio ameshauri. Sasa Mshauri Mwelekezi hatuamulii isipokuwa anatushauri ndio maana anaitwa mshauri, amekuja na *options* zake, lakini mshauri huyo Mhe. Mwenyekiti, amesema kwamba kulibakisha pale kuna gharama za namna mbili; moja ni matumizi ya umeme kutokana na namna lilivyojengwa, yaani kwa kila mwaka kutakuwa na hasara ya dola laki nne na sitini elfu (460,000) ambapo kama ukiliondosha na kulirejesha nyuma gharama hiyo unaiepuka.

Vile vile ukilirejesha nyuma na kuliongezea uwezo anaendelea kusema Mshauri Mwelekezi, kwamba *operational cost* zitakuwa *saved* kwa dola milioni 2. Lakini eneo likiongezeka pia kutafanyika biashara, na kwa wafanya hesabu hawa *ADPI* wanasema itaongeza mapato kwa dola milioni 1,530,000/= kwa mwaka. Kwa hivyo, hiyo gharama ya nyongeza ambayo ingeingiwa mwaka jana tungefanya maamuzi yale Mhe. Mwenyekiti, ndani ya miaka mitano ingeweza kurejeshwa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimalizie hoja yangu, ili nipate maelezo ya mwisho niamue nitafanya nini katika suala hili. Kwa kweli Mhe. Waziri amesema kwamba moja katika hoja alizozizingatia ni muda wa mwaka mmoja, kwamba utaongezeka ikiwa tutaamua kulivunja. Kwanza kusema zimeshatumika dola milioni 35 Mhe. Mwenyekiti hata mimi ambaye si *engineer* ninaona, kwamba kuliweka *frame* lile pale tusidanganyane kama shilingi milioni 35 zimeshatumika.

Kwa hivyo, ninasema tena Mhe. Mwenyekiti, hivi ni vitisho vinavyotolewa na kampuni, ili kunusuru uso wao kutoka na *blunder* waliyoifanya pale, Mhe. Mwenyekiti hizo *cost* zimeelezwa vizuri katika ripoti, lakini naomba nije katika hilo alilolizungumza kwamba hizi gharama walipaswa wabebe kampuni kwa *blunder* waliyoifanya wao na wala tusibebe sisi, na ndio maana kila kwenye mkataba kunakuwa na vifungu vya kutunusuru.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kuhusu muda na ninayo *hansard* yake naomba nisome sentensi moja tu ya mwaka jana, ambayo Mhe. Waziri ananijibu anasema "Katika ripoti ya *ADPI* ukilivunja jengo kuna tofauti ya miezi 12 kamili kuweza kupata jengo jengine na ukilinganisha na kulijenga hili kidogo, hiyo iko sentensi kwenye ripoti ile. Kwa hivyo, sisi tuli-*consider* yote hayo na hatukwenda kwa maamuzi, raghaba wala chochote, lakini kama ingekuwa imefuatwa hiyo *option* ya kuvunja jengo, huo muda aliosema Mhe. Omar Ali Shehe wa Disemba, 2014 ndio tutakabidhiwa, ingekuwa ni Disemba, 2015 ndio tutakabidhiwa kwa ripoti ya Mwekezaji wa *ADPI*".

Sasa Mhe. Mwenyekiti, hili hatukulipata na Disemba kesho kutwa tutalipata jengo na kitabu cha bajeti cha Mhe. Waziri hichi hapa, na leo anatuambia kwamba tutalipata mwisho wa mwaka 2015 si ndio yale yale tumenusuru nini kwa maamuzi yale. Hivi nani anayefaidika katika masuala haya ambayo yanajaribu kufichwa? *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nasema tena kwamba hapa kuna watu ambao wamevuruga, inaweza kuwa ni Mwanasheria wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au Kampuni ya *Beijing Construction* ya China kwa masuala yake wenyewe, na inawezekana kuna watu wamenufaika na wakaweza kufichiwa hapa gharama hizi au hasara hii, ambayo tungeweza kuinusuru kwa muda huu na kumeza machungu na kuongeza kidogo ambacho kimeshafikiwa.

Kwa hivyo, hivi sasa kile ambacho kilichokuwa kinakimbiwa kimeshafikiwa hivi sasa kwa maelezo waliyotupa ndani ya Kamati, yaani tumeshafika milioni 128 ambapo mwaka jana tuliambiwa tutazifika na tayari tumeshazifika na jengo lipo pale pale na tusubiri baada ya muda mfupi tulivunje tena, sasa gharama hii atabeba nani.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumalizia mwaka jana Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, tena ninayo *hansard* yake hapa, nilisema kwamba hawa waliotufikisha hapa hawachukuliwi hatua na akanihakikishia

kuwa tuwape muda serikali na tukija mwaka huu tutapewa maelezo juu ya hatua zilizochukuliwa, na wala hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa. *(Makofi)*

Sasa haya ndio yanayotufanya Wawakilishi wako Mhe. Mwenyekiti tukasema kama humu ndani tunazungumza kuondoshana njiani tu, bajeti ikishapita yote haya yamesahaulika. Naomba maelezo ya kina Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, naona Mhe. Mjumbe ameridhika pamoja na *statements* alizonazo. Sisi tunakubaliana naye kwamba kuna makosa yalifanyika, lakini panapofanyika makosa hufanywa matengenezo na wala hapafanywi tena makosa. Kwa hivyo, sisi tulivyokifanya ni marekebisho ya yale makosa yaliyofanyika.

Lakini mimi binafsi Mhe. Mwenyekiti, nilizungumza na *consultant* mmoja mkubwa ambaye anafanya kazi Dubai na nilimtaka ushauri kwa sababu ni *classmate* wangu nikamtaka ushauri, aliniambia kama *consultant* ametoa *alternative* ya kwamba jengo linaweza likatumika hilo hilo hamna njia nyinyi ya kumwambia avunje, isipokuwa kwa gharama zenu sasa na wala mukimshtaki hamshindi yule *contractor*.

Kwa hiyo, ikazidisha ile hali kwamba sisi sio kama tumemlinda *contractor*, lakini yule *consultant* alipokuja kutoa *alternatives* mbili za kwamba jengo linaweza kutumika hatukuwa na *alternative* nyengine, isipokuwa kuendeleza ule ule mchakato ambao tuliokusudia na wala hatukumlinda *contractor*, kwa sababu *contractor* tunakwenda naye sambamba na *consultant*.

Mhe. Mwenyekiti, hali hiyo inadhihirika wazi hivi sasa kwamba yule *consultant* haondoki tena mpaka jengo likamilike na tumempa kazi mpya ya *supervision*, kwa lengo lile la kazi iendelee. Kutokana na hali hiyo, tunamuomba Mhe. Mwakilishi, Waheshimiwa Wawakilishi wote pamoja na wananchi kwa jumla kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti watuamini, kwamba tunaifanya kwa haki, kwa utaalamu na kwa subira kubwa. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na maelezo mazuri ya Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, naomba kutoa ufafanuzi mdogo kuhusu hatua ambazo serikali imechukua katika kufuatilia makosa yaliyojitokeza katika ujenzi wa uwanja wa ndege.

Mhe. Mwenyekiti, hata mabadiliko ya Katibu Mkuu ambaye yupo ni kutokana na baadhi ya makosa yaliyofanyika uwanja wa ndege, ndio maana tukaona kuna Katibu Mkuu mwengine na baadhi ya Wakurugenzi waliondoshwa katika wizara hiyo kwa msingi wa kurekebisha makosa ambayo yanatokea. Vile vile bado tutaendelea kuchukua hatua kadri tutakavyoona makosa yanajitokeza.

Suala la kuongezeka kwa ujenzi kwa jengo la uwanja wa ndege ukisoma taarifa ya Mhe. Waziri katika kifungu 31 kinaeleza pale, Mhe. Mwenyekiti naomba ninukuu.

Kifungu cha 31 kinaeleza hivi:-

"Kuongezeka kwa ukubwa wa jengo kutoka mita za mraba 17,800 hadi 23,000, kuongezeka eneo la kuegeshea ndege kutoka mita za mraba 23,000 hadi 37,800, kuongezeka kwa urefu wa jengo kwa upande wa kusini kwa mita 36 na upana mita 75 na kuongezeka sehemu ya mbele ya jengo kwa mita 18".

Mhe. Mwenyekiti, haya pia yamesababisha kuongezeka kwa gharama. Kwa hiyo, ninamuomba Mhe. Mjumbe kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, akubaliane na hali ilivyo, na kama kuna tatizo lolote bado tunao uwezo wa kumpeleka *CAG* na kufanya mahesabu, kuona pamoja na kuchunguza na wengine wakaweza kuchunguza kama kuna suala lolote la upotevu wa fedha.

Lakini kimsingi tumefanya hayo, kwa ajili ya kunusuru hali, ili tuwe na kiwanja cha ndege kizuri kiweze kutoa huduma nzuri. Namuomba Mhe. Mwakilishi kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, akubaliane na sisi, ili tufanye jambo hili tuisaidie nchi yetu kwa ajili ya kuimarisha uchumi wetu.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, najua hata nikisimama mara ngapi majibu yatakuwa ndio haya haya, na mwaka jana yalikuwa haya haya na ukawasaidia kupitisha bajeti hii na wengine tukatoka humu ndani.

Kwa hiyo, nadhani si vyema kupoteza muda wa chombo chako Mhe. Mwenyekiti, isipokuwa naomba niseme tu, kwamba haya yanakaa kwenye *records* na ninaomba kuieleza serikali Mhe. Mwenyekiti, ili nikae tuendelee. Nawaomba kama ulivyokuwa mradi huu na amesema Mhe. Asha Bakari Makame watizame huu mradi aliokuwa akituonesha sana Mhe. Waziri wa Uturuki na Pemba. Kwa kweli taarifa nilizonazo ni kwamba yale yale yatakuja tena, yaani haya haya ya Unguja yatakuja tena, kwa sababu hatuko makini tunaokabidhiwa dhamana.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme tena kwa kumalizia kwamba ninaiomba serikali, kuna kifungu nimesema mwaka jana kinaendelea kudharauliwa na serikali, *Public Finance Act* ya mwaka 2005 kifungu cha 23 Mhe. Mwenyekiti, ambacho kinataka kwenye miradi ya maendeleo serikali iwe inatuletea Barazani hapa kwa miradi ambayo imeidhinishwa na Baraza, na miradi ikiletwa ndani ya vitabu hivi ikaombewa ridhaa, maana yake imeidhinishwa na Baraza.

Kwa maana hiyo, inatakiwa serikali itupatie majina ya *contracting parties*, aina ya *services* au bidhaa inayotaka kutolewa pamoja na gharama ambazo zinalipwa kila moja, ili Baraza liidhinishe na hiyo ni sheria ya *Public Finance Act* kifungu cha 23.

Mhe. Mwenyekiti, tumeshasema sana, naomba sasa kwamba sheria hii ifuatwe na hili tukija tukibeba kwa pamoja vichwa vingi humu ndani na ikija kutokezea tutabeba sote lawama, lakini haya yanayofanyika ndio kwa sababu kifungu hichi hakitekelezwi. Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi hii na mimi nitaendelea kuzuia shilingi katika mshahara wa Mhe. Waziri mpaka pale nitakaporidhika na jawabu ya kadhia ambayo tumekuwa tukiisema sana hapa Barazani kuhusu Uwanja wa Ndege wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, sisi kama Baraza la Wawakilishi tumechoka na kunyanyaswa, kusumbuliwa na kudharauliwa na Uongozi wa Mamlaka ya Uwanja wa Ndege. Sasa tumelisema hili karibu bajeti tatu na Mhe. Waziri inaonesha ameshindwa kumsimamia mtendaji wake, na hili sio kudharauliwa Waheshimiwa tu, isipokuwa tulianza kwa Balozi wa Oman gari yake ilizuiliwa uwanja wa ndege mara tatu, mara ya tatu Balozi wa Oman akaamua kuchukua *taxi, Foreign Affairs Zanzibar* wakaamua kwenda kuichukua gari ile, yaani ni kashfa kubwa *VIP* kufanyiwa mambo kama hayo. *(Makofi)*

Kwa kweli wananchi wetu wamekuwa wakinyanyaswa sana, lakini Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wakiwemo Manaibu Mawaziri na hata Mawaziri wenyewe. Kwa hiyo, tumechoka kudhalilishiwa viongozi wetu. *(Makofi)*

Sasa hili jawabu ninalolitaka ni moja tu Mhe. Mwenyekiti, kwamba serikali ikubali sasa kuwa yule aliyepewa dhamana ile imemshinda, na aondolewe apewe mtu mwengine; ambaye atakayeweza kuuletea heshima Uwanja wa Ndege wa Abeid Amana Karume kama lilivyo jina la Muasisi wetu wa Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Lakini Mhe. Mwenyekiti, sio hoja hiyo tu kutokana na kila tunavyosema anazidi kupanda kiburi na matokeo yake hivi sasa ameanza kushiriki katika ufujaji wa fedha za Mamlaka ya Uwanja wa Ndege. Jana nilisema hapa kwamba kuna kashfa kubwa ya ununuzi wa *x-ray machine*, ambazo barua ninazo hapa. Mhe. Mwenyekiti, barua ya tarehe 3 Aprili, 2014 ndiyo iliyotoa mualiko wa kuomba *tender* kwa ajili ya ununuzi wa mashine hizi.

Vile vile, tarehe 2 Aprili, 2014 wale wanaopelekewa kuomba *tender* wameshaleta barua tena anasema hasa "*We thank you for your inquiry and have pleasure in quoting you as* ...". Kwa hiyo, ina maana mualiko wa *tender* umetoka tarehe 3 Aprili, 2014 na aliyepokea *tender* amejibu tarehe 2 Aprili, 2014. Mhe. Mwenyekiti, ina maana hapo ndio ufisadi na tukisikia ufisadi na ndio yale anayozungumza Mhe. Ismail Jussa Ladhu kukiukwa kwa Sheria ya Fedha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ninakusanya ushahidi maana yake Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ameshamwambia Mhe. Ismail Jussa Ladhu apelekwe *auditor* na wala haya hayataki *auditor*, tayari tumeshayafanyia kazi. Kwa mfano, kuna ununuzi wa vitoroli Mhe. Mwenyekiti, Mkurugenzi wa Mamlaka amepewa mamlaka ya

kutumia mpaka shilingi milioni 50 bila ya *tender*. Sasa leo hapa tayari ameshatumia shilingi milioni 120 kwa ajili ya kununua vitoroli pale kwa utaratibu wa ujanja na sheria tumezitunga sisi.

Mhe. Mwenyekiti, kama vile mwezi huu amenunua au ametumia shilingi milioni 40, mwezi ujao pia milioni 40 na mwezi mwengine amenunua au ametumia shilingi milioni 40, alimuradi asivuke ile shilingi milioni 50, yaani milioni 120 ametumia na vitoroli hivi. Ili vionekane vinafanya kazi ndio ule usumbufu unaofanyika pale uwanja wa ndege ukishafika na gari yako, yaani unalazimishwa lazima uende ukapatiwe na vitoroli vya ufisadi, tumechoka! *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho kabisa katika hoja, tumechoka na vikao vya Bodi ya Wakurugenzi vilivyokuwa havina maana. Kwa kweli sheria ya Mamlaka inazungumza mpaka vikao vya bodi kwa mwaka vinatakiwa viwe mara ngapi. Sasa leo Vikao vya Bodi mwezi mara mbili na watu wanakula sambusa, keki, kuku na *perdue*, kuna *arrears* za wafanyakazi wa Mamlaka wanadai zaidi ya miezi minne, tunakwenda wapi.

Mhe. Mwenyekiti, sisi kwa kweli tunayo mengi kama nilivyosema, na jana nilisema kwamba katika hao waliopewa *tender* ya kuleta *x-ray machine* kuna mmoja tayari wameshamtafunia fedha zake wakamrejeshee kabla Kamati Teule haijaundwa. Sasa naomba serikali ikubali kwamba kuna ufisadi umefanyika na kama nilivyosema juzi kama serikali itakataa tutatumia Kanuni ya 120 turudi, ili tuweze kuunda Kamati Teule kwa ajili ya kwenda kuchunguza ufisadi. Na wala sio hayo tu, kuna suala la *parking* na jana nilizungumza, kwamba hivi sasa pale kwa vile *portions* zinazojengwa kama hujatoa chochote pale hupati kitu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa kukusanya hoja zangu zote hizi nidhamu, ufisadi hapa Mkurugenzi amezidi na Mhe. Waziri ameshindwa kumsimamia. Sasa hapa mawili aidha yeye mwenyewe amwambie Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, akamwambie Mhe. Rais kwamba ameshindwa kazi au serikali itwambie kama wanaridhika na matendo yanayofanywa katika Mamlaka ya Uwanja wa Ndege, lakini katika suala la ufisadi sisi hatutakubaliana nalo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kauli nzito sana ambayo itakayorejesha heshima ya Mamlaka ya Uwanja wa Ndege. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, tupate maelezo kuhusiana na hoja hizo tatu. Kwanza ni utaratibu wa utoaji *tender* kwa ajili ya *x-ray machine*, pili ununuzi wa vitoroli na ya tatu ni vikao vya Bodi.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru, kwanza hoja zimekuwa tatu na sijui utaamua vipi, kwa sababu kila Mjumbe anayo hoja moja.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, zijibu. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, ya kwanza naanza na *x-ray machine*. Mhe. Hamza Hassan Juma ambaye ametoa hoja hizi *documents* alizotaja sijui amezipata wapi, lakini tulizonazo sisi ni kwamba tulikuwa na barua ya kutangaza tarehe 28 Machi, 2014 *tender*, na barua ya *quotation* iliyotoka kwenye hiyo kampuni iliandikwa tarehe 2 Aprili, 2014 na iliambatanishwa na barua ambazo zote zilikuwa kwa njia ya *e-mail* yenye kumbukumbu namba *QUOPA0204/1/2014* na hii ndio *quotation*, *invoice* yenye kumbukumbu *SA14/229* na *tender* yenyewe iliandikwa kwenye barua ya *quotation* iliyotajwa.

Mhe. Mwenyekiti, hizi tarehe anazosema yeye Mhe. Mjumbe kidogo zinakanganya, kwa sababu tarehe tulizonazo sisi zimepangana, kwamba Mamlaka walitoa tarehe 28 Machi, 2014 na *quotation* iliandikwa tarehe 2 Aprili, 2014 na ikaletwa tarehe 3 Aprili, 2014 kwa sababu ndio iliyoambatana na barua ya tarehe 3 Aprili, 2014. Kwa hivyo, *sequence* ni nzuri na inakwenda na wala haipingani kwa barua hizi zilizopo hapa na hizo nyengine sijui yeye amezipata wapi, na hilo ni la kwanza.

Jambo la pili ni kuhusiana na ununuzi wa vitoroli. Mhe. Mwenyekiti, vitoroli kwanza ni tofauti vile alivyoeleza yeye, vilianza kununuliwa tokea mwaka 2012 na malipo ya mwisho ndio yamefika tarehe 01 Juni, 2014. Kwa hivyo, sio kwamba kulikuwa na ulaghai au ghilba ya kuona kwamba atatumia zaidi miaka hii tokea 2012 mpaka 2014 ndio inamalizwa kulipa, kwa hivyo vile alivyoelezea Mheshimiwa kwamba labda baada ya mwezi mwezi tu hii haina ukweli, risiti zipo na kila kitu kipo na malipo yao walikuwa wakilipa kwa hiyo kampuni, ilianza tokea 2014 na malipo ya mwisho yalimaliza Juni 1 mwaka 2012 yakamaliza Juni 1 mwaka 2014, sasa hizi *document* alizonazo

yeye ndio hatujui sisi, kwa hivyo labda atakwenda *CAG* kukagua nani atajulikana lakini hapa hatuwezi kupata jibu la moja kwa moja la usahihi hapa, kwa sababu *documents* tulizokuwa nazo sisi na anazosema yeye ni vitu viwili tofauti, sasa nani aliyekuwa mkweli *CAG* aende akatizame hizi.

Mhe. Spika, sisi katika utaratibu wa Kiwizara sidhani badala ya kupitia tu zile hakuna *authority* ya kusema kitu hiki hivi kitu hichi hivi, mdhamini aliyewekwa kukagua mahesbu ya Serikali ni *CAG*, sasa kiti chako kitatoa muongozo kitu gani kifanyike, lakini *documents* anazozitaja yeye na tulizonazo sisi za mamlaka ni vitu viwili tofauti.

Suala la nidhamu mimi niseme kwamba mimi sikushindwa kazi lakini kitu ambacho kilitokea ni kwamba mchakato huu naufanya kwa utaratibu, kwa sababu kuna uongozi na kila linapotokea mimi huwa naingilia kati na tunarekebisha, kwa mfano Mheshimiwa Mwenyekiti tulipata malalamiko kwamba hapa barabarani mbele ya jengo la *Arrival* na *Depature* kwenye lango lile abiria walikuwa hawaruhusiwi kushuka pale na mtu yeyote haruhusiwi kushuka katika gari yake.

Mhe. Spika: Hebu tusikilize majibu halafu kama tena hatukufahamu au hatujaridhika tutamsikiliza mtoa hoja.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Sasa baada ya kufanya majadiliano na ufuatiliaji vibao vile viliondoshwa kwa kuzuia watu wasishuke na vimewekwa vibao vya kuruhusu mtu anaweza kuteremka na kwenda, na kwa sababu pale ndio palipokuwa na chanzo kikubwa cha hiyo udhalilishaji, Mheshimiwa au mtu yeyote anakuja pale kuteremka kwenye gari anaambiwa hapa usiteremke.

Kwa hivyo sisi tukaona badala ya kulishughulikia jambo la mtu kumwambia tulishughulikie kile chanzo chenyewe kwanza tuondoe ule utaratibu wa kwamba pale asishuke abiria asishuke mtu, kwa hivyo hiyo tumeondoa na vibao vile vya kuwa hapana ruhusa ya kushuka abiria vimeondolewa na vimewekwa vyengine kabisa, sasa haya mambo mengine ambayo yanatokea ndio nikasema kwamba tunayashughulikia kwa kadri hali inavyokwenda.

Lakini inawezekana wenzetu nje wanatumia vitambulisho, ukisafiri popote katika viwanja vya ndege ukiulizwa unatoa kitambulisho, kwa hivyo nawaomba sana Waheshimiwa mtu akikuuliza swali mwambie mimi ni fulani na kitambulisho changu hichi hapa sasa umtizame atafanya nini, kwa sababu kile ndio kitakachotoa fursa ya kupata ile huduma inayotakiwa. Ukianza kubishana nae ataona kwamba ni mtu wa kawaida au nini, kwa hivyo inawezekana Mheshimiwa anataka ile *service* lakini hajitambulishi wala haoneshi kitambulisho hapo ndipo tulipofikia, kwa hivyo nawaomba Waheshimiwa waendelee kushirikiana. Na Serikali kama ulivyoieleza imesikia, Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

Mhe. Spika: Kuhusu vikao vya bodi?

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mheshimiwa mimi sina taarifa ya vikao vya bodi vinavyofanywa kila siku au kila mwezi, isipokuwa vipo vikao vya kawaida na vikao vya dharura na moja katika kikao cha dharura ambacho kilifanyika ni baada ya kurudi Dodoma, na nikapata malalamiko mengi sana ya hizi nidhamu zinazovunjwa katika Uwanja wa Ndege, kwamba Waheshimiwa wengi wanavunjiwa nidhamu zao; wanadhalilishwa, kwa hivyo mimi nikataka kikao cha bodi kikutane kwa dharura kulizungumza jambo hili na kuweza kupitisha maamuzi, na hayo maamuzi ya kuondosha vile vibao pale na abiria waendelee kushuka ililetwa na hiyo bodi ambayo imekaa.

Kwa hivyo viko vikao vyengine vya kawaida na vyengine vya dharura, ila kama kuna madai hayo mimi nachukua ahadi kwamba nitafuatilia, lakini katika mashirika mengine ambayo yapo katika Wizara yangu hakuna vikao vya bodi vinavyofanywa nje ya utaratibu.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, unajua leo Serikali ilianza vizuri sana asubuhi Mhe. Naibu Waziri alijibu hoja zetu kitaalamu tena kwa ukweli sana, tena tunamshukuru sana, sitaki kusema sasa bora Naibu Waziri sasa hivi akae mbele Waziri akae nyuma.

Mhe. Waziri wa Fedha hoja zetu alitujibu vizuri sana, Mhe. Mwenyekiti hoja ninazozizungumza ni hoja za wananchi, Mheshimiwa mimi leo nitashangaa gari ya balozi pia akifika pale atoe kitambulisho aseme mimi balozi haijulikani?

Naibu Waziri amekwenda kuwapokea wanamichezo pale mpaka gari ya Mhe. Naibu Waziri haijaandikwa mpaka aseme mimi Naibu Waziri, leo Waziri wa Fedha anayetutafutia fedha hilo jengo analolizungumza Mheshimiwa, basi ina maana watu wake hawajui kusoma Mhe. Waziri kashindwa kazi, naomba kauli ya Serikali. Mkurugenzi wa Mamlaka na haya niliyazungumza haya nilipochangia jana asubuhi, nilisema haya hata Mkurugenzi wa Mamlaka aliidanganya Serikali, alimdanganya Mwanasheria Mkuu ambaye alipewa agizo na Mhe. Rais kwamba Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka achague moja aidha aendeshe kampuni yake ile hanga au awe Mkurugenzi, mpaka leo *negotiation* zote na mambo yote anafanya mwenyewe.

Sasa Mheshimiwa ukichanganya na haya yote ndio yanayompa kibri, ina maana yote anafanya ndiyo yanampa kibri. Mimi nadhani Mheshimiwa mimi naomba kauli ya Serikali kuhusu suala la Mkurugenzi, Mhe. Waziri ameshindwa sitaki anijibu, naomba kauli ya Serikali kuhusu kadhia ya ufisadi, lakini vile vile Mheshimiwa kama Serikali itakataa nitaomba tuahirishe urudi kwenye kiti chako nitumie kanuni niliyoisema ya 102 tuunde Kamati teule ili tukuletee haya, hizo *documents* alizokuwa nazo Mhe. Waziri tutaona kama yeye kapewa mbaya au mbovu na mimi nitaonesha zangu nilizokuwa nazo na vyanzo ninavyo, na yule Mzee waliyemchukulia pesa zake za *x-ray machine* kama nilivyosema naye tutamwita wamlipe pesa zake na mambo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi Mhe. Waziri sitaki kusikiliza kauli yake, ameshindwa kazi, ameshindwa kumdhibiti na kumsimamia Mkurugenzi, nataka kauli ya Serikali.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Sasa hii kutosikiliza kauli hilo ni jambo jengine sasa kwa sababu Waziri bado ndio dhamana ndio tunayemuuliza maswali, sasa kusema kwamba siwezi kusikiliza kauli yake kidogo hapa nadhani sio pazuri, ila sasa Mheshimiwa uliuliza hoja tatu kwa nne na Waziri amejaribu kujibu na akaelezea namna ya tenda ya *x-ray machine*, kaeleza tarehe hapo lakini ameelezea kuhusu suala la ununuzi wa toroli, akaelezea kuhusu vikao vya bodi, sasa ndio nikakwita sasa useme je ile habari ya *floating* ya tenda, ununuzi wa *x- ray machine* kwa mujibu wa maelezo aliyotoa wewe unasemaje ndivyo au kadanganya, bado moja.

Lakini pili kuhusu ununuzi wa toroli kwamba hizi toroli zimekwishanunuliwa ila malipo yalikuwa yanakwenda kwa nilivyofahamu, kama kwa njia ya *installment* kama nilivyofahamu, ile kwamba kuna malipo yameanza moja mbili mpaka malipo ya mwisho. Nimefahamu kwamba malipo yalikuwa yanakwenda kwa *installment* sijui kama ndivyo au sivyo lakini nimefahamu hivyo.

Lakini la tatu kuhusu vikao vya bodi anasema kikao cha bodi ambacho hakijaitishwa kwa mujibu wa taratibu yeye hakumbuki kikao hicho, ila kikao kilichoitwa kimoja kilikuwa kwa ajili ya hivyo vibao vilivyokuwa havitoi ruhusa sehemu fulani kushuka abiria. Sasa ukisema hutaki kusikia lakini ameeleza hivyo, sasa utwambie kama hivyo anavyosema sivyo tufahamishe ili kama kuna hoja nyengine ya kujenga ujenge, lakini kusema sitaki kusikia, hapana, hiyo sio utaratibu, maana kama hutaki kusikia labda utoke nje usisikie lakini vyenginevyo hivyo ndivyo anavyojua yeye.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, unajua ndio pale niliposema Mhe. Waziri katika Wizara hii anatakiwa awe makini sana hoja sikuzitoa sasa hivi, hoja kama sikosei nilizitoa tangu jana leo akanambia kwamba hajui vikao vya bodi, ina maana hata hakukaa na watendaji wake, lakini jengine Mhe. Mwenyekiti...

Mhe. Mwenyekiti: Kuhusu *x-ray machine* unasemaje umeridhika kwa utuo.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Suala la *x-ray machine* sijaridhika kabisa na ndio maana nikaomba Mhe. Mwenyekiti turudi kwenye kiti chako ili sasa tutumie ile kanuni ya kuunda Kamati Teule kwenda kuangalia, kwa kifupi suala la ununuzi wa toroli sijaridhika, suala la ununuzi wa *x-ray machine* sijaridhika, hayo tunataka twende tukayaangalie.

Mhe. Mwenyekiti: Sijui lakini tizama Mhe. Hamza yeye ana *document* inayoelezea utaratibu mzima; tenda matangazo yake na *quotation* na kila kitu, wewe una *document* nyengine sasa labda *document* aliyokuwa nayo yeye useme hiyo siyo hiyo ni feki, nyengine kabisa hiyo uliyonayo ndio sahihi, ukisema hivyo hapa inakuwa hoja ipo.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, mimi ninasema nilizokuwa nazo mimi ndio sahihi, na tukienda kuchunguza baada hata ya hicho kikao alichosema...

Mhe. Mwenyekiti: Hebu mpe alinganishe na za kwake maana...

Mhe. Hamza Hassan Juma: Na hata hicho kikao walichokaa tarehe 28 baadae waliwatuma wajumbe wao wawili wakaenda Afrika ya Kusini. Mheshimiwa kuna mchakato mrefu na mambo mengi, kuna watu walikwenda Afrika ya Kusini kwenda kufuatilia, sasa kwani hawa walioombewa tena ni kampuni moja tu, unajua hapa unapotoa tenda ukaanza kufanya upendeleo mmoja ukamfuata mpaka huko aliko ni sehemu ya ufisadi.

Mheshimiwa tunataka tukachunguze ufisadi kwenye Mamlaka ya Uwanja wa Ndege, kwa sababu sasa hivi Mhe. Mwenyekiti, kutokana na muda huu au labda tuahirishe waende wakatafute vielelezo vyao na mimi nikatafute vielelezo vyangu vya ziada, kwa sababu tukija sasa na vielelezo vya ziada nitataka kujua mpaka ile safari waliyokwenda watendaji wake wawili Afrika ya kusini kwenye hiyo kampuni, na nini walikwenda kukifanya, na walitumia shilingi ngapi, na kwa sababu gani ,kwa sababu tenda imetolewa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, usitake niseme mengi, mimi nafikiri tuachie nafasi rudi kwenye kiti chako kwa heshima na taadhima tutumie kanuni yetu ile niliyoitaja ili tuunde kamati Mheshimiwa twende tukaangalie udhaifu wote kama nilivyosema, kuna mambo mengi tu kule tunapata mengi na kutokana na muda uliotupa hatuwezi kuyazungumza yote, kama nilivyosema mwaka jana waliidanganya mpaka Serikali wameidanganya, na kauli yangu ile niliizungumza, kwa hivyo yote tutakwenda kuyaangalia.

Hanga lile mpaka leo bado analo, nani anali-*manage*, nini anafanya na hayo mambo mengine ya ununuzi wa vitoroli na nini, masuala ya *parking* pia jana pamoja na muda mdogo nilisema mambo mengi sana nilizungumzia suala la *parking* ile, hayo mambo mengine ya *apron* wala sijayataja, ule ujenzi wa vipatisheni kule juu mpaka utoe chochote watasema wale hao waliopewa waliotoa chochote kila mmoja atasema.

Mhe. Mwenyekiti mimi nafikiri hapa tukubali, kwa sababu unajua Serikali ikiwa inajibu majibu ambayo wananchi wanajua kwamba Serikali inadanganywa na inadanganyika na wao wanadanganya hapa ndio tunazidi kuumiza, kwa sababu hizi taarifa tunapewa na wananchi, na hawa wananchi ndio waliofanyiwa hayo mambo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba ukubali tu kwa heshima na taadhima urudi kwenye kiti chako ufanye maamuzi halafu baadae ukishuka Mhe. Makamu wa Pili wa Rais atatwambia kuhusu huyu Mtawala wa Mamlaka ya Uwanja wa Ndege Serikali inamfanya nini, lakini sisi kama Baraza la Wawakilishi tumechoka naye, kuwa kama Mkurugenzi wa Mamlaka hafai!(*Makofi*)

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru tena kwa kunipa nafasi hii. Nilimsikia jana Mhe. Hamza akisema angependa kupata kauli ya Makamu wa Pili wa Rais kuhusu suala hili la Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Uwanja wa ndege, nimezisikia hoja zake ingawa sikuwemo humu ndani lakini nilisikia hoja zake kuanzia mwanzo mpaka mwisho.

Mhe. Mwenyekiti najua namna gani Mhe. Hamza alivyoguswa na suala hili, na ni kweli mara nyingi huwa analizungumza lakini niseme tu Mhe. Mwenyekiti, mimi siwezi kupinga maamuzi ya Baraza, lakini ninachosema ni kwamba sisi Serikali tumesikia hilo na kwa sababu muhusika hayumo humu ndani kujitetea, sisi Serikali tuko tayari kuchukua hatua ya kuchunguza haya na hoja hizi zote; kumwita muhusika na akatupa maelezo.
Na mteule Mhe. Rais nitampelekea salamu hizo ili afanye maamuzi, kama ataunda Tume yeye ya kuchunguza au hizi hoja zote zilizotolewa au anaweza kuchukua hatua za aina gani, lakini hatua yoyote Serikali itachukua, kufanya upelelezi, kuchunguza na kujua hasa ukweli wenyewe, kumwita mwenyewe, kumwita mhusika serikalini akaja akatoa maelezo ili tujue ukweli hasa uko vipi.

Kwa nini anafunga magari kule *Airport*, matoroli haya yamenunuliwa vipi na kama kweli hizo *x-rays* zimenunuliwa kwa taratibu ambazo hazieleweki, haya yote tunaweza kuyachunguza tukapata ukweli wake, na Serikali ikishapata ukweli huu itachukua hatua muafaka kuhusiana na Mkurugenzi huyu.

Kwa hivyo mimi nafikiri niombe Serikali kulichukua Serikalini na kulipeleka kwa Mhe. Rais, tutazungumza na kushauriana na baadae yeye atajua hatua gani ya kuchukua kuhusu masuala haya, lakini kama nilivyosema sioni tabu kama Baraza litaridhia kuundwa Kamati Teule, mimi sioni tabu, lakini nasema bado serikali ina nafasi ya kulishughulikia suala hili. Sasa na Mhe. Rais kutoa ridhaa yake kwa namna gani haya yote yaliyotajwa haya, namna gani yapunguzwe pamoja na yeye mwenyewe kuitwa serikalini kuja kutoa maelezo. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza nimshukuru sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa kutuelewa kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, na namshukuru kwa mambo mawili; kwanza kwa kukubali tuunde Kamati Teule, lakini la pili namshukuru kwamba amekubali maamuzi ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi au ya Baraza la Wawakilishi ya kumkataa Mkurugenzi wa Mamlaka. Sasa naamini kwa sababu yeye kama nilivyosema Mhe. Mwenyekiti kwanza subiri, kwa sababu ninajua yeye si mwamuzi wa mwisho.

Mhe Mwenyekiti: Mhe. Hamza ngoja, hebu ngoja kidogo Mheshimiwa. Umeanza vizuri sana kwamba unamshukuru Mhe. Makamu wa Pili wa Rais lakini haya maneno mengine mimi ninafikiri si vyema ukamlisha, usimlishe maneno ambayo hakusema kwa kweli. Yeye amesema haoni tabu kuundwa Kamati Teule lakini serikali inaweza kuyafuatilia yote hayo, ndio neno alilosema pale.

Lakini la pili, atapeleka salamu kwa aliyemteua huyo, mimi ndivyo nilivyosikia hapa. Sasa ukisema kwamba amekubali amemkataa, hapana. Unajua maneno mengine yanakuwa mazuri sana ukiyasema amekataa kabisa.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Ninakuomba radhi sana rafiki yangu sahibu wangu Mhe. Makamu wa Pili wa Rais pengine labda nimetumia lugha kali sana, lakini kama nilivyosema kwamba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ninajua una majukumu mengi na serikali ina majukumu mengi. Sasa mimi naomba kama ulivyosema huoni tabu kama Baraza litaunda Kamati Teule, kwa hivyo mimi nakuomba utustahmilie hivyo hivyo kwa sababu na wewe pia ni sehemu ya Baraza la Wawakilishi. Basi hilo kama huoni tabu basi na sisi hatuoni tabu kuunda hiyo Kamati.

Kwa hivyo hilo moja nitakuomba Mheshimiwa urudi katika kiti chako ili tutumie hii Kanuni ya 102 nilivyoitaja kama nilivyosema, lakini hili la pili ninaamini na juzi Mhe. Rais alitoa *speech* nzuri sana kwamba kumbe anatusikiliza nini tunachokizungumza. Na alisema Mawaziri tunaomba sana sikilizeni hoja za Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na mzifanyie kazi, kwa sababu maneno yale sio yao ni maneno ya wananchi, na wananchi walifurahi sana walivyosikia kauli ya Mhe. Rais.

Kwa hivyo ninaamini na hili Mhe. Makamu wa Pili akimpelekea salamu zetu kama sisi tumechoka na yule mtendaji pale, na kama tulivyosema ziko nafasi nyengine ambayo mimi nilishauri tu anaweza kufanya kazi vizuri sana, yako maeneo mengine niliyataja jana Balozi alikuwa hayupo kama Baraza la Manispaa. Bustani ameboresha vizuri, gari kama ina-*park* sehemu sio anaifunga, kwa hivyo daladala kidogo zitaweza kufanya kazi vizuri katika Baraza la Manispaa.

Sasa Mheshimiwa kwa kuokoa muda, kwa hivyo mimi nilikuwa naomba nikae kitako ili tukuruhusu kwa kutumia kanuni zetu urudi tena pale kwenye kiti chako tufanye yale maamuzi sahihi kabisa, baadae tuendelee ili tuje tuipitishe hii bajeti.

Ninakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Kabla ya Mwenyekiti hajarudi kitini kwake kama Spika, mimi nilitaka nipate ufafanuzi mmoja kwa sababu tukishaamua kuunda Kamati Teule mtanidai *terms of reference*, lakini nataka nifuatilie kwa karibu sana maelezo ambayo alisema Waziri wa Fedha sasa hivi hayupo, kuhusiana na suala la *tendering* ya hizi *x-ray machines.* Na alifika pahala akasema kama kuna jambo halikufuata utaratibu maana nadhani hazijanunuliwa hizi au zishanunuliwa, Waziri mshanunua *x-ray machine?*

Kwa sababu nilivyomsikia kwamba fedha ambazo Kampuni ya ZAT imelipa ndio ambazo zitatumika kununua *x-ray machine* kama ninakumbuka sawa sawa maana hujaribu kusikiliza kwa makini sana, milioni mia nane na sabini (870). Milioni mia nne na hamsini na milioni mia nne na ishirini ndio kasema yeye hizo ndio anategemea zinunuliwe *x-ray machine* Waziri wa Fedha. Hiyo mimi imenimaanisha kwamba bado *x-ray machine* hazijanunuliwa. Waziri umeshanunua *x-ray machine?*

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mkataba ndio umo njiani hazijanunuliwa bado tumo katika *process* ya mkataba. Hizo zilizokuja ni badili ya kwamba hiyo Kampuni ili kuokoa hali ilivyo. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii labda niseme kidogo kuhusiana na suala zima linaloulizwa la manunuzi ya *x-ray*. Ni kama maelezo ya awali aliyotoa Mhe. Waziri kwamba kwa kipindi kirefu Uwanja wa Ndege wa Kimataifa huwa tuna tatizo la *x-ray*, na hali hiyo

inatokana na uchakavu wa mashine zetu zilizokuwepo pale. Na ni kweli kwamba *life span* ya mashine zile ilikuwa imekufa.

Jitihada za Mamlaka ilikuwa ni kuzitengeneza kuweza kufanya kazi, hilo halikufanikiwa. Na kama utakumbuka Mhe. Mwenyekiti, sisi wenyewe Wawakilishi hapa tulikuwa mashahidi wa kupiga kelele kwamba hadhi ya uwanja wetu haitopendeza kuona ukaguzi wa bidhaa mikoba na wasafiri ufanyike kwa njia ya mikono na kupapasa hasa mikoba ambayo inabeba vitu mbali mbali.

Na kwa kuzingatia kwamba tulikuwa tunakwenda katika *high season* ya utalii ndio mamlaka ikatengeneza utaratibu na kutafuta *x-ray machine*. Katika utaratibu huo walijitokeza watu wawili lakini sote tunatambua sheria ya manunuzi kwamba ukitaka kufanya tenda hesabu ianzie watano ndio mamlaka ikaamua kwenda kwenye *single source* Kampuni ya South Afrika wakatoa *invitation letter* tarehe 28, *quotation* na majibu yake *invoice* yakajibiwa tarehe 2, barua ya majibu ikafika Mamlaka tarehe 3.

Sasa hapa nimelisikia limesemwa kwamba kuna mtu ametoa rushwa hakupewa hiyo *tender*. Mimi ninafikiri sheria ya rushwa iko wazi kwamba anayetoa na anayepokea wote wamefanya kosa la jinai. Sasa mimi nadhani itakuwa jambo la busara kama kuna ambaye ametoa rushwa hakupata hiyo tenda nadhani wataisaidia serikali kumkamata atamtaja aliyempa ili haki itendeke mbele ya sheria. Kwa sababu huo ndio utawala bora. Lakini kwa nini Mamlaka ikaenda kwenye *single source*. Mamlaka ilikwenda kwenye *single source* kutokana na mahitaji ya *x-ray machine* kwa hadhi ya uwanja wetu, uwanja wetu una mapungufu mengi, tuna mapungufu ya *x-ray*, tuna mapungufu ya *fire*.

Leo hii wakija wakaguzi wowote wataokuja kuangalia uwanja ule kwenye huduma za *fire* uwanja wetu unafeli. Kwanza utafungwa, uwanja utashushwa *grade* na uwanja ule hautosomeka tena kama *international*. Mahitaji haya ndio yaliyopelekea kwamba mamlaka waende *single source*, na nini faida ya kwenda *single source*.

Faida ya kwenda kwenye *single source* kwa maana kwamba kama tungempa mtu mwengine ambaye hana kiwanda cha uzalishaji wa mashine hizo maana yake yeye angeenda kwenye soko kwenda kununua, muda huu wa miezi miwili tusingepata mashine. Mtu huyu tuliyekwenda kwenye *single source* ana uwezo wa kuwa nazo hizo mashine za kuzalisha na anazofanyia biashara, na ndio maana kwa sababu tume-*tender,* yeye amekubali muda wa kuzalisha atatuazima za kwake ili tuweze kupata huduma tunayoitaraji. Ndio maana mashine 3 ziliopo pale tumeazimwa ili kupisha kipindi cha kukamilisha mashine ambazo zimekusudiwa kununuliwa.

Sasa hapa suala lilikuwa moja utaratibu wa manunuzi ya *x-ray* tumefuata utaratibu haukufuata utaratibu? Kwa mujibu wa takwimu *document* na hati tulizonazo sisi tumeridhika kwamba utaratibu umefuatwa.

Hoja ya pili kwamba je, huu utaratibu unaosemwa ndio au sio hatuoni tatizo kwenda kuchunguza. Lakini sisi kama Wizara tumeridhika kwa mujibu wa *quotation*, kwa mujibu wa *document* tuliokuwa nazo kwamba utaratibu umekamilika kwa mfumo wa *single source*. Sasa kama kuna hofu na haja kwenda kuchunguza sisi hatupingi lakini mfumo uliotumika lazima ueleweke.

Mfumo uliotumika ni *single source* haikuwa tenda ya kubishania watu wawili, haikuwa tenda ya kubishania watu watatu. Kwa hivyo tunapokwenda kuchunguza tukijua tunachokichunguza ni kitu kipya, tunakwenda kuchunguza utaratibu wa manunuzi kwa *single source* ndio utaratibu uliotumika. Na kwa mujibu wa sheria ya manunuzi utaratibu huo unakubalika kwa sheria yetu.

Sasa kama sheria zetu tunazotunga tunachukua nafasi ya kuzipinga huo utakuwa uamuzi mwengine. Na ningetarajia chombo kikubwa kama hiki, chenye kuheshimika, chenye watu wanaotambua mambo, tutumie nafasi hiyo kutumia madaraka yetu vibaya kwa kuwakandamiza watu wanaosimamia sheria tunazozipitisha.

Mimi nisingeona wala nisingefurahi kuona chombo hiki tunapitisha sheria, tunazisimamia lakini kwa malengo ya kukandamiza watu wanaokwenda kuzitekeleza. Utaratibu wa manunuzi uko wazi, unakwenda kwenye tenda watu watatu, wanne, watano, wana-*compete* ukiwa na mazingira maalum unaruhusiwa kwenda kwenye *single source*. Sasa kama hoja ni kosa kwenda kwenye *single source it's okay,* tuchukue utaratibu twende tukapate uchunguzi. Kama utaratibu wa kwenda kwenye *single source* uko *clear* hatuna sababu ya kufanya hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe mmeona faida ya kutoa maelezo yakafahamika, na kwa sababu tatizo nililonalo mimi kutengeneza Kamati Teule wakati hatujafahamiana. Maelezo aliyotoa Mhe. Naibu Waziri anasema kwamba taratibu zimefuatwa. Ila kwa sababu ya dharura imebidi kutafuta mtu mmoja ambaye bahati nzuri anavyosema kwamba yeye huyu ni mzalishaji wa hivyo vifaa vyenyewe. Sasa kama hali hiyo tunahisi bado inatu-*warrant* tuweke Kamati Teule.

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nirudie yale niliyosema kwamba serikali haijashindwa kuzishughulikia hoja hizi. Serikali ina uwezo wa kushughulikia, kwa sababu lazima na muhusika na yeye apewe haki ya kujieleza.

Sisi ndio tunaozungumza humu ndani lakini yeye atapata nafasi ipi sasa ya kujieleza kusema haya yamekuwa hivi. Ndio nikasema serikali italishughulikia kwa kumwita muhusika atueleze haya yote anayofanya ameyafanya kwa misingi gani na kwa nini pamoja na haya yote yaliyoelezwa kuhusu ununuzi wa *x-ray* na kadhalika. Ingawa ninamshukuru Mhe. Gavu kwa maelezo aliyoyatoa kuhusiana na suala la ununuzi wa *single source*, hili linakubalika kisheria.

Sisi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais tulipokuwa tunatafuta vifaa kwa ajili ya sherehe za Mapinduzi ya miaka 50 tulitoa tenda kwa vifaa tulivyovitaka. Bei tulizoletewa pale zilikuwa kubwa mno tukaomba kibali kwa Rais tutumie *single source* tukamtuma mtu kwenda China kutafuta vile vifaa. Bei tulionunulia vifaa vile tume-*save over one billion shillings*. Sasa kama *single source* imetumika, kisheria inakubalika lakini hata hivyo niseme tu Mhe. Mwenyekiti kwamba bado nasema kwa serikali bado ina uwezo wa kulishughulikia suala hili, Mhe. Rais mwenyewe ana uwezo wa kufanya maamuzi yale yote ambayo yatagundulika.

Kwa hivyo bado Mhe. Mwenyekiti ninafikiri kwamba suala hili liachiwe serikali, mimi nitalichukua kwa Mhe. Rais na Rais atafanya maamuzi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hamza sasa tunataka tuendelee utwambie baada ya kauli hii na ufafanuzi mzuri sana uliotoka kwa Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mhe. Makamu Pili wa Rais, lakini nataka nimuambie Mhe. Naibu Waziri sifa nilizompa asubuhi sasa hivi ninazifuta zote.

Sisi ni Wawakilishi makini tunafanya kazi kwa utafiti, sheria ya *single source* tunaijua Mheshimiwa *haraka haraka haina baraka*. Tumeshaona dalili za mchezo mchafu, Mheshimiwa tumeshaeleza mengi; suala la kumwita Mkurugenzi Mheshimiwa keshaitwa mara ngapi? Nimeeleza mwaka jana nilipozungumza kuhusu suala la hanga si aliitwa kaidanganya serikali na mimi nilikuja na *document*, yeye kule serikalini kaitwa mfano nachukuliwa tarehe 10, tarehe 15 kasaini *document* kupitia Kampuni hiyo hiyo.

Kwa hivyo huyu kwanza yeye mwenyewe unajua kuna mambo mengine ya kienyeji sitaki kuyasema, kwanza anasema haogopi mtu, hajali mtu. Sasa mimi nadhani hiyo kuwa haogopi atajuana yeye mwenyewe lakini mimi naomba Mheshimiwa, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kazungumza vizuri sana, wao walipoitisha tenda bei iliyokuja ni kubwa sana, huku hakujaitishwa hicho kitu.

Kwa hivyo mimi nadhani Mheshimiwa ninamuheshimu sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, na siku zote tulikuwa tunamwambia Mhe. Waziri wa Fedha, Fedha serikali hii zipo zinapotea, fedha za wananchi zinapotea. Mhe. Waziri wa Fedha alitwambia Waheshimiwa Wawakilishi nionesheni mianya ya fedha inayopotea, ndio mianya yenyewe ndio tunaionesha wenyewe sasa hivi. Mheshimiwa unajua nimezungumza mengi tatizo hukunisikia ile jana.

Sasa mimi nadhani hadidu rejea wala usipate tabu, *hansard* niliyozungumza jana ipo, Katibu wetu ataichambua tuna kitengo cha utafiti watachambua, *hansards* za Waheshimiwa mbali mbali waliozungumza kuhusu kadhia za mamlaka ya uwanja wa ndege hizo ndio zitakazokuwa hadidu rejea katika Kamati Teule.
Mimi ninadhani serikali wana utaratibu wao wache waendelee lakini na sisi kama Baraza la Wakilishi tunaomba haki yetu tuipate kwa mujibu wa kanuni uliozisimamia wewe Mhe. Mwenyekiti tuunde Kamati Teule. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti kwa heshima kubwa nakuomba urudi kwenye kiti chako ili sasa tupitishe yale maamuzi ya kuunda Kamati Teule.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti baada ya maelezo mazuri sana ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais sidhani ndugu yangu, rafiki yangu Mhe. Hamza ataelewa jitihada za Serikali katika kulishughulikia tatizo.

Mhe. Makamu wa Pili alieleza kuwa bado serikali ina uwezo wa kulishughulikia jambo hili, na akaeleza hatua mbali mbali ambazo anadhani tungezifanya kwa kushauriana na Mhe. Rais ili kulipatia ufumbuzi tatizo hili, nadhani ingekuwa vizuri sana. Kwanza tukampa heshima yake Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa ahadi ambayo ametoa.

Lakini la pili anaposema hivyo Mheshimiwa maana yake ana nini? Viko vyombo Mheshimiwa vya kufanya uchunguzi za kiserikali. Tunayo TAKUKURU, tunayo Ofisi ya *CAG* na vyombo vyengine ambavyo haya yote aliyosema Mhe. Hamza na maelezo yaliyotolewa na upande wa Wizara yangechukuliwa kama ni ithibati ya mwanzo ukafanywa huu uchunguzi, baada ya uchunguzi na wahusika kuitwa kama alivyosema Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ingetusaidia sana.

Sasa kuwa na hoja ya kuendelea kama tungeona sasa baada ya maelezo hayo na hatua hizi tutakapoleta ile taarifa itakapoonekana kwamba yale yaliyofanyika sasa yanahitaji kuunda kamati Teule tunaweza kufanya hivyo, lakini bado Mhe. Makamu wa Pili wa Rais; Kiongozi wetu Mkuu wa Shughuli za Serikali kanyanyuka mara nyingi kuwaomba Wawakilishi wenzangu walielewe hili, na mimi naona hizo hatua za serikali zitakuwa za karibu zaidi kufanyika na tukapata matokeo kuliko matokeo ya kuunda Kamati Teule hasa ukitizama Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi hapo mbele yetu tuna Ramadhani, tuna Bunge la Katiba tunakwenda tena, kadhalika na kadhalika.

Kwa hivyo mimi nilikuwa ninaomba tuyatazame haya yote ili tuyafanye maamuzi ambayo yatatusaidia kama ambavyo Waheshimiwa Wawakilishi wameonesha. Kwa hivyo nimuombe sana rafiki yangu Mhe. Hamza umeshaeleza vya kutosha, sasa tumkubalie maelezo ya Mhe. Makamu wa Pili ili tuendelee na hotuba yetu hii tuweze kwenda vifungu vyengine, na mimi naamini haya maelekezo ambayo Mheshimiwa ameyatoa basi yatafanyiwa kazi vizuri. Naomba kusema hivyo Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kunipa kuongezea maelezo ya ziada, kwanza nataka nimshukuru sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa maelezo yake na kikawaida tusingepaswa na sisi kusimama baada ya kutoka kauli ya kiongozi wetu. Na vile vile nataka nimshukuru sana Mhe. Issa Haji Ussi Gavu; Naibu Waziri kwa kutoa ufafanuzi wa jinsi ya kadhia hii ilivyojitokeza.

Mimi nataka nitilie nyama yale aliyosema Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwamba serikali inapotoa *commitment* kwamba inalichukua na kulifanyia kazi kuna vyombo, na Mhe. Hamza hapa amesema mambo mengi sana ya pande mbili hasa yanayohusiana na suala la kuwepo kwa dalili ya rushwa. Na ameeleza kwamba kuna mtu ambaye amepewa pesa kwa tegemeo pengine la kutaka kupata *tender*.

Sasa kuna chombo tumekiunda ni vizuri Mhe. Mwakilishi aliyeleta pia ataweza kukisaidia hicho chombo kumueleza pia huyo ambaye ametoa pesa kwa ajili ya kupata *tender* ili chombo kinachohusika kisheria nacho kiweze kupata nafasi yake.

Sasa mimi nataka nikubaliane na wenzangu wote waliozungumza upande wa serikali, nimuombe Mhe. Hamza yeye ana taarifa nyingi ambazo amezieleza na wizara ina taarifa nyingi, taarifa hizi zote zikipatikana zitaisaidia serikali kupata ushahidi wa kuweza kulifanyia kazi vizuri hili jambo.

Mtumishi ambaye amemtaja ni mtumishi anayetawaliwa na sheria ya Utumishi wa Umma, kama alivyosema Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kuna taratibu lazima zifuatwe ili kuweza kumchukulia hatua. Sasa mimi nadhani nimuombe na mimi rafiki yangu aliwahi kunita mwalimu wake, hivyo ni mwanafunzi wangu, kwa jambo hili namuomba sana Mhe. Hamza akubaliane na sisi; amkubalie Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Jana alisema kwa sauti kubwa sana, kwamba lazima asikie kauli ya Makamu wa Pili wa Rais na Makamu wa Pili ameshasema na huyu ndiye kiongozi wa shughuli za serikali hapa Barazani.

Hivyo tumuombe akubaliane na mawazo ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, na kauli ya Makamu wa Pili ya Rais atuachie serikali tulifanyie kazi hili, taarifa alizonazo yeye zitatusaidia sisi kama serikali kuweza kulifanyia kazi hili jambo kwa uzuri na kwa upana zaidi. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hamza nadhani sasa tumalize hili jambo, najua tukizungumzia mama yangu pale Mhe. Asha Bakari alipomuomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais atoe neno na akatoa neno kasema karidhika.

Mhe. Mahamoud pale wala sikumsimamisha Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Mahmoud Thabit Kombo ndiye aliyetoa hoja, Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa hajatoa hoja yoyote, alipotoa hoja nikamwambia kwa sasa kwa mazingira tuliyonayo hatuwezi tukapata jibu amesema anakuheshimu.

Mhe. Hamza umemuomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ameshasimama mara mbili, na mimi naendelea kutaka ufafanuzi wa mambo mengi sana yakatoka yaliyotoka kutoka kwa Mhe. Naibu wa Waziri ambaye kwa kweli hatukuwa tumeyaelewa, baada ya kusema tumeelewa. Mheshimiwa hebu tumia busara zako kama walivyotumia busara wengine tumalize hili jambo, najua hii ni *experience* ya mara ya kwanza kabisa kuwa anasema sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, lakini leo amesema na nimemuona akisema na akizungumzia kusimamia, hebu tusikie kauli yako.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa sana kama walivyoomba Waheshimiwa wenzangu wawili na wakamkubalia Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, sasa wao unajua mambo haya *give and take;* wawili wame-*give* mimi naomba ni-*take*. Na hili Mhe. Mwenyekiti, kwa kumsaidia Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, unajua tatizo sheria zetu zinasemaje, unapokuwa huridhiki na utendaji wa wizara mimi natakiwa nijazishe Wajumbe fomu kumpigia kura ya kutokuwa na imani Makamu wa Pili wa Rais. Sitaki kuja kumfikisha Mhe. Makamu wa Pili wa Rais huko, kwa sababu bado sijaridhika na utendaji na hizi kauli zinazozungumzwa ndiyo maana nikasema tukienda tutapata kupima yote mawili.

Mimi namshukuru sana Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi kwa kulipa nguvu kubwa sana Bunge la Jamhuri ya Muungano, kwa kuweza kuwasamehe Mawaziri wake wapendwa wanne kutokana na Kamati Teule ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

TAKUKURU ipo Tanzania Bara, Mamlaka ya Rushwa ipo; hizo mamlaka zote zilizokuwepo hapa Zanzibar Mheshimiwa zipo. Kwa hiyo, sitofanya makosa kwa kutaka kuunda Kamati Teule wakati Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano ameliruhusu Bunge kuunda Kamati Teule na akafanya maamuzi mazito tena kwa watu wazito. Hapa tunafanya maamuzi, unajua hapa kuna hoja mbili; ile hoja ya mwanzo Mhe. Makamu wa Pili wa Rais nimeshakubali ataichukua atampelekea muhusika.

Namshukuru sana mwalimu wangu na bado naomba uendelee kunielimisha kwa kushirikiana na Waziri wa Utumishi wa Umma watamshughulikia wao wenyewe mtu wao, lakini huku kwenye fedha za umma huku sasa tuacheni Mheshimiwa, ile moja namuachia Mhe. Makamu wa Pili wa Rais akakae na Rais kwa sababu ile ni nafasi ya uteuzi, lakini huku katika mambo ya usimamizi wa hizi fedha za umma na matumizi sheria tulizozitunga sisi, Mheshimiwa naomba *give and take;* hii moja Mhe. Makamu wa Pili wa Rais namuheshimu nampa akashauriane na Mhe. Rais, lakini hii moja ya kuunda Kamati Teule tupe nafasi, na Mheshimiwa tutakuja na mengi sana nyinyi wenyewe mtakuja kushangaa. Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo sasa naomba urudi kwenye kiti chako ili sasa tuweze kupitisha maamuzi ya kuunda Kamati Teule. Nakushukuru.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa tunafanyaje kwa sababu kuna hoja nyengine ziko mbele huku napata hofu tusije tukahitaji Kamati Teule mbili, tatu…

Mhe. Hamza Hassan Juma: Naamini katika mtu aliyeanza kutoa *alert* kwamba kama sijaridhika nitaomba tuunde Kamati Teule nilikuwa ni mimi. Mhe. Jussa hoja yake yeye tayari ameiachia serikali na anaifuatilia, na alituomba kufuatilia na aliwasema kwamba sasa yale maneno ya mwaka huu yawe ndiyo ya mwisho yabakie utekelezaji.

Sasa mimi nadhani hayo mengine tutapiga buti, tutafanya nini, tutarekebisha ili mimi naamini huko mbele ukisharuhusu hili, huko mbele Mheshimiwa mjadala utakwenda haraka sana na tutamaliza kabla ya muda ambao unautegemea wewe. Kwa hiyo, nakuomba Mhe. Mwenyekiti, urudi kwenye kiti chako ili tuweze kufanya maamuzi halafu baadae tuje tuendelee na vifungu. Nakushukuru sana Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, naona ulitoa ushauri mzuri sana na wala ushauri wako ulikuwa hauathiri haya maelezo ya Mhe. Hamza, kwa sababu kama ulivyosema bado hatujamaliza kupitia mafungu, ni vyema tukaendelea kupitia mafungu tukishamaliza kupitia mafungu basi itakuwa hili jambo tumeliweka kando na tunaweza kulirudia tukashauriana kwa utaratibu huo utakaofuata baadae. Lakini kama ulivyosema unaweza ukaahirisha ukarudi kwenye kiti chako halafu likatokea jengine ukarudi tena kwenye kiti chako, ulitoa uamuzi na ushauri wa busara sana.

Kwa hivyo, naomba tukubaliane na ule ushauri uliotoa mpaka hapo mbele tutarudia kulizungumzia tena hili, tuliweke kando tuendelee na haya mengine ili tuweze kupitisha mafungu. Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa ushauri wangu huo.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe hebu tuendelee na sehemu iliyobaki ili hatimaye tuje tuliamue hili mwisho, wakati huo huo nafikiria sana kwamba bado Mhe. Hamza anazingatia juu ya jambo hili. Wakati tunaendelea najua Mhe. Hamza atazingatia juu ya jambo hili, tusilipitishe hili tuendelee jengine kwanza, halafu hilo litafuatia. Kwa hivyo, tuendelee na sehemu inayofuata.

Kifungu 0401 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti 200,585,000

Mhe. Mwenyekiti: Tunachokifanya sasa kwa vyovyote itakavyokuwa maana kifungu hiki tunawauliza Wajumbe kukipitisha au laa? Lakini hatimaye tutakuja kwenye hii hoja ya Mhe. Hamza ya kutengeneza Kamati Teule ambayo imani yangu ni kwamba anaendelea kuzingatia, tukirudi pale tuamue hilo kwanza la Kamati Teule halafu tena tuamue kwa ujumla wake mafungu yote. Imefahamika eeh? Sijafahamika eeh.

Ni hivi, Waheshimiwa Wajumbe kifungu hiki maana hata ikiundwa Kamati Teule labda kama tutasema hii hatuipitishi, hii Mipango na Sera hatuipitishi mpaka Kamati Teule imalize ambayo nadhani siyo hivyo. Vilivyo ni kwamba Kamati Teule inaweza kuundwa kwa kadri nitakavyoona inafaa, lakini kifungu hiki hatimaye kipite ile kazi ifanyike.

Ninachosema sasa ni kwamba acha tupitishe kabla ya kuuliza kwa ujumla tutauliza hoja hii ya Mhe. Hamza ya kuunda Kamati Teule, halafu baada ya hapo kwa kadiri mtakavyoamua, mtaamua hiyo na halafu mafungu yote kwa ujumla. Tumefahamiana, Mhe. Hamza umenifahamu? Usiwe mnyonge!

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nimekubali kupitisha kifungu hiki pamoja na makubaliano ya upigaji wa kura, kwa hiyo ili iingie katika *hansard*…

Mhe. Mwenyekiti: Si ndivyo nilivyosema.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Ndivyo ulivyosema eeh, kama ndiyo ulivyosema basi sawa nakushukuru.

Mhe. Mwenyekiti: Tutakwenda hapo tutauliza juu ya suala la Kamati Teule kabla hatujapitisha ile hoja ya mwisho ambayo Mhe. Waziri kwa kawaida huwa anaomba kwamba sasa kwa kuwa mafungu yote yamepitiwa bila ya mabadiliko naomba sasa yakubaliwe, kabla ya hiyo umenifahamu?

Mhe. Hamza Hassan Juma: Nimekufahamu.

Mhe. Mwenyekiti: Lakini angalizo langu ni kwamba unaendelea kuzingatia kuhusu hoja zilizotolewa hapa, maelezo ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais mpaka tukifika pale itakuwa ushazingatia vya kutosha.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Nimekusikia Mheshimiwa, nimekusikia!

Mhe. Mwenyekiti: Haya.

Mhe Mahmoud Thabit Kombo: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nakupongeza kwa muongozo wako ulioutoa, lakini naomba ninukuu kifungu 158 na naomba nikisome halafu nitatoa haya maelezo yangu.

"Iwapo jambo au shughuli yoyote haikuwekewa masharti katika kanuni hizi, Spika ambapo sasa hivi wewe ni Mwenyekiti, Spika ataamua desturi na utaratibu wa kufuatwa katika jambo au shughuli hiyo na uamuzi huo pia utazingatiwa katika kitabu cha maamuzi ili kuongoza mwenendo wa baadae".

Sasa naomba niulize tu Mhe. Mwenyekiti, kwamba huu ndiyo utakuwa ndiyo mwenendo wetu ambao tutakwenda nao baadae kutokana na kanuni hii (*future norms*). Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Itakapotokea haja hiyo tunaweza tukatumia utaratibu huu, kama kutatokea hoja ya aina kama hiyo, tumefahamiana.

Kifungu 0401 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti 200,585,000

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Asha hebu kaa kidogo, unajua Mhe. Jaku pale alitaka kutoa hoja kwamba tuwe na hoja ngapi, tano. Tulia Mhe. Waziri mimi sikutaka ile tuiwekee utaratibu kwa sababu kuna baadhi ya hoja zinatokeza mbili, tatu kwa pamoja.

Kama Mhe. Hamza ukizizingatia kulikuwa na hoja kama nne kwa pamoja; nidhamu, vikao vya bodi, tenda ile ya *x-ray machine* na ununuzi wa matoroli, hizo ni nne na huko nyuma zilikuwepo nyengine.

Kwa hiyo, hata ile hoja ya Mhe. Jaku, ya kufanya ziwe tano tulikuwa na ngapi kabla? Tulikuwa na saba. Ila kama unataka kutoa taarifa tu Mheshimiwa basi nakuruhusu toa taarifa.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, nitakuja kugonga huko mbele, maana hili fungu halina chochote nimetizama lakini nitakuja kwenye fungu 901.

Kifungu 0401 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti 200,585,000

Kifungu 0701 Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Ismail Jussa Ladhu kaa kwanza maana nishakuwa na watu wengi sana, naanza na Mhe. Mohammedraza Hassanali baadae Mhe. Asha Bakari Makame na Mhe. Mgeni Hassan Juma.

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: Mhe. Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mhe. Waziri wa Fedha na kuiweka *hansard* sawa kwa maelezo yake mazuri jambo ambalo lilikuwa limenigusa mimi na kampuni yangu. Namshukuru kwa ufafanuzi mzuri na kutoa taaluma kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, utakumbuka kwamba nilikuwa nina makubaliano kati ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa maana ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwakilishi wa Jimbo la Uzini kupitia wananchi wangu. Tulipofika mwaka jana hapa nilikuwa ninaulizia zile barabara zangu na Mhe. Waziri kwa kuwa ninazo *hansard* zote alieleza kwamba alikuwa na upungufu wa shilingi milioni 16 ili mashine hii ikatengenezwe.

Mhe. Mwenyekiti, kumbukumbu kwa kuwa zipo kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Uzini na kuona matatizo haya ya barabara zao pamoja na kuona kuwa kunafanyika vifo visivyokuwa na hatia, Mwenyezi Mungu awasaidie kinamama na dada zangu nilikubali.

Kwa bahati nzuri Mhe. Waziri wa Fedha *hansard* yake ninayo kunambia kwamba Mhe. Mwakilishi tunakuomba upitishe bajeti hiyo pesa tunazo hatuhitaji pesa zako za kutengeneza mashine hiyo, ili waziri ikishapita bajeti hiyo ikafanye kazi shughuli zile ambazo tumekubaliana.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa bado nilikuwa sijaridhika kwa heshima kubwa na taadhima ukiwa kama Spika vile vile, ulininasihi kama ni kiongozi katika Baraza la Wawakilishi na *hansard* yako wewe ninayo vile vile kwamba Mhe. Mohammedraza Hassanali pitisha bajeti hiyo kwa kuwa tayari Waziri wa Fedha ameshakiri kwamba pesa zipo Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ikakufanyie kazi yako.

Vile vile ukanitaka niwaandikie nikakae nao, leo tunaingia tena kwenye bajeti hii, na kwa kweli ni siku nzuri kwa sisi Zanzibar kuamkia kesho ni Mwezi 15 Shaaban, jambo hili halijatekelezwa, sikuambiwa, sikuitwa wala

sikufanyiwa chochote, yaani Mhe. Mwenyekiti, hili jambo nimelizungumza kwa niaba ya wananchi. Sasa nataka Mhe. Waziri anijibu kwamba nilitiliwa dhamana, na wewe Mwenyekiti pamoja na Waziri wa Fedha na humu tumerejea tena leo naomba majibu ya Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru, kwanza naomba radhi kwamba suala lake sikuwahi kulijibu pengine kwa kughafilika au matatizo ya muda, lakini ni kweli Mhe. Mwakilishi alitaka kujua, kwanza niseme kwamba barabara hizi anazozitaja yeye ilikuwa amekuja kuelewana na *UUB* ili wamsaidie katika ujenzi na alichangia shilingi milioni 20.

Pamoja na kwamba *UUB* imejenga kilomita mbili kutoka Pagali hadio Umbuji, lakini barabara yenyewe iliyotakiwa kujengwa haikukamilika *bulldozer* likaharibika, na kama alivyoeleza mwenyewe katika maelezo yake kwamba *bulldozer* lile lilipopelekwa mjini likaharibika siku chache, basi kutokana na uchakavu wa zana na ujenzi wa barabara wizara inakubali kwamba imeshindwa kuendelea na ujenzi wa barabara hizo kutokana na kazi nyingi ambazo tunaendelea nazo.

Wizara inachukua jukumu la kurejesha fedha hizo na tunamshauri Mhe. Mwakilishi kuwatumia wakandarasi binafsi ili kukamilisha ujenzi wa barabara hizo. Wizara pia ipo tayari kumpatia wataalamu wa usimamizi wa ujenzi wa barabara hizo bila ya gharama yoyote.

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: Mhe. Mwenyekiti, humu ndani tumo watu wazima na tumekuja kufanya kazi za wananchi, sasa kama tutafika pahala tunaleteana vitu ambavyo sivyo si vizuri. Kwanza mimi sijakubaliana na *UUB;* nina barua ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano sio kweli anavyosema Mhe. Waziri, naona tabu sana kumwambia mtu muongo, samahani sana Mhe. Waziri, lakini si kweli nina barua ya Katibu Mkuu aliyoidhinisha kwamba pesa nitoe hizi serikali itafanya hivi.

Halafu akakubali kwamba atakwenda kutengeneza Waziri wa Fedha kakiri, Mhe. Mwenyekiti ukakiri, leo sisi tunakwenda padogo tu anakuja anageuza kabisa kauli yako wewe, kauli ya Waziri wa Fedha, hii ni serikali, mimi nimekuja kwa niaba ya wananchi na kama tulifanya Mapinduzi ndio neema yake hii.

Sasa huu ni uonevu, hii ni dhulma kwa wananchi; wananchi wanaumia, leo ninafanyiwa makusudi kwa niaba ya wananchi. Mimi sijaridhika na kauli hiyo iliyotolewa ambayo haina kichwa wala miguuu. Naomba Mhe. Waziri aeleze kitu bila ya kutafuna maneno.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, kutokana na hiyo kazi kama nilivyosema mwanzo kuwa kazi ilifanywa ya Pagali mpaka Umbuji yenye urefu wa kilomita mbili (2), lakini Mheshimiwa hakuridhika, sasa kwa sababu sisi tumechukua muda mrefu, wizara imeamua kutokana na hali ilivyo imrejeshee zile zile pesa alizotoa hata kama kazi ile tuliifanya, ili akatafute wakandarasi binafsi, kwa sababu sisi itakuwa wizara yetu haina uwezo wa kujenga zana zake chakavu.

Sasa tutakuja kupigishana kelele bure na tushakubali kwamba zana zetu ni chakavu hazina uwezo, tutakuja kumdanganya halafu aje aseme tena tumemdanganya. Sisi tunataka kumrejeshea kile kitu chake ambacho alikitoa pale mwanzo shilingi milioni 20.

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: Nakubali kwamba serikali inaendelea kuwadanganya wananchi na inaendelea kuwatesa wananchi wa Unguja na Pemba, nataka kauli hiyo serikali itoe iseme kwamba imewadanganya wananchi, na wananchi waendelee kudanganywa na kuteswa na Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Mwenyekiti: Tusaidieni Waheshimiwa maana kuna maelezo hapa ya kwamba Mhe. Waziri yuko tayari kurejesha pesa ili kazi hiyo akatafute mkandarasi mwengine, lakini Mhe. Mjumbe yeye alitoa pesa ili kuiomba serikali isaidiane naye kutengeneza hiyo barabara ambayo imefanyika kazi kiasi ya kilomita mbili (2). Je, kama inatosheleza hiyo au vipi.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, labda aseme yeye anachokitaka ni nini hasa, maana sisi hatukifahamu. Kwa sababu sisi tuliji-*commit* kujenga njia lakini tunakubali kwamba kutokana na zana zetu chakavu, na kwa kipindi anachotaka yeye tumjengee tumeshindwa. Sasa ili kumpa yeye fursa aendelee na kazi

zake wakandarasi binafsi wapo siku hizi, kwa hivyo tumpe ile ile *cash* yake ambayo ameitoa ili sisi tuondokane na lile jukumu hatuliwezi kwa sasa, sijui yeye anataka tumwambie vipi tena.

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: Mhe. Mwenyekiti, bado niko pale pale tulikuwa na makubaliano kati ya Mwakilishi wa Jimbo la Uzini na serikali. Mimi nimetoa pesa zile zikawahudumie wananchi, kama mnasema basi na mimi niko radhi hizo pesa kuzisamehe kwa niaba ya wananchi, Mwenyezi Mungu atanijaalia na iendelee na dhuluma hiyo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mhe. Waziri kwa maelezo yake lakini pia nimshukuru ndugu yangu Mohammedraza Hassanali kwa imani kubwa ya kutaka kusaidia wananchi wake ili aweze kukamilisha ujenzi wa barabara ya jimbo lake.

Mhe. Mwenyekiti, nia na dhamira ya serikali yetu ni kupunguza matatizo kwa wananchi wetu na moja katika eneo ambalo serikali inalipa kipaumbele ni suala zima la ujenzi wa barabara. Lakini kwa bahati mbaya uwezo wa wizara kuzikamilisha kazi hizo kwa wakati mmoja ni mdogo, ndio maana wizara imeweka vipaumbele vya utengenezaji wa barabara hizo.

Sasa kwa sababu ya umuhimu na haraka iliyopo katika utengezaji wa barabara katika Jimbo la Mhe. Mjumbe, kwanza tunamshukuru kwa mchango wake huu ambao aliutoa katika kurahisisha hiyo shughuli, lakini kutokana na hali halisi ambayo Mhe. Waziri ameeleza haitawezekana kufanyika kwa wakati huu ambao Mhe. Mjumbe anataka ifanyike, lakini siku zote serikali nia yake ni kulimaliza tatizo hili.

Kwa hivyo, tunamuomba Mheshimiwa aendelee kuvuta subira wakati wizara ikiangalia uwezekano wa kutengeneza barabara hizo pale ambapo kutatokea uwezo wa kufanya hivyo. Kwa kuwa yako maeneo mengi muhimu vile vile ambayo yanapaswa kutengenezwa, sasa basi tumuombe akubaliane na ushauri kwamba, asubiri wakati wizara inaangalia uwezekano pale tu itapopatikana nafasi ya kutengeneza barabara hizo ziweze kutengenezwa, na sasa hata akisema kwa namna yoyote ile bado tatizo kama ilivyosema wizara kuna uchakavu wa mashine. Kwa hivyo, haitawezekana kufanyika vile ambavyo yeye anataka ifanyike.

Sasa ushauri wa wizara ambao na yeye hakubaliani nao basi nimuombe aendelee kuvuta subira angojee maamuzi ambayo wizara wana nia nje ya kulifanyia kazi, na serikali nzima ina nia ya kuondosha tatizo la barabara, lakini ajue kwamba uwezo wetu kama nchi ni mdogo itategemea hali ya uwezo pale itaporuhusu shughuli hii itaendelea Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: Mhe. Mwenyekiti, *penye nia pana njia*, tulipokuwepo hapa mwaka jana Waziri alisema ana upungufu wa shilingi milioni 16 kwa sababu ya mashine imeharibika, halikuwa tatizo la kutengeneza barabara zangu za Jimbo la Uzini, na nilimwambia hizo shilingi milioni 16 kama mashine imekwama inatakiwa *spare* kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Uzini niko tayari kuzitoa tena, mimi nimetumwa hapa na wananchi wa Jimbo la Uzini.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri wa Fedha akasema ili kazi yako ikafanywe *hansard* hii hapa, basi pitisha hicho kifungu serikali inazo pesa na wewe Mhe. Mwenyekiti ukasisitiza zaidi. Tatizo lilijitokeza kwamba ile mashine Wizara ya Fedha imetoa pesa mashine imetengenezwa, lakini mashine ile imekwenda kufanya kazi *Mkapa Road* sivyo tulivyokubaliana. Sasa hoja yangu iko hapo tu, kwamba vile tulivyokubaliana sivyo, haikuwa kwamba leo Mhe. Waziri kufika kusema kwamba hili jambo haliwezekani.

Mhe. Mwenyekiti, bado nataka nimuombe sasa kwa heshima na taadhima ili tupate kuendelea, Mzee wangu, kiongozi wetu, baba yetu Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar basi anihakikishie kwamba katika muda usiokuwa mkubwa hili suala litafanyiwa kazi kwa kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, maelezo ya Mhe. Mohammedraza Hassanali mazuri lakini pia ningependa kwa sababu Mhe. Mohammedraza Hassanali ana imani kubwa na wananchi, na kwa kuwa pia matengenezo ya *Mkapa Road* yanasaidia sana wananchi wengi katika jukumu hili la kusaidia wananchi, ningependa aendelee kupokea ushauri ambao wizara imeshauahidi, sasa kwamba nia wanayo ya kutengeneza barabara ile lakini ni uchache wa vyombo. Kwa sababu kama alivyoeleza kwamba sasa hivi

wanashughulikia barabara ya *Mkapa Road* kwa vyovyote vile wakimaliza huko wataona sasa uwezekano wa kuzishughulikia barabara ambazo Mhe. Mohammedraza Hassanali amesema, na hiyo ni mipango ya wizara.

Sisi tungewaomba sana wizara, kwa sababu kumbe kulikuwa na makubaliano kati ya Mhe. Mwakilishi na wizara pale ambapo watatengeneza hiyo mashine aweze kutengenezewa barabara zake.

Kwa hivyo, tuwaombe wizara nitashirikiana nao ili kuhakikisha kwamba pale watakapomaliza jukumu la kutengeneza *Mkapa Road* waone uwezekano wa kuishughulikia barabara ambayo Mhe. Mwakilishi na wao wizara walishakubaliana.

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: Mhe. Mwenyekiti, mimi namuheshimu sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Mimi niliipa serikali mkopo wa shilingi milioni 71 Mhe. Waziri akaja akasema sijaikopesha serikali anasema Mapinduzi *CUP* ya *NGO* wakati Mapinduzi *CUP* ya Rais.

Sasa Mhe. Waziri kauli hii anataka kuja kunipa mimi wakati pesa zangu keshazikanusha anasema sijaipa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Makamu wa Pili wa Rais ndiye aliyekuja akathibitisha kwamba Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali pesa kazikopesha na akazilipa, yeye Mhe. Waziri anasema sijakopesha serikalini. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, bado ninaomba jambo hili kwa sababu ni la wananchi, limegusa wananchi, na kama Mapinduzi basi vile vile Bambi yalianza Mapinduzi Matukufu katika kuchangia nchi hii.

Kwa hivyo, ninachoomba bado nataka nipewe haki yangu kama ni Mwakilishi wa Jimbo la Uzini nimekuja hapa kwa niaba ya wananchi. Serikali kupitia baba yangu Makamu wa Pili wa Rais na Kiongozi wa Baraza hili tukufu siwezi kuzungushwa. Mhe. mwenyekiti wewe ushadanganywa, Waziri wa Fedha keshadanganywa, mawaziri wote kasukuma hapa, kilichobakia ni Makamu tu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa kaa kwanza.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, muda unakaribia kumalizika, kazi tuliyopanga kumaliza hatujaimaliza. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa muda ulio mbele yetu hautoshi kumaliza shughuli iliyo mbele yetu. Na kwa kuwa muda wetu tunamaliza saa mbili kasorobo na kazi iliyopo ni kubwa, tuliombe Baraza lako Tukufu tuweke kanuni kando ili tuweze kumaliza shughuli iliyo mbele yetu. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe, wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

Kamati ya Matumizi

Mhe. Mwenyekiti: Tulifikia pahala kwamba Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali alikuwa anaomba kauli ya Serikali. Mhe. Makamu wa Pili wa Rais karibu.

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru tena maana nimegeuka kuwa *Sectoral Minister* sasa. Mimi ningependa kwanza kumshukuru ndugu yangu, rafiki yangu na mwanangu Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali kwa uvumilivu aliouonesha kwa muda mrefu ambapo huduma aliyoiomba hakuweza kuipata kwa ajili ya wananchi wake wa Uzini, lakini nimuahidi kwamba sasa suala hili nitalichukua mimi na nitalifuatilia na Waziri muhusika kuhakikisha kwamba yale ambayo Serikali na yeye wamekubaliana yanatekelezwa. Namuahidi kwamba nitalifuatilia hilo kwa kina kuhakikisha kwamba hilo linafanyika. Ahsante.

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa na hekma aliyoitoa mzee wangu, na busara na usikivu, basi mimi nina imani na Serikali yangu kwa kauli yake aliyoitoa Serikali ya Mapinduzi

ya Zanzibar. Na ninaamini yeye pamoja na Mhe. Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, naomba tuendelee nimeridhika na kauli yake.

Mhe. Asha Abdu Haji: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, suala hili kila siku na mimi nalitaja. Kwa kuwa Wajumbe wote kila anayesimama anatupia Serikali, na mimi kila siku nikizungumza suala hili la njia ya ndani ya Jambiani Mfumbwi hadi Kibigija ambapo suala hili kila tukilizungumza hatufanikiwi. Na mimi naomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais pia anitengenezee njia ile angalau kwa kifusi tu ili wananchi wafaidike na matunda yao ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Tupate maelezo ya Mhe. Waziri kwanza.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, naomba na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli suala analoliuliza Mhe. Asha Abdu Haji lina umuhimu. Barabara ya katikati anayoizungumza kwa watu wenyeji wa Kusini nadhani inaishia kule Domokuchu, kutoka Jambiani Mfumbwi-Kibigija-Kichakanyuki mpaka Paje. Eneo hili ni eneo la utalii, na ni kweli kwamba barabara hii ni barabara ya pili. Ukitoka Makunduchi Kigaeni unaishia Paje *round about.*

Lakini siku zote limekuwa likiulizwa na majibu ya Serikali yapo wazi kwamba kutoka huko huko Kigaeni mpaka *round about* ya Paje tayari Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeshajenga mradi mkubwa wa barabara ya lami. Katika mradi wa barabara za lami umetoka Paje mpaka Michamvi Kae, ukatoka Paje mpaka Makunduchi Kigaeni.

Sasa majibu ya Serikali yapo wazi; kwamba jukumu la barabara hii ya ndani tunayoizungumza ni jukumu la halmashauri. Na kwa kutambua kwamba halmashauri zetu mapato yake madogo, Mfuko wa Barabara kwa mara ya kwanza mara hii umetenga fedha maalum kuziwezesha halmashauri zetu kuwa na fedha. Na Wizara yetu tumekuwa tukisema kwamba tupo tayari kutoa msaada wa vifaa na wataalamu katika kusaidia na kufanya kazi za ndani.

Sasa tunachochelea kusema kwamba barabara hii yenye urefu takriban zaidi ya kilomita 10 kuwa wizara yetu tutaijenga hatuwezi kufanya kwa sababu hatuna bajeti ya hilo, hatuna nguvu ya kufanya hilo. Sasa kama kuahidiwa tunaweza kumuahidi lakini hatutotekeleza. Ndio maana tumekuwa tukisema kwamba busara tukae tuzungumze na wenzetu wa halmashauri. Na kwa sababu mara hii wamepata pahala pa kuanzishwa nguvu, sisi tupo tayari kutoa msaada wa vifaa na wataalamu wetu kwenda kujenga kwa kiwango cha kifusi.

Sasa kama wenzetu hawatuelewi wawe na sababu nyengine, lakini kama sababu ya uwazi ndio huo. Kwa sababu Serikali hiyo hiyo haiwezi kujenga barabara *parallel* mbili kwa kiwango cha lami katika eneo moja. Sote tunahangaika kuona angalau tunatanua mtandao wa barabara kwa maeneo yote. Kutoka Paje mpaka Makunduchi tayari barabara ya lami imeshajengwa. Hatuwezi leo hii Serikali tukalazimisha kujenga barabara nyengine ya lami kutoka Paje ile ile mpaka Makunduchi kwa kupita ndani.

Sisi kama Serikali tupo tayari kujenga kwa kiwango cha kifusi kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kusini. Msaada wetu ni ufundi, msaada wetu wa vifaa tena vikiwa vizima. Tupo tayari kwenda kusaidiana nao. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Asha Abdu Haji: Mhe. Mwenyeki, namshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini namuuliza ni vifaa gani ambavyo atatuletea. Ikiwa eneo la kuchimba fusi kule Jambiani lipo. Atwambie atatuletea gari au atatuletea vifaa gani?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, nadhani utaratibu wa kujenga barabara uko wazi. Fusi, mchanga kwa kiingereza wanaita *materials* ambazo ndizo wanazotumia katika ujenzi wa barabara. Tunapozungumza vifaa ni zile zana zenyewe kama kijiko, *bulldozer*, gari la kuchimbulia na gari ya kubebea kifusi na zana nyengine. Tunapozungumza vifaa tunamaanisha zile zana za kuweza kutumika kwa ajili ya ujenzi wa barabara.

Kwa hivyo, tunatambua kwamba eneo la Paje mpaka Makunduchi tuna maeneo mengi ambayo yanamilikiwa na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ya kuchimba kifusi. Kwa hivyo, tunapozungumza vifaa kwa maana ya kwamba zana za kufanyia kazi, vile vitendea kazi vyenyewe. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Asha Abdu Haji: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, namuuliza Mhe. Naibu Waziri. Je, hawa Mwakilishi na Mbunge anaomba wachangie nini. Na mimi katika maombi yangu sio naomba kwamba atutilie lami, naomba atutilie fusi tu.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, nikuombe tu baada ya kupitisha bajeti hii Mhe. Mwakilishi aje ofisini tutazungumza tuweze kuona mpango gani wenzetu Wabunge hawa wataweza kutoa kwa kupeleka kwenye halmashauri yao ili tuweze kwenda kuifanya kazi hiyo.

Mhe. Asha Abdu Haji: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru lakini kila siku hadithi ndio zile zile. Ningemuomba anitajie ni lini, nitamchukua na Mwakilishi wangu, maana yake mimi ni Mwakilishi wa Viti Maalum, lakini huyu ndiye Mwakilishi wangu. Na mimi ni mkaazi wa kule kule Jambiani ndio ninakoishi yale matatizo nayaona. Gari kubwa kila siku zinaharibika difu, na gari ndogo kila siku zinaharibika *shock absorber*. Sasa nauliza lini anatuhakikishia atatutengenezea njia ile kwa fusi tu hatutaki ya lami, njia yote imeharibika kuna mashimo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Asha Abdu Haji alichosema Mhe. Naibu Waziri kwamba baada ya kumaliza shughuli hizi nyinyi mwende ofisini mpange hayo. Wewe Mwakilishi na Mwakilishi, kama kuna na Mbunge, basi mwende mkapange hayo.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa hii ya kuweza kumuuliza tena Mhe. Waziri. Mhe. Mwenyekiti, wakati nikichangia nilizungumzia suala zima la barabara ya Kisiwandui-*Wireless*.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana na nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo yamenipa mwelekeo mzuri na kunipa tamaa kwamba barabara hii sasa itaanza kushughulikiwa.

Pamoja na hayo Mhe. Mwenyekiti, nimezungumza na Katibu Mkuu vile vile na yeye ameniahidi kwamba watakapomaliza pale barabara ya Mkunazini *round about* basi vifaa vyao hawataviondosha na watavileta katika barabara ya Kisiwandui.

Mhe. Mwenyekiti, nilimuuliza hapa Mhe. Waziri na hilo nataka tena kulijua. Wameniambia watamaliza lakini ni lini watakuja pale. Nilikuwa nataka kauli yake mwenyewe Mhe. Waziri kwamba lini watakuja katika barabara ile na kuanza kuifanyia matengenezo. Naiomba kauli sasa ya Waziri.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, kauli yangu haitatofautiana na kauli ya Katibu Mkuu wangu. Kwa hivyo, kama alivyosema Katibu Mkuu mara baada ya kumalizwa pale Haile Sellassie-Mkunazini basi tutachapia pale pale hazitaondoka zana tukijaaliwa.

Lakini kuna tatizo moja ambalo ni la kimkataba. Hii kampuni inayoitwa *Abdalla Contractor* ilikuwa imeshatia mkataba na ujenzi wa barabara ile. Sasa inashughulikiwa kwa sababu wameshindwa kazi ili tuweze kuishughulikia wenyewe.

Lakini naamini kabisa kutokana na ile ari tuliyoianzia ile kazi ilikuwa sasa hivi iwepo mbali. Lakini mazingira ya kimkataba yametuzuia kuingilia upesi upesi asije akapata nafasi ya kudai jambo ambalo lipo nje na uwezo wetu. Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Mwakilishi hasa hasa vile vile Mhe. Mwenyekiti wetu, Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa ambaye naye ni Mwenyekiti wa Baraza, Mwenyekiti wa Kamati yetu katika Mawasiliano na Ujenzi, basi vyeo vyote hivyo kwenye viti viwili hatuwezi kuwaangusha.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, sasa Mhe. Waziri kidogo amenitia wasiwasi. Amesema kwamba mpaka yule ambaye wamefunga naye mkataba wafanye makubaliano. Sasa Mhe. Waziri hapa kidogo umenitia wasiwasi, inavyoonesha inaweza kuchukua zaidi ya ule muda ambao tulikuwa tunautarajia. Mhe. Waziri nimetaka kauli yako ni lini barabara ile itajengwa?

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema mwanzo kwamba tutahakikisha tukijaaliwa ndani ya mwezi wa Julai basi mambo yote yanakamilika na kazi itaanza, hiyo ni hakika kabisa. Kwa sababu hata huyo mkandarasi tutakuwa na njia naye, kwamba mwaka wa fedha umeshamalizika Juni 30, hakuna njia tena ya kurudia nyuma. Kwa hivyo, tukiingia Julai tukijaaliwa ni hakika kwamba kazi ile itakuwa

imeshaanza. Na hilo tutalihakikishia kwamba linatokea, lakini kazi ile Mhe. Mwenyekiti, na mimi inanihusu binafsi, yeye anajua jinsi gani ambavyo ni mpenzi wa Kikwajuni. Kwa hivyo, kazi ile tutaifanya kwa njia zote tukijaaliwa. Pale pana msikiti mzuri Mhe. Mwenyekiti. Kwa taarifa yako kabla hatujaondoka pale ndio uliokuwa msikiti wetu.

Mhe. Mwenyekiti, msikiti ule una kitu kizuri katika Zanzibar padogo sana unapopata. Mhe. Mwenyekiti, siku ya Ijumaa unatiwa udi ule msikiti, kwa hivyo watu wote waliomo ndani tunawapiga kampeni wakasalie pale. Sasa ikiwa hakuna barabara watakwenda vipi wale. Kwa hivyo, tunamhakikishia Mhe. Mwenyekiti wawili hawa kwamba barabara ile tutaishughulikia tena katika kiwango cha lami.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Waziri kwa kutoa ahadi hiyo na mimi ningewaomba sana wananchi wa Kikwajuni, basi pale ambapo barabara hiyo itaanza kujengwa waweze kutoa mashirikiano. Nakushukuru sana Mhe. Waziri.

Kifungu 0701 -	Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara	165,488,000
Kifungu 0801 -	Idara ya Usafiri na Leseni	200,515,000
Kifungu 0901 -	Idara ya Uendeshaji na Utumishi	

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub, baadae Mhe. Hija Hassan Hija.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana kwanza. Baada ya muda mrefu kusimama na hivi kuweza kuniona.

Hoja ilikuwa Mhe. Hamza Hassan Juma, kwanza ukurasa 59 (3), Mhe. Waziri, naomba kunukuu baada ya kulipotosha Baraza;

"Mjumbe yeyote anapokuwa akisema Barazani atawajibika kuwa na sababu za msingi kwamba maelezo anayotoa ni sahihi na sio mambo ya kubuni au kubahatisha tu. Mhe. Spika, au mjumbe mwengine yeyote anaweza kutamka Mjumbehuyo anayesema atoe uthibitisho wa usemi wake anaohusika".

Mhe. Mwenyekiti, niliuliza swali mimi hapa katika kipindi cha maswali na majibu. Swali Nam. 23, kuhusu usumbufu wanaopata wananchi Uwanja wa ndege wa Zanzibar. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejitahidi kuhakikisha kuwa wananchi wake wote kuwa hawapati usumbufu wanaopata huduma mbali mbali, ukweli huo upo kinyume na hali inayoendelea katika hali ya Uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Abeid Aman Karume Zanzibar, iwapo mlango wa kutokea nje wa uwanja wa abira huathiri, kumeathiri mkanda wa kuzuia na kupita, badala yake abiria wanatakiwa wazunguke upande wa kushoto mwa mlango hali ambayo inawasumbua abiria waliochoka safari nyengine kuwa ni za mbali. Kwa nini mlango ule umeekwa ukanda wa kuzuia abiria unaoathiri wasipite, wakati wafanyakazi wanapita na hapana sababu. Jawabu nililolipata hapa halikuniridhisha kabisa na maneno aliyotoa Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, leo anasema bodi imeshusha vibao pale. Mhe. Ismail Jussa Ladhu, juzi kenda pale vibao havipo na gari zinafungwa. Mhe. Waziri, kwanza aombe radhi kwa Wajumbe wako sisi, kwa kulipotosha Baraza, gari mpaka leo zinafungwa.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu baada ya kuomba radhi, lini utakwenda wewe mguu kwa mguu ukaacha kuchukua usemi wa kubahatisha tu, kukaa Ofisi ukaambiwa jambo hili lishafanyika wakati hufuati majukumu yako. Ni lini utafuatilia majukumu yako. Wananchi wanateseka, wagonjwa wanateseka, *wheel chairs* hapana, pale anashushwa mgonjwa gari inafungwa. Wazanzibari kweli hawana haki katika nchi hii.Mgonjwa anapelekwa matibabu, anakuwa na matibabu mengine pale pale *Airport* anapewa na maradhi mengine. Ninataka kauli sasa hivi serikali itoe tushachoka kupiga kelele humu ndani, mimi nikawa ninaleta maswali pale ukanda umefungwa, hakuna sababu ya kufungwa ukanda ule, huku abiria wanateseka.

Hoja yangu ya pili. Eneo la Forodhani (Forodha mchanga) kufungwa. Pamejengwa eneo pale, bado meli zinapata usumbufu kwenda kufunga kwa sababu ya kima cha maji ni kidogo na imekuwa ni ya dharura. Leo tumeshuhudia meli ya kasa kukaa siku nne. Hatuendi kwa ubaguzi na ni kinyume na Katiba ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, naomba majibu.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, hoja ya mwanzo nimekwisha kuijibu na ipo kwenye meza yako inangojea maamuzi ambayo aliitoa Mhe. Hamza Hassan Juma, katika hoja zake nne alizozichangia kwa mpigo. Ni hoja ya maegesho ya Uwanja wa ndege na imo katika hoja nne alizotoa Mhe. Hamza Hassan Juma, ambayo yanaongojea maamuzi ya Baraza. Kwa hivyo, maelezo ndio yale nilikwishakutoa mimi, nijitahidi yangu kama nilikwisha kusema mwanzo nilivyofanya na bodi walifanya, kama Baraza halijaridhika maamuzi yapo kwenye meza ya Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, lakini hoja ya pili, kila kitu kinapangwa kwa utaratibu na sidhani kama tutakuwa kila kitu tukiulizie baada ya kwisha kupita ule utaratibu. Bandari ni eneo ambalo serikali huwa inalichagua makusudi kwa ajili ya shughuli ile na lina taratibu zake, lina wafanyakazi wake na lina mipango yake. Pale pana *Post master*, pana sijui nani, watu na vyeo vyao tofauti. Hii ndio inaitwa bandari, lakini sio kila pahala pataegesha vyombo. Sasa hapo Forodha mchanga anapozungumzia yeye, zilipewa ruhusa zile meli zilizokuwa hazina mvungu kwa muda mpaka pale fursa itapopatikana. Bahati nzuri pale bandarini tumepata *Terminal* mpya ya boti wanayopanda abiria, lakini pembezoni yake pamejengwa *ramp* na mfanyabiashara maarufu Ndugu Said Bakharessa. Sasa *ramp* ile iliyojengwa wakaelekezwa meli zote za aina ile zifunge pale ili ziteremshe mizigo na kama kuna watu vyovyote vile wateremshwe pale ili ziweze kuangaliwa na bandari zijulikane saa ngapi zinaingia na saa ngapi zinatoka.

Mhe. Mwenyekiti, mamlaka ya Mji Mkongwe ikishirikiana na Mkuu wa Mkoa na Manispaa, ndio waliofunga eneo lile la Forodha mchanga kuegesha zile za aina hiyo. Sasa ukisema urudi tena kuziruhusu meli zifunge pale. Sasa utaratibu huo upo wapi katika uendeshaji wa bandari. Wakati hapa aliuliza swali Mheshimiwa huyo huyo, nikamwambia kwamba sio kweli kwamba meli nyengine haziruhusu, kwa sababu mimi mwenyewe nimeshuhudia kwa macho yangu si chini ya mara tu au nne, ninapita pale meli nyengine ikiwa *Buraq* na wengine wanateremsha na kupakia mizigo pale katika hiyo *ramp* inayotajwa.

Sasa mambo mengine sio yetu sisi, ni ya Manispaa na Kamati ya Ulinzi na Usalama, sio ya wizara yetu. Sisi ilikuwa yetu wakati ilipokuwa ni bandari. Sasa tumeiondoa kwenye bandari haimo tena, si bandari. Kwa hivyo, kama kinakuja chombo chengine kuweka nanga pale, sio mamlaka yetu ya bandari kwa sababu sisi kwa bandari hairuhusiwi tena meli kibandari kutia nanga pale au kuegesha pale.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nitazungumza kidogo kidogo ili apate kunisikia Mhe. Waziri, labda nilikuwa nafikiri nazungumza haraka haraka hapati kunisikia. Mhe. Waziri, naomba unisikilize kidogo kidogo.Ulipokuwa ukijibu swali mulisema pale vile vibango vimeshaondoshwa na gari haitofungwa, ndio hoja yangu na Mhe. Hamza Hassan Juma yake mbali na yangu ni tofauti, vibao vile vimeondoshwa na leo bado watu wanateseka.Leo kama wewe Waziri umeshatoa amri hiyo, sasa hiyo bodi na wewe waziri nani mkubwa? Nafikiria bodi ipo chini ya dhamana yako. Mimi nafikiri twende tukashuhudie ukatoe amri mbele yako na uite mkutano, bado wagonjwa wanateseka pale, kuondoshwa si hoja, bado watu wanasumbuliwa, kuondoshwa wameondoshwa.

Mhe. Mwenyekiti, vibao vimeondoshwa, lakini bado wafanyakazi wanawatesa, watendaji sio wamo humu ndani, aseme tu Waziri. Wale watu wameshachoka kuteseka kuna wagonjwa. Tumeshuhudia Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, humu kafiliwa na mama yake, alikutana na mimi, ana uchungu wa mama yake huku gari inafungwa. Tunafanya nini? Ajibu tu kama tunakwenda kesho au keshokutwa, twende tukashuhudie hapafungwi gari na ikifungwa gari atachukua hatua gani, atawafukuza wafanyakazi.

Mhe. Mwenyekiti, hoja ya pili, ni kuwa pale pana mkanda pale, abiria akishakushuka umefungwa mkanda, hakuna sababu ya kuzungushwa nyuma huko, utafikiri anakwenda kuchinjwa. Watu siku nyengine wanakuja na pesa zao, ni lazima ashushe pale pesa, hawezi kwenda kule kwa sababu ya suala la ujambazi, usalama haupo.

Mhe. Mwenyekiti, hoja ya tatu, ilikuwa pale palipojengwa alisema mfanyabiashara mmoja kumwita, bado meli kima cha maji hakiruhusu kwenda.Sijui umeshanifahamu Mhe. Waziri, haya niliyoyazungumza.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze na hii hoja ya mwisho ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Ni kweli kwamba kama maelezo aliyoyatoa Mhe. Waziri, kuwa eneo la Mji Mkongwe kwa mujibu wa sheria zetu wenyewe tuliyoingia na *UNESCO*, sheria za Uhifadhi wa Mji Mkongwe kuna utaratibu maalum kwa magari yetu ya kuingia Mji Mkongwe, si magari yote yasiingie Mji Mkongwe. Kwa mujibu

wa sheria ile inaelekeza kwamba Mji Mkongwe ni *Free traffic zone*, kwa maana kwamba ni eneo ambalo halitakiwi kuingia magari, lakini katika utekelezaji wake ikawa inakwenda hatua baada ya hatua, kuna magari ya tani nne, kuna tani mbili. Mhe. Waziri, hapa ameeleza vizuri kwamba kwa mujibu wa taratibu za kibandari, eneo la Forodha mchanga lilikuwa likitumika kwa wakati maalum kwa mahitaji maalum.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kutambua kwamba eneo la Forodha mchanga ni eneo la Mji Mkongwe na kwa kutambua ile sababu ya msingi kwamba hatukuwa na maeneo mengine ya maegesho ya meli za *Land craft*, tukalazimika tutumie eneo la Forodha mchanga ili kuweza kutoa huduma. Hivi sasa tayari serikali kwa kushirikiana na mfanyabiashara tumepata eneo la *ramp* kwa ajili ya kutoa huduma ya kuegesha za *Land craft*.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hoja ya Mhe. Mjumbe, kwamba kichelezo kiliopo bandarini kuna baadhi ya wakati hakiwezi kutumika, kwa maana ya kwamba kima cha maji kinakuwa kidogo. Hilo ni kweli na serikali tumesema zaidi ya mara tatu kwamba sisi kama bandari kwa kushirikiana na mfanyabiashara huyu, tayari mwenzetu huyu ameingia gharama za kuagiza mashine mpya za kuchimbia, lakini pia, mtaalamu kutoka Nigeria ambaye anakuja kumsaidia namna ya kuweza kuchimba vizuri ili *ramp* iweze kuvutwa mbele ili tuweze kupata huduma ya kuegesha meli kwa wakati wowote.Yeye mwenyewe binafsi meli yake ya *Sealink* ambayo kwa bahati nzuri maumbile yana mkuku chini, maji yanapokuwa yapo *tight* hapo chini, hawezi kuifunga.Kwa hivyo, yeye mwenyewe binafsi inamshawishi na kumtia hamasa kuweza kuona kwamba tunachimba mbele zaidi, kurefusha kichelezo ili kuweza kutoa huduma.

Mhe. Mwenyekiti, lakini Kamati ya Ulinzi na Usalama iliangalia kwa kina, zaidi ya kwamba tunapata nafasi ya kuegesha katika eneo la Forodha mchanga, wakaona kwamba kiulinzi na kiusalama tunalazimika kwamba eneo hili tuzuie kuingiza na kuegesha vyombo kwa kutambua kwamba unapoegesha vyombo pale, utashusha mizigo wakati wa usiku na mchana, utapakia magari wakati wa usiku na mchana na hali ya usalama kwa walipozuia haikuwa vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, sasa mimi nimuombe sana Mhe. Mwakilishi, kwamba azingatie yote mawili; La kwanza, umuhimu wa kuwa na *Ramp,* kima cha maji kinakidhi serikalini. Tunalazimika kushirikiana na mwenzetu tuongeze kima cha maji ili *Ramp* ile iweze kutumika muda wote. La pili, usalama wa nchi yetu nao ni muhimu kwamba kule Forodha mchanga, wenzetu wa vyombo vya usalama wameona kiusalama hapako vizuri kuendelea kufanya shughuli hizo. La tatu, pale kwa mujibu wa taratibu za Uhifadhi wa Mji Mkongwe hatulazimiki kufanya tena shughuli zile za kuegesha meli kwa sababu yale malengo ya Mji Mkongwe yanatuzuia.Tumejibu pale kwamba tokea kutiwa eneo lile wanaishi pale, wanaofanya biashara pale wameridhika na utaratibu na kimya.

Mhe. Mwenyekiti, suala la pili, alilouliza Mhe. Mwakilishi, alizungumzia suala la mikanda. Yaani mtu ambaye anashuka ndege na mtu ambaye anataka kwenda katika ndege kwa ajili ya safari. Nalo tumelieleza kwamba madhumuni makubwa hatuhitaji kuona mwananchi abiria anapata usumbufu wa aina yoyote, lakini tumesema kwamba mazingira ya mlango ule uliopo, kwa maana ya ile *arrive* na anayetaka ku-*departure* yapo karibu sana. Tukasema kwamba baadhi ya nyakati sasa siku za msimu, wanakuwa wageni wanaotoka wanakuwa ni kundi kubwa. Kundi lile linalotoka kukiwa na watu wanaotaka kuondoka kuna taratibu zake kiusalama. Hatukuzuiwa kwa utashi na kama vigezo vitaelekeza kwamba kama hakuna athari hatuoni tatizo, kuruhusu ukitoka badala ya kuzunguka mkono wa kushoto, upite moja kwa moja.

Mhe. Mwenyekiti, lakini tutambue utafika wakati kuna kundi la wageni linafika na kuna kundi linataka kuondoka, tunaweza tukapata tatizo iwe la kiusalama, taratibu za uhamiaji au tatizo jengine lolote, kimsingi kwamba malengo ukitaka kuona kwamba tupate urahisi mzuri kwa wanaofika na wanaotaka kuondoka, lakini mamlaka haikuzuiya, ama serikali haikuzuiya kwa malengo au kwa madhumuni ya kutaka kuwakomoa watu. Kwa hivyo, sisi tupo tayari kushirikiana na wenzetu tuweze kuona namna gani ya kuweza kuimarisha huduma kwa wanaosafiri na wanaoingia nchini bila ya kusababisha usumbufu kwa kuzingatia vigezo na maelekezo ya serikali, pamoja na taratibu za Kimataifa za usafiri wa anga.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu utaratibu wa usafiri wa anga hau-*reflect* na sehemu moja, taratibu zao ni lazima tujue kwamba ni taratibu za nchi yetu lazima ziendane na taratibu za kikanda, lazima ziendane na taratibu za Kimataifa. hayo yakiwa yametimia. Hatuoni tabu kuondoa mkanda ili watu wapite, lakini ikiwa hayo hayakutimia, tutalazimika tuendelee kuweka mkanda kuzuia ili uwanja wetu kama tunavyotaka kuitwa *International*, maana yake ni lazima tuendane na vigezo na maelekezo ya kikanda na maelekezo ya Kimataifa.

Mhe. Mwenyekiti, suala la tatu, limeuliziwa suala la kwa kiasi gani kwamba watu wanasumbuka wanapotaka kushuka. Suala la kwanza, ilikuwa ni vibao ambalo yeye mwenyewe Mhe. Mjumbe, amekiri kwamba vibao vimeondoka, tumemshukuru. Suala la pili, ni kwamba watu wanasumbuka, wananyanyaswa na wanadhalilishwa. Hili naomba tulichukue. Tutalichukua na kuona kwamba kama taratibu ambazo tumezielekeza Mhe. Waziri, amesema tulifanya kikao cha bodi cha dharura siku ya Jumamosi, Afisi ya kwake Mhe. Waziri kwa kukutana na bodi ili kuzungumza haya. Kama hilo halijachukuliwa ni lazima tuone kwa kiasi gani na sababu iliyofanya hayo yasichukuliwe, lakini sisi kama serikali hatuoni sababu yoyote ya kumsumbua mtu ambaye anataka kusafiri. Utaona kwamba mtu anayetaka kusafiri na anaingia nchini, anapata huduma zetu nzuri kama vile ambavyo tumekusudia kwamba mtu aje Zanzibar kwa kuona kwamba Zanzibar ni njema atakaye aje.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, usumbufu huo wanaoupata wananchi ama wakati wa kuondoka ama wakati wa kuja, tutaona sisi kama wizara tunakaa na wenzetu wa mamlaka ili tuone kuna sababu ipi ya msingi inayosababisha hili.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu ya kijana mwenzangu ya kati na kati, jina la mwanzo kama alivyojibu kuhusu Forodha mchanga. Afisi ya Mkuu wa Mkoa iliagiza panapo dharura wanaruhusu chombo kwenda, lakini watendaji wake wa mamlaka wa bandari hawakubali. Walikitunga kitabu hicho na ukitaka nitakuleta, patakapokuwa na dharura pataruhusiwa na dharura ipo wakati mwengine. Maji hayajai Mhe. Naibu Waziri, patakapokuwa na dharura pataruhusiwa kwenda, lakini watendaji wako wanakwambia mimi ninaogopa Mkuu wa Mkoa. Sasa wananchi wateseke. Haya si maneno yangu, ni maneno ya Kamati ya Mkuu wa Mkoa, patakapotokea dharura na tumeshuhudia juzi meli ya kasa imekaa siku nne. Katiba ya Zanzibar inatukataza.

Mhe. Mwenyekiti, la pili, maagizo munayotoa hapa watendaji wenu wakurugenzi wa Uwanja wa ndege hawafuati. Hapo tunahangaika kutuma maswali mmoja ni mmoja, wa pili ni Mhe. Saleh Nassor Juma, mimi ninakesha. Sasa jitihadi zangu kwa serikali haina maana ya kuleta maswali hapa. Mimi nihangaike nipoteze nguvu zangu, halafu mtu anakuja kujibu anavyotaka kujibu, hatuwezi kwenda.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Mkurugenzi yupo tutekelezeni wajibu wetu na tuwatumikie wananchi, mimi ninatumia wananchi kwa upande wangu na Naibu Waziri tumikia wananchi kwa upande wako, wape kauli nzuri, kauli nzuri ni sadaka. Watu wanateseka. Hili halitaki kukaa na bodi, kukaa na nani, ni kutoa amri tu ya serikali, hakuna sababu. Unashuka pale na gari yako, abiria unampeleka, sio mpaka mukakae siku tatu, maamuzi yatoke sasa hivi ndani ya chombo cha wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, suala la mkanda, ule mkanda wa kuingia abiria mwanzo hauna tatizo, upo mbele yake mtu, ule upo pembeni umezungushwa huku, ni usumbufu. Hoja hizi ni za wananchi, si zangu mimi Jaku Hashim Ayoub. Mimi sikupata jimbo kutoka Ikulu, wala viti maalum, nimekuja kwa wananchi humu ndani. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Hebu Mhe. Asha Bakari Makame subiri kidogo. Mhe. Jaku Hashim Ayoub sijakufahamu ume...

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka anijibu Waziri au Naibu Waziri, bado hoja yangu hawajaifahamu. Kamati ya Mkuu wa Mkoa imeridhia kwamba eneo lile pakawa na dharura panatumika na uchungu wa mama aujuaye mzazi. Mimi nina wananchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, kama nitakuwa nimemfahamu vizuri Mhe. Jaku Hashim Ayoub, anachokisema kwamba anakiri kwamba eneo lile limezuiwa na bila shaka maelezo yake hana pingamizi na hili, lakini anachokisema kwamba amesikia taarifa kwa Afisi ya Mkuu wa Mkoa kwamba penye dharura panaruhusiwa, hili hatuna tatizo nalo, lakini tunachokiamini. Utaratibu wa ufanyaji kazi katika taasisi za serikali kama kutakuwa na hiyo dharura, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa itawasiliana na Idara ya Bandari.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, hebu tuwe watulivu tusikie vizuri, naona kuna mazungumzo mengine ambayo yanaingiliana.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, kama kutakuwa na dharura inayolazimisha kwamba meli ikafunge pale, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ambayo ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, atawasiliano na mtendaji wetu mkuu wa bandari, baada ya kuwasiliana na mtendaji wetu mkuu

wa bandari, mtendaji mkuu atawaelekeza wasaidizi wake kuweza kuruhusu, lakini kama kutakuwa kuna dharura, akitoka mtu binafsi kwenda kuzungumza katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, bila ya Shirika letu la Bandari kuzungumza baina ya chombo cha dola na chombo cha dola, kwa maana ya serikali na serikali, basi haiwezi kuchukuliwa hatua, kwa sababu kutakuwa na hofu ama kutokuaminiana.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, kama taarifa hizo ni za kweli kwamba Mkuu wa Mkoa amesema kwenye dharura ataruhusu, basi awasiliane tu, akiwasiliana na Mkurugenzi Mkuu, Mkurugenzi Mkuu ata-*delegate* kwa watu wake na watakwenda kusimamia na huduma hiyo inayotakiwa itatolewa, kwa kutambua kwamba dharura maalum imeruhusiwa na kwa kutambua kwamba Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, ndiyo Mwenyekiti wa Kamati za Ulinzi na Usalama katika mkoa wetu. Kwa hivyo, kama iko hivyo, sisi hatuna tatizo. Msingi ni kuona vyombo hivi viwili vinawasiliana katika kuona kwamba malengo yaliyokusudiwa ya ulinzi, malengo yaliyokusudiwa ya kulinda Mji Mkongwe na malengo ya kutoa huduma yetu sote tunafanya kwa pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, suala la pili, alizungumzia suala la huduma ya Uwanja wa ndege. Nimthibitishe tu Mhe. Mjumbe, kwamba sisi hatuna kikwazo na kuimarisha huduma zetu na ndicho tulichosema kwamba kama kuna kikwazo, basi kikwazo hicho kiondoke, ili tuweze kuona watu wetu wanapata huduma vizuri, lakini kama kuna maelekezo ya taratibu za Uwanja wa ndege iwe za ndani, iwe za kanda au za Kimataifa na sisi tutalazimika kuzifuata. Kwa hivyo, ni lazima tukae tujadili ili tuone vikwazo hivi vinatokanana nini, taratibu za ndani, taratibu za kikanda au taratibu za Kimataifa.

Mhe. Mwenyekiti, maana vyenginevyo tunaweza tukaamua kitu baadae tukaja tukajuta na maamuzi yetu, kwa kuona uwanja wetu na baada ya kuwa na malengo ya kutaka kuendelea mbele, tunarudi nyuma, ni lazima tukae tuona na ndio maana nikasema kama tatizo la watu kushindwa kupata huduma kwa sababu ya mkanda, hakuna kipingamizi cha taratibu za uendeshaji wa uwanja kwa mujibu wa sheria za ndani, sheria za kikanda na sheria za Kimataifa, basi hili liondoke kama kuna kikwazo basi wenzetu watatueleza, lakini kama msingi wa hayo hayapo hatuoni tatizo watu kupata huduma. Nakushukuru.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, lakini narudia tena kwa lugha nyepesi na laini kabisa. Mkanda ule wa kuingilia na kutokea hauna tofauti, lakini kwa nini wafanyakazi ule ule wautumie na mimi naona kwa macho yangu kule, watu wakazungushiwe nyuma au wale hawana haki. Wengine watumie na wengine wasitumie, kwa sababu gani inatia uchungu na tofauti wa kuingia mbali na wa kutokea mbali na huingii ndani mule mpaka uulizwa, kwa sababu gani tusogee kule, hakuna vurumai, tunalipotosha Baraza.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Naibu Waziri, mimi nikuombe tena, kaa na watendaji wako kwa heshima ya hali ya juu, lakini pale hakuna sababu ya msingi ya kufunga, hata mtaalamu utakayempeleka. Suala la pili, wagonjwa bado wanateseka kupelekwa pale kama amri imeshatoka, basi ithibitishwe amri ile. Mtendaji Mkuu yupo wa Uwanja wa ndege atatuthibitishia tu, atakileta ki-*note*. Kwa hivyo, suala atalisimamia ndio majukumu yake.

Mhe. Mwenyekiti: Hoja ile ya kwanza nadhani haina matatizo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ile hoja ya mwanzo haina matatizo, tatizo ni kwenye hoja zangu mbili hizi tu, ilo la mwanzo atajua jinsi ya kufanya.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, nadhani hilo suala la Uwanja wa ndege, mimi namuheshimu sana kiongozi wangu mkuu wa serikali Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, alitoa kauli kwamba yeye mwenyewe binafsi analichukua suala la Uwanja wa ndege. Sisi kama wizara tutashirikiana naye kikamilifu ili kuona kwamba linafikia pahala pazuri, yeye ndiye atakayetuongoza tafanye nini na nini kwa sababu keshalibeba yeye. Kwa hivyo, mimi na Naibu Waziri wangu hapa na watendaji sote tutakuwa china ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais mpaka hili suala likae sawa na yeye ndiye atakayetuambia, sasa ni sawa, hili tufanye hivi. Kwa hivyo, suala hilo tunalihakikishia kwamba sababu limebebwa na serikali na sisi tuko chini ya serikali, sio dogo tena, ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hivyo, Mhe. Jaku Hashim Ayoub, litasimamiwa kama ilivyoahidiwa na serikali.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, yeye keshatoa kauli mwanzo, kuwa keshaagiza. Kwa hivyo, bodi ifuate maagizo yake, sasa tena kurejesha tena kule haya maagizo sio kama tunajizonga, yeye keshatoa maagizo

kama waziri bodi ifuate maagizo yake, kwa nini bodi haifuati na watu tunajizonga. Hii sio mara ya kwanza Makamu wa Pili kumtupia mizigo, kila mzigo tutamtupia Makamu wa Pili.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, kwa ujumla litasimamiwa hili suala. Kwa hivyo, tuiwachie serikali isimamie kama ulivyoomba. Mhe. Asha Bakari Makame. Aaah! Samahani. Mhe. Hija Hassan Hija nilitangulia kumwita. Wewe kaa kwanza, Mhe. Hija ndiye nilitangulia kumwita.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana na niendelee kukupongeza kwa jinsi unavyotuendesha vizuri, Mwenyezi Mungu akupe afya na uwezo zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, nilipochangia kwenye hotuba hii ya Mhe. Waziri, nililalamikia jinsi utendaji ambao hauridhishi na hapa tuko kwenye fungu la mshahara wa Mhe. Waziri, na nikatoa hoja kwamba kwenye kitabu chake katika ukurasa wa 25 kifungu cha 56, aliwaambia wananchi wa Zanzibar, kwamba barabara ya Mgagadu-Kiwani imejengwa na imekamilika kwa kifusi tabaka mbali mbali. Ili barabara ikamilike, kuna hatua nyingi za kupitia.

Mhe. Mwenyekiti, hatua ya kwanza ni kuweka *subgrade*, hatua ya pili, ni kuweka *subbase* ambayo hii ni nchi 6 mpaka 8, hatua ya tatu, ni kuweka *base*, kwa maana ya nchi 6 mpaka 8 na hatua ya mwisho, ni kuweka lami. Barabara ya Mgagadu-Kiwani ambayo Mhe. Waziri, ameiandika humu na wananchi wameinukuu haijafanyiwa hatua hizo, maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba akisema kuwa imefanyiwa tabaka mbali mbali, maana yake ni kuwa mwakani wakipata fedha watakwenda kuweka lami juu ya mgongo ambao haukutimia kitaalamu.

Mhe. Mwenyekiti, sasa Mhe. Waziri, hapa ndipo penye utendaji ambao mimi nililalamikia kuwa ni utendaji ambao hauridhishi. Ningependa atuwekee sawa na wala sina haja ya kumnyanyua Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, mambo mengine ni *size* yake. Atuwekee sawa ili niweze kuridhika kwa maana kuwa alikusudia kutuambia nini, wakati barabara ile imewekwa kifusi cha mwanzo na sio kifusi tabaka mbali mbali.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nashukuru sana kwa Mhe. Hija Hassan Hija, kwa kuikazania sana barabara yake ya Mgagadu-Kiwani, kwa sababu ni haki yake na ndio jimbo ambalo lililomchagua, lakini barabara hii anaijua yeye fedha iliyojengewa, ilikuwa ikitajwa kila mara katika bajeti hii ya serikali. Barabara hizi zinazojengwa kwa fedha ya serikali zinajengwa katika utaalamu ambao sio ule unaojengwa na barabara za Kampuni, kutokana na makisio yake ya fedha, sote tunatiliwa fusi la aina hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mwenyewe binafsi nina barabara inayotoka Wesha kuelekea Mkunguu, imetiwa fusi la aina hiyo hiyo ambayo imetiwa kule, kwa sababu inajengwa na mfuko wa serikali. Kwa hivyo, namuhakikishia kwamba umadhubuti uliomo katika utiaji wa fusi huo umeshapimwa na wataalamu, lakini haizuwii wakati wa kutia lami kwamba ndio limeshamalizwa lile. Naamini kwa asilimia 100 kwamba kabla ya kutia lami, kuna fusi jengine ambalo litaletwa litiwe katika barabara hiyo, hilo ndilo naamini mimi, ila lilipotajwa katika *layer* mbali mbali, aseme kwamba barabara ile haikushindiliwa, ndio maana zikawa *layer* mbali mbali. Ukishashindilia halafu ukatia tena fusi jengine ukashindilia ni *layer* ya pili, hiyo sio *layer* ile ile.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, tunamuhakikishia Mhe. Mjumbe, kwamba ile barabara ni madhubuti, sisi tumekwenda na tumepita. Barabara ya fusi ikiwa haijatiwa lami, basi hailingani na barabara ya lami, lakini tunaamini kabisa na tunamuhakikishia Mhe. Mjumbe, kwamba hata hapo itakapokuja kuwa sasa itiwe lami, basi haitotiwa lami juu ya kile kifusi ambacho ni kile kile kilichotiwa, ni lazima itarejeshewa fusi la juu na lina utaratibu wake wa kulishindilia na kulimwagia maji kabla hujatia lami. Sasa ku-*predict* kitu ambacho hakijatokea, si dhani kama kaifanyia haki wizara. Namuomba sana aichukulie, labda Mhe. Naibu Waziri aongeze.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, ukiona watu wanaimba, halafu wanang'ong'ona, hiyo nyimbo kidogo ilikufa betri.

Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwamba Mhe. Waziri, amekiri kwamba ile barabara haikushindiliwa. Hoja yangu ni kuwa amewaambia wananchi wa Zanzibar, bila shaka hata Taifa zima limeambiwa hivyo, kwamba barabara ile imetiwa kifusi tabaka mbali mbali. Tabaka mbali mbali, maana yake ni *three layer*, ndio mwisho wake inakuja lami. Ile barabara nashukuru kuwa amethibitisha kuwa haikushindiliwa, lakini imetiwa kifusi ambacho hakizidi hata inchi tatu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ni mtu, kwani na yeye labda kama kaenda kutembea tu labda kwa harusi, lakini mimi ndiye mtu wa Kiwani. Hivi sasa barabara ile haipitiki kwa sababu hii mvua iliyonyesha juzi iliathiri barabara ile kwa sababu haikutiwa kifusi hicho. Hoja yangu kwanza abadilishe ile kauli hapa sio *layer* mbali mbali, ili mwakani wakija wakipata fedha wasije kutufanyia ule ujanja, maana yake ukisema tabaka mbali mbali, maana yake sasa hivi imebakia tabaka ya kutia lami, mwakani wasije wakafanya ujanja ule ule wanaoufanya mara zote kule ofisini Pemba, wakatuzimia tukala hasara. Pili, nimwambie kwamba hoja ya kuwa hakuna fedha, ndio wakatudanganya kuwa tabaka mbali mbali, si wangesema tu kwamba hatujapata fedha.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru kwa kuwa na hadhari sana katika barabara ile, lakini namuhakikishia kwamba lami ni ghali sana na hata ukiitisha *tender* ya lami kwenda kuiweka pahali, huwa umeshajidhatiti kwamba mimi ninacho kitu cha kuweka lami. Kwa hivyo, hilo halitotokea kwamba mseme sisi Mgagadu-Kiwani tunataka kuitia lami tutaiwacha vile vile, lakini pia, hapa tabaka mbali mbali imekusudiwa kwamba ule ujenzi wenyewe wa ile barabara kuna sehemu zimetiwa fusi zaidi na kuna sehemu za mwisho mwisho zina fusi kidogo zaidi. Kwa hivyo, halijakuwa sare lile fusi ambalo limewekwa pale, ndio maana ya ile kuwekwa kwamba ni tabaka mbali mbali. Nyengine zimetimia *layers* mbili au tatu na nyengine bado kutokana na hali ya fedha iliyopatikana, lakini hatuwezi, pamoja na yote, lakini wataalamu tunao wa kuweza kufanya yote. Kwa hivyo, sidhani kama itatokezea kama hivyo ambavyo anafikiria yeye, kuwa itatiwa lami, halafu ije inyofoke kama ile ya mwanzo iliyotiwa, ahsante.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, mimi najua uwezo wa kutia lami hawana, wala sizungumzii lami, nazungumzia maandishi aliyoyaandika, kwa sababu haya ni kumbukumbu kubwa sana kwa Taifa. Sasa kumbe nimemfahamu kuwa wametia kifusi sehemu mbali mbali, nimemfahamu sasa. Ugomvi wangu ulikuwa ni tabaka mbali mbali, kwa maana ya *three layers*, sasa kumbe wametia kifusi na ndio uhalisia wenyewe, wametia kifusi pale wanapoona huyo Mwakilishi hatosema, kwa sababu kule kulikuwa kuna mbio za Mwenge, labda hawa watu wa Mwenge wataona bado *network*. Nimemfahamu kwamba wametia kifusi sehemu mbali mbali ili kuwaziba watu macho.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hoja yangu ni kwamba kwenye fungu la fedha nitakwenda kwenye ule mradi wa Kiwani, nitaongea baadae huko mbele, lakini namtahadharisha Mhe. Waziri, awe makini sana na utendaji wa wizara yake chini ya fungu hili. Haya makelele ya Wawakilishi, sio kwamba wanamchukia Mhe. Waziri, wengi hawana kitu tumewaachia tu, lakini ile *business as usual*, hapa ndio nyumbani kwao. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, kwa kuweka kumbukumbu vizuri tu ni kwamba Wawakilishi wenzangu muelewe kuwa barabara hii chini ya Mhe. Rashid Seif imetiwa kifusi sehemu mbali mbali. Tuendelee. *(Makofi)*

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, namsikitikia sana Mhe. Mjumbe, kwa kulia wivu wa kimaendeleo, simlaumu, lakini nitazungumzia kuhusu habari ya *Sealink* ya mzaliwa wetu wa hapa Zanzibar ndugu Bakharesa.

Mhe. Mwenyekiti, waziri alipokuja kutoa hotuba yake alituonesha kitabu hichi, ndio kinasema na hii ndio sheria, hasemi ni kitu gani kinasema ndani ya hicho kitabu,hukikamata na kusema kwamba hiki ndio kinazungumzia sheria. Sasa mimi namuuliza Mhe. Waziri, na nasema tena kwamba waziri kwa kweli huwajibiki ipasavyo katika kazi zako, ungekuwa unawajibika, basi ungetuambia kile kitabu kinasema nini na ni sheria ambayo unayo wewe mwenyewe. Kwa hivyo, mimi nasema hivi, kwa kweli mimi namtaka radhi sana ndugu Bakharesa, kwa nini nikasema hivyo, kwa sababu tunamtia kwenye maafa ambayo yeye sio aliyefanya matatizo, ni wizara husika ndio inamfanya aonekane Bakharesa, ndio anayefanya makosa. Sio Bakharesa na nawaomba Waheshimiwa Wajumbe, wenzangu jamani huyu mtu ametusaidia mambo mengi hapa na ni mzawa. Kwa hivyo, tusifanya mambo tukamvunja moyo.

Mhe. Mwenyekiti, nitazungumza kama yeye waziri, hajui mimi nitajibu kidogo. Hii *Sealink* huko Ulaya ilikotoka ina *Certificate* yake ya kuchukua abiria 1,500, ndio kile kitabu alichokuwa anakizungusha tu mkononi, lakini waziri hakulisoma. Wakati wa baridi huko wenyewe walikuwa wanachukua watu 300 au 200, wakati wa joto ndio watu 300 na gari. Ilipokuja hapa ndio ikaambiwa ichukuwe watu 700, ilipochukua idadi hiyo walikaa awamu kisha wakaongezwa, baada ya kuongezwa tena awamu ya tatu wakafika watu 1,400. Sasa Mhe. Waziri, hakutueleza haya, tumamtia makosani matu ambaye kwa kweli anatugharamikia sisi, kututafutia vifaa ambavyo sisi hatuna uwezo navyo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi namuomba sana Mhe. Waziri, uwajibike ukae usome mkataba na sheria na pia utembee katika wizara yako, haya tunayokueleza hata huko kwenye hiyo sehemu hukujui, basi utembee, wewe ndio muajibikaji kwenye hili Baraza la Wawakilishi, hatokei Katibu Mkuu kule au Mkurugenzi akaja akajibu hapa. Kwa hivyo, mimi nataka aje atowe maelezo ambayo ya kina kuhusu habari ya hii *Sea Link*, tusimtie mtu hatiyani ambaye anatusaidia tukamvunja moyo, huyu ni muwekezaji ambaye anasaidia sana katika nchi yetu maelezo nataka.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru nipokuwa nikitoa majumuisho yangu, nilisema kwamba hili suala hili lilianza katika suala la ndani ya Baraza na nikajibu, liliulizwa suala la nyongeza kuhusiana na uwezo na nikasema hivyo inavyotajwa sivyo, kwa sababu sisi tunao ushahidi wa *document* kamili na nitakuletea kwa maandishi na nilipokuwa nikitoa majumuisho yangu nilikwambia kwamba jana hiyo hiyo nilipata barua kutoka Baraza la Wawakilishi kutaka hayo maelezo ya jibu la nyongeza na sisi tulikuwa tumeshatayarisha mpaka barua ya katibu, kwamba haya ndio maelezo ya ziada na kitabu hichi tulikabidhi Baraza la Wawakilishi na nilipokuwa nikitoa maelezo vile vile mlisema maelezo ya moja kwa moja idadi ya abiria wanaotakiwa kuingia yamo katika ukurasa wa 18 na 19, usipate tabu katika kitabu hichi kwenda wapi. Ukifika ukurasa wa 18 na 19, maelezo kamili yapo, nashukuru wamenifahamu.

Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mhe. Asha Bakari Makame, kwamba kajua kwamba hilo lililokuwa likizungumzwa silo na nilisema kwamba wale waliofanya vile, basi ilikuwa ni kupitikiwa *information* ambazo hazikuwa sahihi walizokuwa nazo. Kwa hivyo, tumuombe radhi yule muwekezaji wetu mzee wetu ili tuweze kuendelea mbele, ndio nikakwambia kwamba baadhi ya mambo ambayo tunazungumza huku ndani ya baraza, tuwe na uhakika nayo, tusije tukawaingiza watu wengine katika hatiya au katika midomo ambayo hawapo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, hilo ndilo ambalo nimelizungumza kwamba kile chombo kwa mujibu wa *stability book* hii ambayo ipo *ZMA* ni abiria 1500, kulikuwa na maelezo kwamba imerekebishwa sheria yetu tuliyoirekebisha hapa, inasema kwamba marekebisho yaliyofanywa ni ya kuongeza urefu, upana na kina, ndiyo yaliyokatazwa. Kwa hivyo, nikasema kwamba ile ilivyofanywa marekebisho ni kujazwa viti mle ndani *internal design* na *Internal Design* haikatazwi *for longest* ile *turn-age* inabakia ile ile na hapa nitaisoma ile sheria tuliyopitisha wenyewe hapa ya marekebisho.

Kifungu cha 17(a) Nam. 3 kinaeleza hivi:-

" *No ship shall be registered in Zanzibar or license for the purpose of caring passengers in Zanzibar if such ship has been modified from its original construction"*. Imetajwa hasa hapa. Halafu limeelezwa zaidi "*For the purpose of this section, modification shall mean any modification to the ship*
structure from alteration of the main dimension such as length,breadth or depth". Hapa ndio yaliyotajwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, hakukuwa na kwamba sisi kama wizara hatukulijibu hili suala, tulilijibu, lakini halikufahamika, vyengine ilikuwa ni hamasa au jazba, lakini tulilijibu vizuri na tunamshukuru sana Mzee wetu Said Salim Bakharesa kwa kutuvumilia hili ambalo lilitokezea na katufahamu kwamba tumeweza ku-*defend* kile kitu ambacho kipo, hayo ndio maelezo na namshukuru Mhe. Asha Bakari, kusema kwamba tutoe maelezo, yenyewe ni hayo hakuna mtu aliyediriki kuweza kufanya kinyume na ile sheria ambazo tumezipitisha hapa za ubora na ukubwa wa vyombo vya vinavyochukua abiria.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, mimi nisingetaka maelezo mengine, lakini sasa ameeleza maana alitukamatia hichi kitabu, wenzangu shahidi humu, hili ndio linasema angeeleza mwanzo hayo, mimi nisingehoji na hapa Wajumbe walikuwa wakali kwamba wanataka kuuliwa watu, umesikia Mwenyekiti, wewe ulipokuwa kwenye kiti chako cha Uspika pale, kunataka kuuliwa watu, watu wanaongezwa hata na mimi nilisema ni kweli, lakini nilipokwenda nikautafuta ukweli, ukweli ndio huu, mimi sina matatizo, lakini namuomba tena Mhe. Waziri, akae apitie mambo yake.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho, kisha tutaendelea namuomba sana Mhe. Jaku, atake radhi sana kusema kwamba yeye kaja hapa kachaguliwa na wananchi, hakuchaguliwa viti maalum, wala kwa Mhe. Rais, sote sisi tunakwenda kwa Katiba hii, Mhe. Rais ana uwezo kwa mujibu wa Katiba ana watu wake kumi na sisi tumeingizwa kwenye Katiba akina mama na mimi nawataka radhi akina mama wa Jimbo la Muyuni waliomchagua Mwakilishi huyo, kwa sababu

kama si wanawake wote hawa, kama sio kura za wanawake, asingepita. Kwa hivyo, atuheshimu na tuheshimike, yeye kachaguliwa kwenye Jimbo, sisi tumechaguliwa kimkoa, mimi nimechaguliwa Tanzania nzima.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, atutake radhi Mhe. Jaku hapa.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Haya ujumbe umefika, tusikilize hoja ya mwisho.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, muungwana hanuni akaonyesha na mimi sikununa, nina wajibu wangu, lakini ninalosema tuwe wakweli katika kujibu hoja, suala la *Sealink* mimi tusidanganyene kama mtu mnampenda mpendeni tu, tusidanganye sheria, hii hapa *document*, mtandao huu kutoka nchi za nje, mwaka jana nilileta mpaka picha, hata meli haijaja hapa, ukisema umeongeza viti, ina maana tayari umeengeza watu, jamani tuambiwe kila siku tunaua tusiseme maneno ya uongo, kitu cha uongo tusiseme, tuseme ukweli, sheria mmeikiuka na wajibu wenu mjiuzulu, sheria mmeikiuka ukweli tuseme, hii hapa inasema; "*seven hundred people passengers*, hii hapa inasema, mimi sisemi uongo, hii hapa nimeichukulia *document*, twendani kwenye mtandao ipo tusifiche kitu, tusemeni kweli, tunamsaidia huyu mpenzi wetu, huyu muwekezaji wetu hili tukubali, kwa nini tukatae.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, hebu isome hiyo sheria.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, niisome sheria ipi, hii *manifesto?* Mimi sina sheria, hii hapa sheria, ipi unayosema wewe? Mimi sijafahamu, hii nimekwambia *manifesto* yenyewe inaeleza jinsi gani hiyo meli ukubwa wake na mambo yake, sikukwambia kama hii sheria, nataka unielewe hivyo, ionyeshe kiasi gani hiyo *capacity* inavyoeleza humo na sheria imesema ukiengeza maumbile, tumetunga wenyewe hapa au mmesahau leo, hatutotoa leseni yoyote kama tuta-*change* maumbile na ndio maana M.V. *Skagit* iliyoua hivi karibuni, iliongezwa maumbile na ndio sheria hiyo tukaleta hapa, tumeleta hapa mswada, mmesahau leo hii tukasema huwezi kupewa leseni yoyote na *Hansards* zipo, lakini sema kwa kuwa mmeanza kunichanganya mapema tu.

Mhe. Mwenyekiti, *Hansards* zipo, nimenukuu hizi hapa, naweza nikasoma, nisikilize sasa naanza kukusomea *Hansard* wanaeleza vipi; "hakuna meli itakayosajiliwa au kupewa leseni kwa madhumuni ya kuchukua abiria ndani ya Zanzibar ikiwa meli hiyo imebadilishwa kutokana na hali asiliya utengenezaji wake" Nasema sheria gani tumesema, si ndo hii sheria, ipi nyie angalieni lakini mimi ndio nasema hapa.

Mhe. Mwenyekiti, unaona ulivyokuwa hunipendi, wangekuwa wengine ungelikuwa umeshasema nyamazeni Wajumbe, mumsikilize Mjumbe, mimi nasema unawaachia watu wanasema kule, wanani-*interfere* katika mazungumzo yangu, mimi niseme bora niachilie iendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Maelezo zaidi Mhe. Mshimba, vipi!

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, ikiwa mimi naongea, unawaachia watu wanaongea huko, ingekuwa wengine ilivyokuwa mimi hunipendi, wengine ungekuwa umeshasema msikilizeni Mjumbe anavyoeleza, lakini wewe unashughulikia makaratasi, wale wanaongea, sasa niseme nini mimi? Hili jambo mnasema hamlitaki, sasa mimi naondoka huko twende kwengine.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mshimba, hebu sikiliza kaa kitako, Waheshimiwa Wajumbe, hii karatasi niliyokuwa nasoma ndio karatasi aliyoleta mwenyewe, sasa nilikuwa nathibitisha hayo uliyokuwa unayasema, kopi ameleta huku, vyenginevyo usingeleta hii kopi, umeleta kwa Mwenyekiti ili niitizame sasa tatizo liko wapi hapo, sasa kama umeridhika na majibu yaliyotoka tuendelee, kama hoja bado unayo endelea.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, leo unanipa maajabu makubwa, wakati gani nimeleta kopi kwako, mimi sijaleta, nimeonyesha, la kama ina miujiza imekuja kwako *automatic Inshaallah*, ndio nina miujiza leo hii, mimi sikuleta ila nimeeleza tu, nimempa nani hii? Haya leo maajabu makubwa, nimempa nani mimi?

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, hoja unayo huna.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee na hoja nyengine, hiyo nimegundua leo haitakiwi, ishafukiziwa, sasa twende kwengine. Nilipokuwa nikichangia suala la Uwanja wa ndege hapa Zanzibar,

nilisema suala la gari yale mabasi kuwa ni mabasi ya pikiniki, kwa bahati nzuri nikasema kama utani mwisho, basi kama hakuna mabasi tulete japo, punda apelekwa kule, lakini kwa bahati nzuri sikupata maelezo mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba hili Mhe. Waziri, kupitia kwako anijibu vizuri ili niridhike tuondoe hilo, lakini jengine mimi nimeshituka kuhusu habari ya Uwanja wa ndege wa Pemba nilisema niruhusiwe nilete mishumaa ipo nje, niruhusu niweke kutokana na zile taa, lakini kutokana na jibu nikapata jengine nikashituka kabla sijapata jibu zuri, hata lile jina la mwenyewe hayati Baba yetu Abeid Amani Karume ambae kiwanja kile aliyekijenga, naambiwa sasa linaondosha na linaandikwa Pemba *Airport,* kidogo ningeomba na maelezo haya. Ama leo umenipiga chuma kweli! Ahsante sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nisingesimama, lakini sasa naona maji yanazidi unga, hiki chombo ni kukubwa sana na hadhi yake na haiba yake mbele ya wananchi, itategemea sisi namna tunavyo-*behave* humu ndani na namna tunavyojiheshimu huko nje.

Mhe. Mwenyekiti, nimesimama kutilia mkazo Kanuni ya sita inayozungumzia mamlaka ya Spika na kama alivyozungumza Mwanasheria Mkuu, Spika anaweza kuwepo juu, anaweza kukalia kiti cha Mwenyekiti, ni hadhi inabadilika, lakini mamlaka yake yapo pale pale. Naomba sana usifikishe pahala chombo hiki, mimi ni mmoja kati ya Wajumbe wakali sana, lakini mimi nakiheshimu sana hiki kiti, nikiambiwa nikae huwa nakaa hapa, pamoja na ukali wangu wote, kwa sababu tunaheshimu taratibu za humu ndani, chombo hichi kina nidhamu zake, mara nyingi Mhe.Mwanasheria Mkuu anatwambia tungeweza kujadili hapo hilo rungu likawa wazi, lakini umewekwa utaratibu kwamba tukijadili Kamati rungu linafunikwa kitaratibu zilizowekwa zinafuatwa dunia nzima, kama sisi wenyewe Wajumbe hatukiheshimu chombo hichi, chombo hichi kitapoteza hadhi yake kwetu na kwa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, nakuomba sana katika hili usiwe kabisa ukatuachia, tunaweza kuzungumza mamlaka yetu, tunaweza kuzungumza kwa hisia kali, lakini ikifika hadhi na haiba ya chombo hichi na mamlaka ya kiti, naomba uwepo makini sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Ismail Jussa Ladhu, nakushukuru kutukumbusha namna tunavyotakiwa tuwe, tunaweka nidhamu na kuheshimu chombo chetu, sasa nashukuru kwa hilo na nafikiri Mhe. Makame Mshimba, pamoja na Waheshimiwa wengine wote tutafuata maelekezo na yale ambayo umetukumbusha, kwa sababu tunayajua, lakini ni kukumbushana tu. Sasa Mhe. Mshimba, hoja moja ameiachia, hoja ya pili, kuhusu utaratibu wa kuwasafirisha abiria pale kwa ile baa, hili tunahitaji maelezo, hoja ya tatu, nadhani isingekuwa hoja kubwa ya jina la Uwanja wa Pemba, ni kweli ilikuwa Karume *Airport*, lakini imebadilishwa, ila sasa lile jina la Karume lije hapa kwa sababu ya kupewa hadhi ya kiwanja ili kiwe cha Kimaaifa na ile imejibiwa muda mrefu huko nyuma, isiwe hoja hapa tena, tujibu hoja hii ya kuhusu utaratibu wa kuwasafirisha abiria.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi, ni kweli kama maelezo aliyoyatoa Mhe. Mshimba, kwamba wakati wa kuchangia aliwahi kufanya maskhara kusema kwamba tuna mabasi ya kuendea pikiniki, lakini kwa nini tuna mabasi hayo, sote tunatambua haja na hoja ya kufanya mabadiliko katika Uwanja wa ndege kwa sekta ya miundombinu na Mawasiliano, popote tukipita tunaona mabadiliko yaliyopo hivi sasa kwamba kuna ujenzi wa *Apron* na hapo *Apron* iliyopo sasa imeshakuwa kongwe, inahitaji kutengenezwa na kuwa na nguvu za kuweza kuhimili kukaa ndege mpya, kwa msingi huo tutalazimika wasafiri tutoke katika jengo letu tulilopo hivi sasa kwenda upande wa kusini kwenye *Apron* mpya ili kuweza kutoa nafasi kwa *Apron* iliyopo hivi sasa katika *terminal* yetu iliyopo hivi sasa iweze kutengenezwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kutambua kwamba ni kipande kirefu mamlaka imejaribu kutafuta utaratibu wa kuweza kutoa huduma kwa wasafiri wetu na ni kweli kwamba tulilazimika kukodi mabasi ya kawaida ya kuchukua abiria 28 mpaka 30, ili kuweza kutoa huduma hiyo, kwa kutambua kwamba kiutaratibu tunatakiwa tuwe na mabasi makubwa, mabasi ambayo yana gharama kubwa, basi moja lenye muundo kama treni, gharama yake haipungui *Euro* laki mbili. Sasa kutokana na ngugu ya kifedha na muda uliokuwepo, wakaona kwamba muda wa kutafuta mabasi yale makubwa itakuwa ni mrefu, lakini la msingi viwanja vyote duniani wanalo jukumu la msingi la ku-*save* vyombo vya usafiri, ni wale *ground area*, kwa maana ya kwamba wanapokwenda Dar-es-salaam, utakuta mabasi wanayopanda abiria wanapokwenda kupanda ndege yameandikwa *Swister,* wale ndio wenye jukumu la msingi la kusafirisha abiria.

Mhe. Mwenyekiti, sasa mamlaka kwa kuona mazingira hayo na kwa kutambua kwamba tuna haja ya kufanya hivyo, wakakodi mabasi yale kwa muda, lakini jambo la faraja kwamba leo nimepata taarifa rasmi kwamba wamenunua mabasi mengine matatu makubwa ya kuweza kuchukua abiria 40 mpaka 60, baada ya kufanya marekebisho ndani, mabasi haya ni mapya *new brand* aina ya *TATA 909 Bus* na kila basi moja limegharimu shilingi milioni 76,130,000/= kwa ujumla wake ni milioni 228,390,000/=, lakini mabasi haya yamepata *Exertion,* maana yangelipewa malipo yote yangegharimu shilingi milioni 265. Kwa hiyo, kwa hatua ya awali wamenunua mabasi hayo matatu kwa ajili ya kuweza kutoa huduma kuwasafirisha watu kutoka kituo kilichopo sasa *terminal* kwenye *Apron* kwa ajili ya safari, lakini hoja yetu ya msingi inabaki pale pale, tuwaombe au tuwatake wenzetu wa *Grand Handler* wakae na mamlaka wazungumze na wakubaliane, ili waweze kuimarisha huduma hizi kwa kufuata taratibu, nyenzo pamoja na vifaa vya Kimataifa kama vile tunavyosema kwa uwanja wetu.

Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, kwa maelezo ya Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, lakini kuna kitu kimoja nataka kumuuliza kwamba kuna kitu kikiwa *new* kinaitwa "*new"* na kuna kitu kikiitwa *brand new* inakuwa ni "*brand new"*? Sasa hapa nataka kidogo anisaidie tafsiri yake ikoje, kwamba ikiwa *new* au *new brand* na hilo ni la kwanza.

Mhe. Mwenyekiti, pili Mhe. Naibu Waziri, amesema kuwa wahusika wenye mambo yale wanatakiwa wale watu ambao kwa hapa kwetu inatakiwa iwe ni *ZAT*, ndiye mhusika anayehusika na masuala kama yale. Je, Mhe. Naibu Waziri, hawa watu muliwahi kuwaita, yaani kiutaratibu mulikaa nao na kama hamkuwaita, hivi Mhe. Naibu Waziri, yuko tayari kukaa nao kwa ajili ya kuelekezana juu ya suala hili lilivyo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Naibu Waziri, tupe maelezo ya ziada inaonekana Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, anaelekea.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii, ni kweli kwamba mabasi haya tumesema mapya na tunaposema mapya, kwa maana ya *new brand*, yaani zero kilomita *per hour*, yaani ile *speed mitre* yake inaonesha hivyo, kwa maana hayajatumika. Kwa hivyo, yamekuja pale na safari yake ya kutumika ni kufika pale yalipo tu ni mapya na sio yale ya *second hand* yaliyonunuliwa Dubai na wala hayakutoka kwenye *Yard*. Kwa kweli ni mabasi mapya ambayo yameagizwa na mamlaka kwa mkopo kutoka *PBZ*.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ambalo ameuliza Mhe. Mjumbe, ni kwamba je, kama wizara muko tayari kukaa na hawa *Operators*, kwa maana ya *Grand Handler*. Sisi hatuna kikwazo na kama wizara au mamlaka hatuna tatizo na tunalazimika tusiwe na tatizo la kuzungumza na hawa, kwa sababu hawa ndio wabia wetu na tunapozungumza uimarishaji wa huduma za *Airport*, maana yake hawa ndio watoaji. Kwa hivyo, sisi kama serikali au wizara, ama mamlaka tukisema hatuelewani au hatufahamiani na hawa hatuwezi kupata huduma, maana hawa ndio *services delivers*, wao watoe *services* vizuri ili sisi tuweze kuijenga hiyo haiba na taaswira ya nchi yetu. Kwa maana hiyo, sisi hatuna tatizo na hata ikiwa kesho kutwa Jumatatu tuko tayari kukutana nao na kama kuna kasoro yoyote tuweze kuzungumza kwa msingi wa kutaka kujenga na kuendeleza umoja wetu, mshikamano wetu na kuimarisha huduma tunazozitoa katika uwanja wetu.

Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, kwa kweli Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, anasema haya mabasi ni mpya kabisa, kwa maana ya *brand new*, pengine ukisema *new brand* inaleta maneno kidogo tofauti kama vile ina mpya, lakini ni *brand new* kwamba ni mapya kabisa.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, ninakubaliana naye kutokana na alivyonieleza kwamba mabasi hayo ni mapya kwa kuwa mimi sijayaona ninakubaliana naye, kwa sababu sijayaona najua hawezi kunidanganya kwa sababu na mimi ninakuwa ninafuatilia na nitafuatilia, lakini nimalizie tu na kwamba naomba sana kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kutoa ushauri wangu wa bure bila ya malipo, hebu waitwe hawa *ZAT* wakae nao na kama kuna mikataba wafunge mikataba kwa nia nzuri tu, ili suala hili la hitilafu ya pale iweze kuondoka kwa nia nzuri tu, kwa sababu sidhani kama Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohamedali ataitwa na Kampuni yake waweze kukataa. Tuendelee. *(Makofi)*

Kifungu 0901	Idara ya Uendeshaji na Utumishi-	3,269,314,000
Kifungu 0902	Mamlaka ya Usafiri Baharini-	

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. Leo nilikuwa sitaki niseme sana kwa sababu ninayo hoja ndogo kuhusiana na hapa na zile za kilimo zote nilizosema za wakulima wangu ni kweli, ingawa nimeambiwa si kweli, lakini nije kwenye hii Mamlaka ya Usafiri Baharini.

Mhe. Mwenyekiti, usafiri wa bahari ni usafiri muhimu sana kwa nchi za visiwa na wala sio tu kwa ajili ya kutoa huduma hata kiuchumi, kwa sababu jana nilipokuwa nikichangia nilisema hivyo.Vile vile, nilisema kwamba *Virgin Butterfly* iliweza kuwaunganisha Wazanzibari na Watanga na Wamombasa kwa siku moja ilikuwa inatoka Dar-es-salaam, Unguja, Pemba na Mombasa na ikaweza kuwainua wajasiriamali wadogo wadogo, siku zile akina Bopari na kua wafanyabiashara wakubwa, lakini kile chombo kimeondoka miaka mingi sana.

Je, serikali ina mpango gani sasa wakuweza na wao inaonesha hawana uwezo wa kuleta chombo kama kile, hivi kuna mpango gani wa kuweza kuwahamasisha wawekezaji wakaweza kuleta chombo ambacho kingekuwa kama vile *Virgin Butterfly*, ili kuweza kutoa huduma kama ile kwa ajili ya kuinua uchumi wa mtu mmoja mmoja pamoja na Taifa kwa jumla. Hilo la kwanza.

Mhe. Mwenyekiti, jengine katika suala hili la usafiri baharini hichi ni chombo kikubwa sana, yaani hili Baraza letu na wala hili si jukwaa la kuwanadi wafanyabiashara wa mambo ya bahari humu ndali, lakini lazima tukubali kwamba wawekezaji wengine ni muhimu sana kama vile Said Salum Bakharesa ni mfanyabiashara makini na mahiri na wala sio tu katika kuwahudumia wananchi, kwa mfano sisi Wapemba kule Said Salum Bakharesa ametukomboa kwa kutuletea ile *Azam Sealink*. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sasa hoja yangu ipo hapa kwamba Said Salum Bakharesa alitaka kujenga gati kama aliyojenga hapa Unguja pamoja na kujenga mambo kama yale pale Wesha au Wete, jambo ambalo lingekuwa ni muhimu sana na sio kwa wafanyabiashara wadogo wadogo, lakini hata kutuunganisha na Mombasa kule kama ilivyokuwa zamani. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu ya pili, ni swali hili, je, Said Salum Bakharesa mfanyabiashara huyu anayependa kutusaidia sana Wazanzibari na hasa sisi kutoka kule Pemba kwa kweli kwa sababu bila ya *Azam Sealink* hapa ni tatizo.

Je, akapewa kule yale mahitaji, kwa sababu mcheza kwao hutunzwa na amecheza hapa sana Said Salum Bakharesa kutusaidia Wazanzibari na hili jambo analitaka muda mrefu sana, kwani alitaka sehemu ajenge Ofisi hajapewa, alitaka sehemu ajenge gati pale Wesha au Wete hajapewa, sasa na mcheza kwao hutunzwa, atapewa lini hizi sehemu ajenge, kwa ajili ya kuweza kutuunganisha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli namuomba sana Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, wamkubalie kwa sababu *Azam Sealink* ikifanya kazi hapa, mutakula maboga kutoka kwao Mhe. Hija Hassan Hija, Mwambe, ambapo yeye ndio alijenga hoja kwamba inazuiliwa isichukue abiria hapa, ni vyema ichukue abiria na iongeze. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu ukiangalia utaalamu wa kwamba ile uzito wake ni huu, ile meli inayo uwezo wa kuchukua gari 100 na kwa safari za Unguja na Pemba haichukui hata gari 10. Sasa kuongeza abiria ni uwezo wa kuchukua gari 50, si watu karibu 500 au 1000 hapa. Kwa maana hiyo, Said Salum Bakharesa aruhusiwe kuongeza watu kwenye *Azam Sealink*, ili watu wapate usafiri. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ninamalizia hoja yangu ya tatu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, subiri kwanza. Kwa kweli shida iliopo ni kwamba Mhe. Saleh Nassor Juma, huwa unachangia upya kwa ajili ya kutengeneza hoja, kwa bahati nzuri mimi ndiye niliyekuwepo kitini pale na nimesikia michango ilivyokuwa. Kwa hivyo, nilifikiri katika hili ulikuwa unataka kuulizia ile bahari ya kwamba je, serikali mtafanya mpango wowote kwa ajili ya kutayarisha usafiri kutoka Pemba-Tanga angau wiki mara moja, nakumbuka ulisema hivyo, sasa hiyo ndio hoja yako, lakini hili jipya. *(Makofi)*

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, mwisho kuitaka serikali nayo itusaidie ikiwa huyu Mheshimiwa ameamua kuzuia ile meli kwa mwezi huu wa Ramadhani, amsalie Mtume (*S.A.W*) asiizuie ile meli, kwa sababu watu wa Makunduchi watakosa kula majimbi kutoka Vitongoji, watu wa Mwera watakosa kula ndizi kutoka Wete, hivyo meli iendelee. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, mimi nasikitika kidogo kwamba hivi sasa tulikuwa tuweke sawa zile hoja zilizoulizwa hazikupata majibu au majibu yake siyo ambayo yalitarajiwa, yaani hayakutosheleza vile tulivyojibu, lakini ninazo nukta za Mhe. Saleh Nassor Juma, hakuna masuala haya ambayo ameuliza sasa kwa ruhusa yako Mhe. Mwenyekiti, nifanye nini.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, nafikiri ufundi wake katika hili Mhe. Waziri, wewe yachukue hayo mambo na kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima yako tunayachukua. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Saleh Nassor Juma, mambo yanachukuliwa na kufanyiwa kazi.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, sawa ayachukue haya na pia alichukue hili la kututafutia chombo kama vile *Virgin Butterfly*. *(Makofi)*

Kifungu 0902 Mamlaka ya Usafiri Baharini-

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana wakati nilipokuwa nikichangia nilimshukuru sana mfanyabiashara marufu Said Salum Bakharesa na nilisema pia nalishukuru Shirika la Meli kwa kutoa huduma kwa meli mbili hizi kwa Unguja na Pemba. Hata hivyo, nilisema meli ya *Azam Sealink* inaondoka muda si muafaka inasubiri abiria kutoka Dar-es-salaam na kuweza kuingia abiria kwenda Pemba. Pia, nilisema siku nyengine inaondoka saa 3:30 na siku nyengine 4:00 na hata siku nyengine saa 5:00, yaani haina muda maalum kutokana na shughuli zake na hivyo, kupelekea abiria kufika usiku na abiria wote sio kama wanakaa mjini na wengine wanakwenda mashamba mbali, kwa mfano abiria wengine wanakwenda mpaka Makangale Msuka.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na hali hiyo, tukasema tufanye utaratibu meli kuondoka mapema kama inavyoondoka Meli ya *MV*. Maendeleo saa 2:00 asubuhi, kwa sababu Meli ya *MV*. *Azam Sealink* inakwenda kwa mwendo wa masaa 6 kutoka Unguja na Pemba, ikiondoka saa 2:00 asubuhi itafika saa 8:00 na mpaka ikifika saa 12:00 jioni tayari watu wameshafika nyumbani kwao.

Mhe. Mwenyekiti, tukaiomba serikali pamoja na mfanyabiashara huyu, ili iondoke mapema na kwa sababu nikazungumza tena kwenye mfano mwengine nilisema asubuhi bahari inakuwa shuwari na ikifika saa 4:00 imeshakata mkondo na kama utakuta asubuhi bahari sio shuwari, siku hiyo hakwendeki katika safari na nililiomba hilo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa Mhe. Waziri, katika majibu yake, mimi nasema alinidharau sana na alinijibu kwa kebehi, maana alisema hiyo ni mijadala ya Wajumbe tu na akamuomba radhi Said Salum Bakharesa kama aendelee hivyo. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba Mhe. Waziri, atoe msimamo katika jambo hili, ili nipate kufahamu vizuri pamoja na wananchi na sisi ni Wawakilishi wa wananchi, ndio wanaotutuma wanafika usiku wakati mwengine mpaka saa 3:00 au 4:00 za usiku, ndio wanafika hasa wanaokwenda njia kongwe na ikifika saa 12:00 hakuna gari tena. Hilo ni moja.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine nilisema katika Shirika la Meli, kwamba zamani ilikuwa meli ya *MV*. Maendeleo na *MV*. Mapinduzi, zilikuwa zinakwenda Tanga na hivi sasa Pemba na Tanga hakuna usafiri na vyombo kama majahazi vimezuiliwa kuchukuwa abiria na wananchi wetu wanakwenda huko. Je, ni lini Meli ya *MV*. Maendeleo itafanya safari ya kwenda Tanga angalau mara moja kwa wiki?

Mhe. Mwenyekiti, naomba kupata jawabu zuri.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na namuomba Mhe. Mjumbe, anijibu vizuri kwa sababu majibu haya yote mawili nilitoa kwa ufasaha kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, nilisema hivi kwamba meli pekee ambayo inakwenda Pemba na kusubiri abiria kutoka Dar-es-salaam ni hii. Kwa hivyo, kwa sababu wale wenzetu au ndugu zetu wanaotoka Dar-es-salaam na wanataka kuunganisha kwenda Pemba. Kutokana na hali hiyo, tunaomba wananchi wawavumilie na wao, kwa sababu wangeteremka hapa inabidi wateremke na mizigo yao yote waliyokuja nayo na waingia kwenye gari waende majumbani na halafu wakatafute tiketi ya siku nyengine kama meli ya *Azam Sealink* inaondoka siku ya Jumatano na inakwenda tena Jumamosi wakae mpaka Jumamosi au wapande Meli ya *MV.* Maendeleo siku ya Ijumaa pengine.

Mhe. Mwenyekiti, lakini ile Meli ya *Azam Sealink* imewarahisishia kwamba wanaoteremka kwenye boti kutoka Dar-es-salaam wanaingizwa moja kwa moja kwenye meli ya *Azam Sealink*. Kwa hiyo, ile gharama ya usafiri inawapungukia, sasa tuwavumilie ili na wao wenzetu waweze kusafiri.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la pili, kwa sasa Pemba hali ilivyo gari ni nyingi mno za abiria. Hivyo, inatosheleza watu kufika, sasa yote mambo mawili ni kuvumilia. Kwa hivyo, mtu ambaye anahisi wakati unapokuwa na ushindani wa kibiashara anayehisi anataka kwenda mapema *MV.* Maendeleo ipo. Pia, anayehisi kwamba atapanda ile meli ya *Azam Sealink*, lakini meli ya *Azam Sealink* imeweza kuwarahisishia wale abiria wanaotoka Dar-es-salaam na kwenda Pemba na kwetu sisi tunaotoka Unguja kwenda Pemba pengine ni zito, lakini kwa wale wanaotoka Dar-es-salaam wanataka kuwahi Pemba, kwao ni faraja na ni neema. Kwa hiyo, na wao tuwavumilie ndivyo nilivyolijibu.

Mhe. Mwenyekiti, suala la meli ya *MV.* Maendeleo kwenda Tanga. Kwa kweli suala hili pia nimelijibu kwamba Bandari ya Tanga ina kina kidogo cha maji. Kwa hiyo, hairuhusu meli itakapofika ikafunge isubiri mpaka maji kujaa na wakati wa kutoka vile vile na abiria sasa hutakiwi uwashushe kwenye matishali au kwenye mashua, isipokuwa wanataka uende moja kwa moja, lakini hivi sasa *MV.* Maendeleo ni meli ya kibiashara kwa sababu Mashirika ya Serikali yanatakiwa yafanye biashara. Kwa hivyo, inapokwenda Pemba, ili siku ya pili iondoke ikiwa itakwenda Tanga haiwahi kurudi kwa wakati ule na itabidi safari zote zivurugike.

Mhe. Mwenyekiti, bado tunaendelea kuzungumza na wawekezaji mbali mbali kwa ajili ya kuweza kupata usafiri halisi wa Pemba na Tanga ambao hautokuwa na matatizo, lakini bandari ya Tanga ndio inayokwamisha bado haijakuwa *developed*. Hivyo ndivyo nilivyojibu na namuomba Mhe. Mjumbe, akubaliane na majibu haya ambayo ni sahihi kabisa.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, bado sijaridhika na majibu ya Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, hata kidogo. Nadhani Bandari ya Tanga si mgeni na kuna meli kubwa kuliko meli ya *MV.* Maendeleo na zinafunga gati. Sasa hapa alivyonijibu wakati wa kutoa majumuisho pale alisema kama atapoteza ratiba au wanasubiri meli mpya itakapokuja ndio ratiba itakwenda Tanga, lakini ninasema abiria kutoka Pemba kwenda Tanga tuhurumiwe ni abiria kama wanaotoka Unguja kwenda Pemba. Pia, wanayo mahitaji yao.

Mhe. Mwenyekiti, haya ninayoyazungumza sio kutoka kichwani kwangu, isipokuwa ni kutoka kwa wananchi, kwa sababu wanapata usumbufu na vyombo vyote vya majahazi vimepigwa marufuku kuchukua abiria. Kutokana na hali hiyo, Mhe. Waziri, tunamuomba kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, atupangie safari ya Tanga angalau mara moja kwa wiki, kwa mfano kuna meli ya *MV.* Sepide na *MV.* Mapinduzi zilikuwa zinakwenda na leo sababu gani meli ya *MV.* Maendeleo isiende Tanga.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, nilisema hapa kwamba tunamshukuru Said Salum Bakharesa kwa kutupatia usafiri huu, lakini muda si muafaka. Namuomba Mhe. Waziri, atofautishe Morogoro na Dar-es-salaam katika miji yake, yaani yeye akiteremka Mkoani gari yake ipo na mimi pia ninayo gari yangu na Waheshimiwa Wajumbe wote wanazo gari zao, lakini watu wengine hawana gari wanafika usiku. Kwa maana hiyo, tuangalie na ile ni biashara, mtu yeyote anayetaka kwenda safari yake atajua meli gani na inaondoka saa ngapi, lakini kusema kama inawasaidia wenzetu kule abiria hajipangii mwenyewe, lakini ukipanga safari unaondoka saa 2:00 wataondoka hiyo saa 2:00 na ambaye yuko Dar-es-salaam atajua siku fulani ninawahi meli ya *Azam Sealink* atakuja kwa muda muafaka, ndivyo ilivyo. Hivyo, namuomba Mhe. Waziri, kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, anipe jibu sahihi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, kabla sijamtaka Mhe. Waziri, atoe majibu sahihi, naomba nitoe maelezo kidogo. Waheshimiwa Wajumbe, unajua hivi vyombo vya *private*, serikali inayo nafasi yake kutoa maelekezo, lakini serikali

haiwezi kutoa amri moja kwa moja, kwamba fanya hivi na taratibu zetu za Kanuni juu ya jambo ambalo serikali halina mkono moja kwa moja hairuhusiki kuzuia fungu. Hilo moja, lakini la pili, Mhe. Waziri, amesema kwamba na hili nalo ni muhimu tunazungumzia sasa meli yetu ya *M.V.* Maendeleo, meli ya serikali, lakini imetakiwa ifanye shughuli zake kibiashara.

Waheshimiwa Wajumbe, hatuwezi tukatoa amri ya moja kwa moja kwamba iende Tanga mara au mbili kama itakuwa hakuna abiria, sasa hiyo maana yake tutakuja kutia hasara, haya mambo lazima tuyaangalie katika pande zote. Chombo hiki si vyema kije kitoe maamuzi kuelekeza chombo cha serikali, hatimaye inaangukia hasara huku na ndio maana nikamwambia Mheshimiwa hebu chukua mambo hayo yakafanyiwe kazi, ndio maana yake hiyo.

Waheshimiwa Wajumbe, hili la vyombo vya *private,* inabidi aanze kurekebisha utaratibu wa safari zake kuanzia Dar-es-salaam, sasa hiyo si kazi ya Mhe. Waziri, anaweza kumpa taarifa hiyo akawa na *Management* yake akatizama na atafanya utaratibu gani ili abiria wanaotoka Dar-es-salaam, wanafika Unguja waondoke muda gani kule ili sasa iwe kuna nafasi ya namna ya kuja kuunganisha kwenda Pemba ili wasifike usiku, hiyo itabidi anaweza kupeleka ujumbe huo akapeleka salamu hizo, lakini *Management* kule ikae ifanye kazi, kwa sababu zile si meli zake yeye. Nazungumzia meli za Bakhresa, yetu hii ambayo tunataka pia vile vile iende kibiashara anaweza kuchukua ujumbe, lakini tutizame kama hakuna *volume* ya kutosha ya abiria wanaokwenda Tanga utaipelekaje meli? Mhe. Waziri, chukua haya ukayafanyie kazi. Tuendelee.

Kifungu 0902

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, hoja yangu ya kwanza nashukuru sana, *actually* umeijibu vizuri sana, kwa sababu sisi tunatakiwa tumshukuru zaidi huyu Sheikh Said Salim Bakhresa na ninaweza kumwita Mheshimiwa kwa sababu alishawahi pia kuwa Mshauri wa Mhe. Rais hapa Zanzibar, lakini hapo hapo nataka kusema juu ya hiyo hiyo kwamba mimi niliwahi kufanya ufatiliaji wa hii *route* yake kutoka Zanzibar kwenda Pemba. Hii anatufanyia ihsani kwa sababu haimlipi *route* hii kabisa, lakini anatufanyia ihsani kubwa sana ya kwamba takriban asilimia 20 ana-*subsidize* anafidia kutokana na *route* hiyo, r*oute* inayolipa ni Zanzibar/Dar-es-salaaam na ndio maana ana-*subsidize* kutoka Zanzibar Dar-es-salaam *route* kwenda Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, lakini naomba nije kwenye hoja yangu niliuliza swali dogo tu katika kifungu hiki cha mamlaka ya usafiri baharini 0902 ambayo nitaomba ninukuu kidogo hotuba ya Mhe. Waziri. Ukurasa wa 43 kifungu cha 100 kinasema hivi:-

> "Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, mamlaka imepanga kukusanya jumla ya Tanzania shilingi bilioni 1.38 na kutumia jumla ya shilingi bilioni 1.359 kwa matumizi ya kazi za kawaida ikiwemo ruzuku ya Tanzania shilingi milioni 300,000,000 ya mishahara ya mamlaka'.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hizi milioni 300,000,000 ya uzuku tunaziona hapa. Suala nililokuwa nauliza na wengine nimeuliza watendaji nje huko pia kwamba hii jumla ya Tanzania Shilingi bilioni 1.359 ya matumizi iko wapi? Mimi nataka kufahamishwa hivyo tu, kwa sababu nimeitafuta sana sikuiona. Inawezekana ile 1.38 bilioni ya makusanyo ipo kule kwenye kifungu kikuu cha makusanyo, lakini kule tukiangalia tutaona ni kwenye milioni mia nne na kitu haijafikia hata bilioni moja. Sasa huku kuna matumizi ya bilioni 1.359 na kule kuna mapato ya 1.38 yote mawili siyaoni haya. Sasa ningependa kuelekezwa kwa sababu tunapitisha vifungu hapa vya matumizi na mapato viko wapi hivi? Ahsante.

TAARIFA

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali: Mhe. Mwenyekiti, mimi napenda kutoa taarifa kwa Wajumbe kupitia kwako kwamba kuna malalamiko kwamba tokea hivi jioni wananchi wamekosa huduma hizi tunazozifanya hapa, huko mjini na sehemu mbali mbali hawazipati, labda nimuombe tu Mhe. Waziri, anayehusika akatupa taarifa hii kwa sababu vyombo havionekani huko kwa wananchi ambao wanakosa haki yao.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru, namuomba Mhe. Mahmoud, ajue kwamba hili ni Shirika. Kwa hivyo, lina uwezo wa kutumia mapato yake moja kwa moja na hii ni ruzuku kutoka serikalini.Kwa hivyo, inachanganya na ile mpaka hapo watakapojiweza moja kwa moja, kwa sababu hili Shirika linalelewa, ndio linapata ruzuku. Kuna baadhi ya mashirika hayapati tena ruzuku.

Mhe. Mwenyekiti, sasa Mhe. Waziri, anazidi kunichanganya zaidi, amenambia hili ni Shirika na huku hii ni Mamlaka, yaani *Authority*, Mamlaka ya Usafiri Baharini kwa Kiengereza *Marine time Authority* ni mamlaka, Shirika inakuwa *Corporation*. Katika kitabu chake pia ukurasa wa 40 imeandikwa Mamlaka ya Usafiri Baharini. Kwa kuwa nilifanya uchambuzi wa kina wa suala hili, nimewauliza na wenzangu wataalam walionipita kwa *experience* kwa miaka, ujuzi na uzoefu ndani ya Baraza hili na wao pia wakanijibu kwamba kwa kuwa sasa hivi haya ni mamlaka hesabu zake zinakuwa tofauti na kule zamani, ndio maana kule kuna maziro mengi na Katibu wako amelikwepa eneo lile hajalisoma.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani kanikubalia kurasa zile amezikwepa kama kurasa mbili amezipita hakuzisoma. Mhe. Waziri, ananambia sasa hivi ni Shirika tena kidogo hapo amenipoteza, kama ni mamlaka ina matumizi yake nioneshwe tu yako wapi na mapato yake yako kwenye kifungu gani? Hapa inaoneshwa ruzuku tu ya serikali, kwenye kitabu kizima nimeshatafuta tayari. Kwa hivyo, sijasimama kuzungumza mazungumzo ya mitaani tu. Nimesimama kuuliza baada ya kufanya upembuzi huo. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti, arudie kwenye ukurasa wa 42, niliposema kuhusu Shirika, nilikosea kidogo, lakini nilikusudia chombo kinachojitegemea. Ni mamlaka kama Shirika, matumizi yake yako *independent*, lakini ukitizama ukurasa wa 42 ndipo iliposemwa Mamlaka ya Usafiri Baharini kwa mwaka huu ilikadiria kukusanya hiki na mwaka 2014 yapo makusanyo yake na matumizi yake. Sasa mimi sijakufahamu suala lako labda uulize zaidi.

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Mhe. Mwenyekiti, ahsante, naweza kuchukulia katika jibu lake Mhe. Waziri, labda kwa sababu hajanifahamu swali langu, mimi naomba nisirudie swali, lakini naweza kuchukua katika jibu lake kwamba hizi bilioni 1.38 na bilioni 1.35 hazimo kabisa katika kitabu hiki tuchukulie hivyo.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, nasema zipo katika ukurasa wa 42, kifungu 98 zipo hizo. Mamlaka ya Usafiri Baharini kwa mwaka 2013/14 pana pesa zake za makusanyo na matumizi na hadi kufikia mwezi Machi, imetumika hiyo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mahmoud, unauliza kwenye hili *vote book.*

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunifahamu.

Mhe. Mwenyekiti: Imo kwenye kitabu, lakini huku hakuna. Kwenye *vote book* hamna. Sasa hoja yake.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, hii ishakuwa ni mamlaka. Kwa hivyo, haiingii tena humu, hapa kifungu kimetajwa kwa sababu ya ile ruzuku tu iliyotolewa na hapo utaona katika kifungu alichotaja yeye ni ile ruzuku iliyotolewa kwa sababu ruzuku inatolewa katika Mfuko Mkuu wa Serikali, ndio inaingia Mashirika mengine au Mamlaka mengine ambayo hayapati ruzuku hata hamna kabisa, lakini hii ni mamlaka inayolelewa sasa hivi. Kwa hivyo, inapata ruzuku ndio kikatajwa kifungu hiki. Kwa hivyo, ile *total amount* haitokei katika *vote book,* tulikuwa hatujafahamiana mpaka limetajwa *vote book.*

Mhe. Mwenyekiti: Unakusudia kusema 300,000,000 ni ruzuku inayotolewa na serikali kwa mamlaka hii, sio bajeti yake yote.

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba tuendelee, lakini nitakuja kwako wewe baadae, tena unifahamishe vizuri zaidi, kwa sababu hivi sijafahamu bado. Nitakuja kwako wewe na kiti chako ili unifahamishe zaidi na makatibu wako labda nitapata elimu kidogo. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Hapana, usichukue hilo jukumu, wacha tuendelee, lakini uwafate ofisini.

Kifungu 0902	Mamlaka ya Usafiri Baharini-	300,000,000
Kifungu 1001	Idara ya Mawasiliano-	179,527,000
Jumla ya Fungu-		**5,600,078,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na
Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu 0301 Ofisi Kuu Pemba- 19,716,998,000
Kifungu 0401 Idara ya Mipango na Sera-

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu hapa ni moja tu na nikipatiwa ufafanuzi, nadhani sitakuwa tena na sababu ya kuendelea. Nianze katika mchango wangu niligusia pia na kama alivyokiri mwenyewe Mhe. Waziri, suala la Uwanja wa ndege wa Pemba na katika kitabu cha Mhe. Waziri, katika miradi ya maendeleo aliyoitaja kwenye ukurasa wa 17, kuna mradi aliyouita uimarishaji wa huduma za Uwanja wa ndege wa Pemba. Kuna maelezo mengi sana, lakini miradi mengine yoyote aliyoitaja imetengenewa fedha nyengine hata zile fedha za kutafutia fedha pia zimewekwa, lakini mradi huu hauonekani.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naogopa yale tutokuja kumwambia baadae mwakani kwamba tunapewa maelezo hewa. Mradi ulitajwa ndani ya kitabu na ukifika pahala pakutajwa ndani ya hotuba ya bajeti, tayari ni mradi wa maendeleo ya serikali, lakini katika fedha za maendeleo hakuna hata senti moja, naomba maelezo. Kuna miradi ya mikopo imewekwa. Kwa hivyo, tumeambiwa mradi huo umetolewa kwa mkopo kwa kupitia Benki ya *Exim* ya Uturuki, lakini hapa ni ziro. Naomba maelezo mradi huu utatekelezwa vipi ikiwa Baraza hili haijaidhinisha fedha zake?

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, bajeti ya maendeleo ni ule mradi ambao unatakiwa kufanywa. Kwa hivyo, tumesema kwamba mradi huu tulioutaja hapa wa *Airport* ya Pemba ni mradi uliombewa mkopo na bado yale makubaliano ya mwisho hayajafikiwa. Sasa hautojitokeza hapo kwa sababu haujafikiwa yale makubaliano ya mwisho ya kufanya ile bajeti. Ikiwa itatokezea kwamba mradi ule utapita katika kipindi hiki cha bajeti hii itabidi tutakuja hapa katika Baraza la Wawakilishi kuweza kuuombea idhini ya kuupitisha, lakini sasa hivi hatujaweza kuiingiza.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, watu wamechoka sina haja ya kukirefusha kikao hiki, lakini niiambie serikali kwamba majibu yao mara nyengine ndio yanayowaletea matatizo, kwa sababu tangu Mhe. Waziri wa Fedha wamechukua *commitment* kubwa kubwa hapa, wamewapa Wajumbe hapa kwa kuwaridhisha kwamba mradi huu unaanza mwaka huu. Mwaka jana uliombewa fedha mradi huu bilioni 2.7 ni Mjumbe wa Kamati zikatengwa milioni 900,000,000 zikachukuliwa kenda akalipwa *Mecco* Uwanja wa ndege wa Pemba ukaachwa kama ulivyo. Sasa leo anauingiza katika kitabu na naomba kwa *record* zake mwenyewe niseme *paragraph* moja katika *paragraph* nyingi alizozielezea, *paragraph* Nam. 40 inasema:-

"Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara inakusudia kuendelea na utekelezaji wa mradi kwa mkopo kupitia benki ya *Exim* ya Uturuki".

Mhe. Mwenyekiti, sasa kama hamjafikia makubaliano kutuandikia humu, si kutudanganya Wajumbe humu ndani. Mimi nadhani kama kumefika pahala mazungumzo yanaendelea, ungetupa taarifa hiyo Mhe. Waziri wa Fedha asubuhi katoa maelezo mwanana na fasaha ya Vikokotoni anatu-*convince* Baraza kwamba mradi huu utatekelezwa mwaka huu kwa mkopo ambao haupo, bado unazungumzwa na sasa Mhe. Waziri, anatwambia majibu yale yale, sasa nasema atwambie moja, ama aufute katika kitabu hiki, tujuwe hapo utapopatikana serikali, inaruhusiwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar kuleta nyongeza *supplementary budget* itatuletea hapa tutaidhinisha, lakini kutuingizia humu kitu ambacho hakipo, ni kuendelea kuwadanganya wananchi wa Pemba na kuendelea kutudanganya sisi Baraza la Wawakilishi kwamba tuendelee kujenga matumaini ambayo hayapo.

Mhe. Mwenyekiti naomba kauli ya serikali, mradi huu upo au haupo na kama bado fedha zake hazijakubaliwa, maana yake haupo asitudanganye.

Mhe. Mwenyekiti: Nadhani tungesubiri kidogo tukamaliza hii kazi, kwa sababu tunapotoka namna hiyo, maana yake sasa *quorum* ya maamuzi mnaiteteresha. Niwaomba walioko nje, basi warudi ili tumalize kazi hii.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, inaelekea kuna makosa katika uchapaji wa hiki kitabu cha *vote book* kama ambayo yalijitokeza mwanzo. Kwa sababu fedha hizi zipo na zimetajwa bilioni 2.9 kwa ajili ya uendelezaji wa Viwanja vya ndege ambacho kimoja ni cha Pemba. Kwa hivyo, kuwa hazionekani hapa inaelekea kuna matatizo ambayo yalizungumzwa mwanzo kabisa katika utayarishaji wa hivi vitabu.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hivyo, Mhe. Waziri, tunafanyaje katika hali hiyo.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, haya ni matatizo ya Wizara ya Fedha, basi tuamueni hapa tutafanya nini. Sisi tumetaja katika kitabu chetu cha bajeti kwa sababu zipo.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa tunapitisha nini kuhusiana na hoja ya Mhe. Ismail Jussa Ladhu.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, sina hakika tatizo liko wapi? Lakini kama nilivyosema mimi napata wasi wasi kwa sababu kama kweli ni matatizo ya Wizara ya Fedha au ni serikali kwa jumla kwamba mnatudanganya, kwa sababu miradi mengine yote hata katika hotuba ya waziri alipomalizia akatutajia na fedha anazotuomba, mfano mradi wa barabara wa zinaingia Mjini Zanzibar, umeombewa shilingi milioni 50 katika hotuba imetajwa huku naona, lakini hata katika hotuba yake hii hakutwambia hapa utaona maelezo mpaka yamefika mwisho, yanazungumzia baadae jumla ya fungu lote lilokuwemo katika miradi hiyo nishaisoma *paragraph* ya 41, inazungumzia miradi ya usafiri wa anga kwa jumla yake.

Mhe. Mwenyekiti, hiyo 2.9 aliyoisoma Mhe. Waziri, labda inawezekana kachoka sana leo, hiyo haihusu Mradi wa Uwanja wa ndege wa Pemba, hiyo *paragraph* 41 inazungumzia jumla jumla ya miradi ya usafiri wa anga iliyoko wizarani kwao. Bado nasisitiza kwamba mradi wa Uwanja wa ndege wa Pemba na hata haiwezi kuwa ni 2.9 kwa sababu alivyotwambia Mheshimiwa hapa kwamba kuna fedha nyingi hakututajia kima. Kwa hiyo, nasema watwambie ukweli mradi huu kama haupo, wasiwadanganye wananchi, watudanganye sisi Wawakilishi wa wananchi, wasikidanganye chombo kikubwa kama hiki.

Mhe. Mwenyekiti, kama mradi huu utakuja itakapokuwa serikali ina-*commitment* ya mkopo, kama bado mazungumzo yanaendelea watuandikie, lakini kutwambia wizara itaendelea na utekelezaji wa mradi ambao hauna hata senti moja, huko ni kuwadaganya wananchi kupitia chombo hiki. Naomba waziri aifute *paragraph* hii tuendelee na bajeti hii.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, kama alivyosema mwanzo pale kwamba *commitment* ya serikali ni kupata mkopo kutoka *Exim Bank* ya Uturuki na Uturuki imesha-*confirm* huo mkopo. Kwa hivyo, itakapopatikana kwa sababu sasa hivi tunataka kueleza *amount* gani, bado haijafikiwa yale makubaliano ya *construction cost* na mkopo utatoka kiasi gani.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema chombo hiki kina utaratibu wake na namna ya uendeshaji wake na tunaongozwa na Katiba, Sheria na Kanuni zetu. Sasa kama nilivyosema mradi ambao ingekuwa hotuba yake inatwambia tu kama serikali inatafuta sawa, lakini serikali imechukua *commitment*, ndiyo hilo ninaloliogopa mimi na Wajumbe wengi wameridhika hapa baada ya kupewa maelezo kwamba mradi huu unakwenda kutekelezwa mwaka huu, unaenda kutekelezwa mwaka huu, wakati hauna hata senti moja mazungumzo yanaendelea, huko hakuna kitu cha kushika.

Mhe. Mwenyekiti, sasa ndiyo maana nasema ingelikuwa ni mradi ambao una mkopo unajuulikana kama ilivyokuwa mengine yote hapa miradi mingi unaiona iko katika *foreign loans*, kuna fungu lake. Kwa hivyo, nasema kama tayari una *commitment* hatuwezi kupitisha hivyo bila ya kupata marekebisho ya hilo, lah, kama haupo, basi tuambiwe kama haupo. Kwa hiyo, akae katika *record* ili kitabu chake *paragraph* hii ifutwe.

Mhe. Mwenyekiti, hatuwezi kupitisha maneno hewa hapa yakuweza kuwadanganya wananchi, halafu haya ndiyo yanatuletea matatizo, kwa sababu sisi tunachukua haya tunakuja kuihoji serikali mwakani, mtakuja kutupiga maneno tena hapa. Kwa hivyo, ninachosema itwambie hapa ndani mradi kama hauna *commitment* ya fedha, bado mazungumzo yanaendelea ufutwe mpaka itakapopatikana *commitment* ya *loan*, kuna utaratibu wa kuleta bajeti ya *supplementary* hapa watatuletea kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti: Hebu Mhe. Waziri wa Nchi, kuna maneno gani hapo juu ya jambo hili, maana hii lazima sasa tujue serikali itafanyaje hapo itakapofikia kwamba sasa mchango wa serikali unatakiwa wakati huku, hakuna chochote tutazitoa wapi pesa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mhe. Jussa, kwa ku-*raise* hoja hii ambayo maelezo yako yanayo ukweli, kwa sababu kwenye kitabu hiki haioneshi fedha ambazo zitasaidia katika kuendeleza mradi huu ambao kiundani ni kweli kama maelezo ya Mhe. Wazir, kwamba serikali

imefanya jitihada kubwa ya kuendeleza mradi huu na ni kweli maelezo ya Mhe. Waziri, kwamba tumeshafikia katika hatua za mwisho wao na *Exim Bank* ya kule Uturuki kwa msingi wa kuendeleza mradi huu. Kwa kuwa na mradi huu pia unafanywa na *private sector* kutoka Uturuki, sasa kwa njia moja ama nyengine kwa kuwa hapa maelezo hayapo, lakini kwenye kitabu cha Mhe. Waziri ameeleza vizuri, ni vizuri tukubaliane na hii hoja anayosema Mhe. Jussa, kwamba kwa kuwa bado serikali inaendelea kulifanya jambo hili.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo, dhamira ya serikali kufanya jambo hili na pale mara tutakapokubaliana na wenzangu, basi tutazungumza na serikali ili ifanye utaratibu kutoka mfuko mkuu wa serikali ili tuweze kuendelea na mradi. Kwa msingi huo, tunaweza kupunguza maelezo yaliyomo kwenye kitabu kwa kuwa kwamba mradi huu utaendelea kuufanyia shughuli ili kuhakikisha kwamba kiwanja hiki cha Pemba kitajengwa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, mimi kama serikali imekubaliana na hoja yangu sina maelezo zaidi, napendekeza na nashukuru kwamba wamekubali kuwa maelezo haya yafutwe hapo itakapokuwa tayari wana-*commitment* watatumia Katiba yetu, watatumia Sheria ya *Public Finance*, watatumia Kanuni zetu kuleta bajeti ya nyongeza inaruhusiwa kuombea mradi huu idhini ya Baraza, lakini kwa sasa hivi hatuwezi kupitisha maneno, ahsante sana. Tuendelee.

Kifungu 0401 Idara ya Mipango na Sera- 129,519,456,000
Kifungu 0701 Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara-

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, katika Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara, kuna Mradi unaoitwa Ujenzi wa Barabara za Mjini Unguja (*Construction Town Road*) umeombewa milioni 50. Katika mchango wangu niliuliza kwamba fedha hizi ni za nini? Kwa sababu kimsingi mradi huu bado haujapata ufadhili wa aina yoyote uwe mkopo, iwe ufadhili na wizara imetwambia inaendelea kuutafutia. Sasa kwa kadiri ninavyokumbuka kwa bajeti za miaka iliyopita, ulishaandikiwa mpaka *feasibility study*, lakini kama ni suala la kuendelea kutafuta mfadhili, nadhani hiyo ni shughuli ya kawaida ya wizara.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo, bajeti yake inapaswa kubebwa na bajeti ya *recurrent* ya wizara na shughuli za kawaida za watendaji wa wizara. Sasa nilitaka kujua hizi milioni 50 za nini na nataka kulijua hilo, hasa kwa sababu Idara hii hii naidai milioni 40 za Jimbo la Mji Mkongwe ambapo mpaka sasa hivi Mhe. Waziri, anatupiga chenga, barabara zetu hajatujengea katika Mji Mkongwe, lakini bado wamezitafuna milioni 40 zetu na hapa kuna milioni 50 zinaombwa hatujui za kazi gani. Naomba maelezo.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, maelezo tulikwishayatoa kwamba ni *follow up find* ya huo mradi, bila ya kufuatilia hatuwezi kupata kitu, kuna wakati inabidi usafiri, kuna wakati inabidi ukutane na wafadhili. Imeelezwa katika majibu yangu kwamba ni *follow up find* hiyo ya kufuatilia, *Otherwise*, itakuwa hau-*take off.*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, mimi naridhika kama fedha hizi hazina matumizi tuziondowe.

Mhe. Mwenyekiti, nimesema tena hayo maelezo aliyoyatoa Mhe. Waziri, yanathibitisha hoja yangu niliyotoa wakati nachangia, kwamba kumekuwa na utaratibu wa kuwekwa fedha udoho udoho kama hizi katika miradi kama hii, kila mwaka mara unaambiwa shilingi milioni 50, milioni 100 zinapigwa wizarani huko, halafu hakuna chochote, zinaendelea kuombwa nyengine. Shughuli ya kusafiri, shughuli ya kukutana na wafadhili, ni shughuli ya *recurrent* ya wizara, bajeti yake inahudumiwa na *recurrent*. Huwezi ukawa na fungu la maendeleo shilingi milioni 50, eti za kusafiri za kwenda kutafuta mfadhili, hakuna utaratibu huo.

Mhe. Mwenyekiti, utaratibu huu ni mpya, lakini si mpya, ni taratibu zilizozoeleka miaka mingi, utakuta *feasibility* zinaendelea miaka na miaka kila mwaka kunapigwa milioni 50, milioni 100. Sasa na huu unataka kufanya utaratibu huo, kama maelezo yake ni hayo, basi afadhali ziondoke zirudi katika mfuko mkuu wa serikali, kuna mahitaji yanakosa fedha, shughuli ya kutafuta mfadhili kama ni kusafiri wana fungu lao la safari, fungu la *recurrent*, fungu la vikao vya Kamati vyote, tushapitisha, hatukuhoji humu wakafanyie kazi hiyo, hizi milioni 50 hazina sababu zifutwe. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, hakuna kitu ambacho kinaweza kufanyika bila ya fedha, fedha tulizoziripoti zinazoingia za *OC* kazisikia yeye mwenyewe, *fifteen to twenty percent*. Sasa

ikishatokea hiyo haja-*vote* hiyo utaipata wapi? Kwa hivyo, lazima kuwe na *vote* ambayo inaku-*guarantee* kwamba huo mradi utafuatiliwa. *OC* sasa zikifika inabidi uitishe kikao umpe nani na umuache nani. Sasa hizi kweli ni fedha za ufuatiliaji wa mradi zinatosha, ndiyo maana kikaombwa kifungu hicho ili kuwekwa kwa sababu *special* ya huu mradi, ni muhimu sana kwa sababu mji wetu unatanuka na barabara zishafanyiwa *feasibility studies*. Kwa hivyo, namuomba Mheshimiwa akubali…

Mhe. Mwenyekiti: Hebu chukua maelezo zaidi hapo.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, nimepata la ziada kwamba hii ni pamoja na ulipaji fidia wa barabara ya Mwanakwerekwe/Makaburini hadi Kwarara urefu wa kilomita 1.75.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani una haki hasa kukipongeza chombo chake hiki cha Wawakilishi kwa kazi zilofanyika humu ndani. Hii ni uthibitisho tena kadiri yakitoka maelezo yanathibitisha kwamba fedha hizi zimewekwa, zina madhumuni yao wanayajua wenyewe watendaji wake. Utawezaje kulipa fidia mradi ambao wa kipande kidogo cha barabara tele nilizozitaja katika kitabu hiki ambazo zinaingia katika mradi wa barabara za Mjini.

Mhe. Mwenyekiti, labda ili nimsaidie akumbuke vizuri aangalie katika kitabu chake hiki katika ukurasa wa 11 Mradi wa Barabara zinazoingia Mjini Unguja ametaja barabara sitaki kupoteza muda wako Mheshimiwa kuisoma hapa, unambie kuna fidia hapa, fidia hii imetokea wapi? Ndiyo yale yale mambo ya fidia tushawahi kuyapigia kelele humu ndani yanavyotumika, fidia unalipa una mfadhili, mradi unakwenda mkavunje nyumba, mnakwenda kulipa fidia ya nyumba, mradi ambao haujaanza hata mfadhili hauna. Mimi nasema ndiyo maana mwanzo alikuwa na maelezo tofauti anasema za kufuatilia safari sasa hivi anatwambia za kulipa fidia.

Mhe. Mwenyekiti, fedha za namna hii zinawekwa mara nyingi wanazijua watendaji wanavyozifanya na akiniambia kwamba suala la kufuatilia ufadhili ni kwa sababu ya *OC*. *OC* hata hizi hana hakika atazipata hii ni bajeti, tunapitisha bajeti ya mwaka huu zote tulizokuwa tumezitaja, hata haya mabilioni yote hatuna hakika kama yatapatikana haya, *priority* inategemea itakavyoingia na itakavyotumika. Fedha hizi hazina maelezo na ni bahati mbaya sikulisimamia tu na kwa msingi huo huo nina wasi wasi hata zile milioni 500 zilizoombewa mradi wa Mpigaduri, lakini sitaki kurudi huko.

Mhe. Mwenyekiti, ninachosema hapa, narudia fedha kama hizi mara nyingi zinawekwa hazina maelezo, ukiomba hupati chochote. Naomba fedha hizi zirudi katika mfuko mkuu wa serikali zitahudumia mambo mengine. Hapa hapana maelezo huwezi ukalipa fidia mradi ambao haupo na wala haujaanza kwa sababu hauna kitu, huwezi ukasafiri kwa fedha za maendeleo, kwa sababu kusafiri ni sehemu ya *recurrent*, bajeti yake tayari ipo haipatikani hilo ni suala jengine halihusiani kabisa. Huwezi ukawa na fedha katika fungu la maendeleo kwa ajili ya kusafiri au kulipia fidia mradi ambao haujaanza. Naomba sana hizi fedha zirudi, nawaomba wenzangu waniunge mkono katika hili fedha hizi zirudi katika mfuko mkuu wa serikali. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ehe! Tunafanyaje anachoomba ni kwamba kwa kuwa hakuna maelezo mazuri kuhusu fedha hizi, zirudi kwenye mfuko mkuu, ndiyo anachosema Mhe. Ismail Jussa Ladhu pale.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, sisi tushatoa maelezo yetu. Kwa hivyo, kama hakuna maridhiano urejeshwe fedha zipo hapa hapa pao.

Mhe. Machano Othman Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Mwenyekiti, nakumbuka mwaka jana tulikuwa na kadhia kama hii, Ofisi ya Rais Baraza la Mapinduzi kuna fedha tukazuia, lakini hatukuziondoa. Kwa hivyo, naomba na hizi tuzuie, lakini tusiziondowe tukipata maelezo mazuri waachiliwe waendelee nazo kuliko kuziondoa moja kwa moja wakati watu wa Wizara ya Fedha hawapo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nasikitika nafikiri suala hili tuliamua tuendelee tusicheleweshe kikao, kadhia aliyoizungumza Mhe. Waziri wa Nchi Asiye na Wizara Maalum, haifanani kabisa na kadhia hii, kadhia ile ilikuwa inahusu shamba la JKU, wala si mwaka jana, ni tangu mwaka juzi aliitoa Mhe. Mtando, sisi wengine akili zetu ziko timamu bwana, tunakumbuka kila alilolipitisha la miaka mitano iliyopita, ukiniuliza tunalikumbuka humu ndani. Zilizuiwa kwa sababu palikuwa na mashaka juu ya mradi ule, hizi hapa, hapana mradi mpaka sasa hivi kwa sababu hakuna mfadhili aliyepatikana na maelezo naona yanabadilika kila wakati na kusema

kwamba zikae, hilo tunalihalalisha kwamba anaamua nani umuhimu wake? Wanaamua watu wa fedha ambao wanajiona wenyewe ndiyo wao wako wao kama alivyotwambia kwa ufedhuli Mhe. Waziri, hapa kwamba ziko kwao hizi ikiwa watazitaka watazivuta watumie tu.

Mhe. Mwenyekiti, nasema fedha hizi zifutwe katika sehemu hii irikodiwe katika *Hansard* hapo na naomba wenzangu mniunge mkono kwani hazina maelezo hizi. Kuna Hospitali hazina madawa kunahitajika fedha, kuna mambo chungu nzima yanahitaji fedha, milioni 50 zinaweza kuonekana si nyingi, lakini kwa huduma za msingi zinaweza zikasaidia pahala pengine. Naomba sana hii katika maelezo ziondoke, mradi utakaopata fedha watatumia fedha zao za *recurrent* kutafuta mfadhili na anayehusika kutafuta mfadhili ni hao, siyo Idara ya Ujenzi, ni Idara ya Mipango, Sera na Utafiti watapozipata hizo wakampata mfadhili watatafuta fedha nyengine watakuja kutuomba kwa sasa ziondoke.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, sisi tulivyokubaliana ziende kujenga barabara ya Kiwani kama hapa hazina maelezo mazuri, basi zisiondoshwe katika mfuko ule, lakini zitakwenda kwenye barabara ya Mgagadu/Kiwani.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, anaendelea kutucheleweshea kikao tu. Serikali haiendeshwi namna hii yakuamua pale kwamba ziende katika mradi gani. Mimi nilidhani angalau angeniambia zile 40 zangu za Mji Mkongwe alizozitafuna atazitumia hizo akanitengenezea barabara zangu ili kuondoka na fedheha kwamba leo Mhe. Mwakilishi wa Mji Mkongwe kenda kumuomba Mhe. Waziri Magufuli wa Muungano asiyehusika na mambo ya mawasiliano hapa kuja kutujengea barabara, yeye amezitafuna fedha zetu hasa ule Mgagadu/Kiwani, haya ni kuhalalisha tu kwamba zibakie, watutumia vipi, wanajua wao, mimi siliwafiki hilo, kama nilotoa hoja nasema fedha irudi Hazina, ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, tuliamua hili ili tuweze kumaliza kwamba fedha hizi kwa kuwa hakuna maelezo zaidi…

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum: Nadhani Mhe. Waziri, ametoa maelezo yakutosha, lakini wazo la Mhe. Ismail Jussa Ladhu, kwamba hizi pesa zirudi kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina. Nadhani zikirudi kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina huu mradi ukiwa tayari tutakwenda huko kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina tukaziombe tutazitumia. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hiyo, tunakubaliana kwamba fedha hizi ziende Mfuko Mkuu wa Hazina, nadhani uliseme Mhe. Waziri, itapohusu mradi uko tayari atajenga hoja. Kwa hiyo, sasa tunatoa shilingi milioni 50 kutokana na kilichopo hapa, ni sawa.

Kifungu 0701 Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara- 10,904,456,000

Mhe. Mwenyekiti: Ukitoa shilingi 50 milioni ambazo zinarudi kwenye Mfuko wa Hazina, tunakubaliana?

Wajumbe: Ndio.

Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa naomba muongozo wako, kwa sababu kitaratibu bajeti kuu ya serikali ishapita na zile fedha zishaidhinishwa, tunapotaka kuondosha tunatumia utaratibu upi? Kuzuia ni sawa, lakini kuziondoa, naomba muongozo wako.

Mhe. Mwenyekiti: Mimi nafikiri hizi pesa zikienda Mfumo Mkuu bado ile *sum total* itabakia vile vile ambayo hatimaye itakuja katika *proportional bill,* itabaki ile ile, isipokuwa sasa Mfuko Mkuu huo utakuwa umeongezewa pesa hizi. Sasa wale watendaji wa fedha waelewe hilo kwamba hii sasa inakwenda huko, lakini kimsingi sio kwamba sasa kutakuwa kuna kitu kimepotea potea aa, zina Mfuko wake pahala, ndio zinatiwa na ndicho tulichokubaliana hapa, mradi ukiwa tayari watajenga hoja.

Jumla ya Fungu- 160,140,910,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kulikuwa na kazi moja ndogo ambayo ilikuwa tuifanyie maamuzi kabla hatujamaliza shughuli yetu, ambayo Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, alikwishaitolea ufafanuzi juu ya suala zima la *X-Ray Machine* na suala la ununuzi wa *Troll* na suala la nidhamu juu ya Mkurugenzi wa Mamlaka kwamba salamu hizo atazifikisha kwa Mhe. Rais, lakini hata vikao vya bodi pia Mhe. Waziri, mwenyewe alisema kwamba hilo atalifuatilia na hoja zote hizi zilikuwa zimetoka kwa Mhe. Panya Ali Abdalla. Sasa serikali iliahidi kwamba mambo haya yatafuatiliwa na kimsingi hasa hoja ile ya *X-Ray Machine* kilichoelezwa ni kwamba imetumika sheria kwa sababu ya dharura.

Waheshimiwa Wajumbe, sasa tukiacha jambo hili, kulikuwa na hoja ya kuunda Kamati Teule tukasema basi tutakaporudi hapa itakuwa kazi ya kwanza hata kabla ya kumwita Mhe. Waziri, ili kuomba makisio yakubaliwe. Nilipotoa maelezo hayo nilisema kwamba Mhe. Hamza Hassan Juma, mtoa hoja atazingatia juu ya hoja yake hiyo na haja hiyo baada ya kuzingatia kwa makini sana yale maelezo ambayo yametolewa na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Mhe. Hamza Hassan Juma sasa nimerudi kitini nakusubiri.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena nakushukuru kunipa nafasi hii na mimi nataka niseme tu kwamba suala la Mamlaka ya Mkurugenzi haliko kwenye Mamlaka ya Baraza la Wawakilishi. Kwa hiyo, nimemuachia Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, ili walishughulikie katika utaratibu wa kawaida. Sasa hilo lililobakia la *watchdog* lile, kama kazi yetu Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kusimamia utendaji wa serikali, basi bado tuendelee tupate nafasi ili twende tukaisimamie vizuri serikali katika utendaji. Nakushukuru sana.

Mhe. Spika: Sijui kama nimefahamu sawa sawa kwamba unakubaliana kwamba serikali ikafuatilie hayo kwa ujumla wake.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kuna hoja mbili, suala la nidhamu kuhusu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka nimemuachia Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kama alivyosema atalibeba, nalipeleka kwa ajili ya suala zima la nidhamu. Suala la tuhuma za ubadhirifu na ukiukwaji wa sheria za manunuzi na matumizi, hilo nitaomba tuliundie Kamati Teule ili kwenda kukagua na kuja kutoa ripoti. Kwa hivyo, naomba sasa utuulize wale wataokubaliana na kuundwa Kamati Teule ili kwenda kuchunguza fedha ambazo tunahisi hazijatumika vizuri na taratibu za kisheria ambazo hazijatumika vizuri. Hii hoja ya pili, naomba uturuhusu tupige kura kwa ajili ya kuunda Kamati Teule. Ahsante.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache, naomba kutoa hoja ili Baraza lako tukufu lipige kura kwa ajili ya kwenda kuisimamia serikali katika utekelezaji wa shughuli za kila siku. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hoja ya Mhe. Hamza Hassan Juma, ni kwamba iundwe Kamati Teule ili kufuatilia masuala ya manunuzi yale ya *X-Ray Machine*, lakini vile vile ununuzi wa *Troll*.Mmoja anasema hiyo anamuachia kazi Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Sasa hoja hiyo imetolewa na maelezo ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, mliyasikia niwahoji basi, wale wanaokubaliana na hoja hii ya kuunda Kamati Teule wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokataa wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa kwa kukataliwa)

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha ya wizara yangu bila ya mabadiliko au pamoja na mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri, mabadiliko yapo, sema pamoja na mabadiliko.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha ya wizara yangu pamoja na mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza iliyakubali makadirio hayo. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, naomba sasa niwahoji wale wanaokubaliana na makadirio haya pamoja na mabadiliko wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, ni dhahiri kwamba mmefanya kazi kubwa sana, nataka niwashukuru wote Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Waziri na Naibu wake, Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Mawaziri wengine wote, lakini niwashukuru zaidi Waheshimiwa Wajumbe, kwa kuwa makini kufuatilia masuala mbali mbali hatimae tukafikia hapa tulipofikia, nawapongeza sana na ni jambo jema hapo, tulipofikia nafikiri kila mmoja ameridhika na kile kilichopitishwa hapa. Basi baada ya hayo machache, sasa niahirishe kikao hiki hadi tarehe 16 siku ya Jumatatu saa 3:00 barabara za asubuhi.

(Saa 4:11 usiku Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 16/06/2014 saa 3:00 asubuhi)